**30 JANUARI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA PILI

**Kikao cha Nne – Tarehe 30 Januari, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Nimwite Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 50

**Kuongeza Ajira Kupitia Miradi ya Kimkakati**

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuongeza ajira kwa wahitimu wa vyuo kupitia miradi ya kimkakati, viwanda vidogo, vya kati na programu za ubunifu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Washa *microphone*.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO (MHE. RAHMA R. KISUO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa nafasi hii. Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mlezi kwa siku ya leo na siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninapenda kumshukuru Jemedari wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani isiyo kifani kwangu kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, na Mahusiano. Nimwahidi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu Mkuu nitafanya kazi hii kwa dhati, ari na uthabiti ili kuleta matokeo bila kusahau ushirikiano mzuri sana na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu swali zuri la Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, na Mahusiano, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inahakikisha wahitimu mbalimbali wa vyuo wanapata nafasi za ajira kupitia miradi ya kimkakati inayotekelezwa nchini kwa miaka ya hivi karibuni, ambapo zaidi ya ajira 35,000 zilizalishwa katika ujenzi wa Reli ya *SGR*, zaidi ya ajira 10,000 katika Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, zaidi ya ajira 10,000 katika Ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere la Kuzalisha Umeme, zaidi ya ajira 1,500 katika Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, Dodoma, zaidi ya ajira 1,500 katika Ujenzi wa Daraja la JPM (Kigongo – Busisi), na zaidi ya ajira 3,000 katika upanuzi wa Bandari Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali imetoa mafunzo ya uzoefu wa kazi maarufu kama *Internship* kwa wahitimu 29,902 wa ngazi mbalimbali za elimu pamoja na kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi 19,075 katika sekta za hoteli, madini, usafirishaji, kilimo na usindikaji wa mazao ya kilimo kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii inalenga kuwapatia walengwa ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko la ajira. Vilevile, Serikali imeandaa Mwongozo wa Taifa wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahitimu kwa lengo la kuweka utaratibu wa utoaji wa mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa wahitimu ambao unatumika waajiri wote (Sekta ya Umma na Sekta Binafsi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imeandaa Mwongozo wa Kujitolea katika Utumishi wa Umma wa Mwaka 2025 ili kuweka utaratibu rasmi wa kuwapata na kuwasimamia vijana wanaojitolea katika Taasisi za Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati mingine iliyochukuliwa na Serikali inajumuisha, kutoa mikopo yenye masharti nafuu na ruzuku kupitia mifuko ya uwezeshaji kwa wahitimu wanaoanzisha biashara, na kutoa mafunzo ya ujasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nishukuru kwa majibu mazuri ya Wizara, na niipongeze Serikali kwa sababu kuna uwekezaji mkubwa sana umefanyika katika sekta ya elimu. Kuna mikakati mingi imefanyika na Serikali ya Awamu ya Sita, lakini nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, pamoja na miradi hii ya kimkakati kutoa ajira kwa vijana, je, Serikali ina mpango wa kuweka Sera au miongozo itakayolazimisha miradi yote ya

uwekezaji kutenga asilimia maalumu ya ajira za kitaalamu kwa wahitimu hawa wa vyuo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO (MHE. RAHMA R. KISUO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na mwuliza swali 100% kuwa miradi ya kimkakati imeonesha uwezo mkubwa wa kuzalisha ajira. Hata hivyo, Sera za Ajira zinaelekeza ajira zitolewe kwa ushindani bila kutoa upendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Kazi, Ajira, na Mahusiano inaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni (Na.1) ya Mwaka 2015, ambapo pamoja na mambo mengine inaelekeza wafanyakazi wa kigeni yaani wataalamu kurithisha ujuzi kwa wazawa katika ajira za kitaalamu ili pale kibali cha kazi cha wageni kitakapokwisha, mzawa aweze kuchukua nafasi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele kwa wafanyakazi wazawa katika miradi ya kimkakati kwa nafasi za kazi ambazo utaalamu wake siyo adimu katika soko la ndani ya ajira. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nimekuona, Mheshimiwa *Eng.* Fadhili Chilombe.

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeuliza swali la nyongeza kwenye Swali Namba 51.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Mheshimiwa unataka kuuliza swali la nyongeza? Endelea, jitambulishe kidogo.

**MHE. ASHA J. FERUZ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu ni Asha Juma Feruz, Mwakilishi ninayewakilisha kundi la Vyuo Vikuu. Ninaomba kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mkakati gani maalumu katika kutumia fursa za ajira katika kundi la vyuo na vyuo vikuu kupitia mahusiano ya kikanda na kidiplomasia tuliyonayo hasa zile kozi tunazoziita *rare professionals? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO (MHE. RAHMA R. KISUO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na vyuo na vyuo vikuu, imeanzisha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wanaoendelea na masomo katika ngazi mbalimbali za elimu za vyuo na vyuo vikuu na vyuo vya kati ikiwa ni sehemu ya mtaala ili kuwawezesha kuhitimu elimu katika ngazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali inatoa Mafunzo ya *Internship* yanayojumuisha wahitimu wa ujuzi wa ngazi mbalimbali za elimu hususan elimu ya juu na kati ambapo wanapatiwa fursa ya kujifunza kwa vitendo mahali pa kazi. Lengo la mafunzo hayo ni kuwapatia wahitimu ujuzi, maadili ya kazi, uzoefu na kufanya kazi za taaluma zao na kuwawezesha kuajirika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea swali linalofuata, bado tuko Ofisi ya Waziri Mkuu. Nimwite sasa Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini, aulize swali lake.

Na. 51

**Ubovu wa Barabara Manispaa ya Morogoro**

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD** aliuliza:-

Je, lini kero ya Barabara za Mitaa katika Manispaa ya Morogoro ambazo ni mbovu hususan katika Kata za Bigwa, Mkundi na Lukobe itakwisha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul–Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 Serikali imetenga shilingi milioni 380 kwa ajili ya matengenezo ya barabara katika Kata za Lukobe na Bigwa, ambapo katika Kata ya Lukobe, Barabara za Kilombero – *Mazimbu Farm* kilometa moja, Tushikamane kilometa moja, *Cape Town* kilometa 1.6, Nzimale kilometa moja, na Lukobe kilometa 0.6 zitajengwa kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027 kupitia Miradi ya Benki ya Dunia, Serikali inatarajia kutekeleza ujenzi wa Barabara ya Kilombero – Mazimbu *Farm* kilometa sita kwa kiwango cha zege ambapo kwa sasa taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri zinaendelea kwa ajili ya kufanya usanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Bigwa, Barabara ya Vituli kilometa 0.45 itawekwa tabaka la zege kwa shilingi milioni 92.52. Aidha, katika mwaka 2025/2026, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.04 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi za Barabara ya *Suluhu New City* kilometa moja kwa kiwango cha lami katika Kata ya Mkundi. Utekelezaji wa mradi huu upo hatua za manunuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood. *(Makofi)*

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ninataka nimwambie, hali ya Barabara za Manispaa ya Morogoro, kata 26 zote ni mbaya mno, zimeathiri uchumi wa Manispaa na barabara zote hazipitiki. Kuna magari yanayokwenda shuleni hayafiki, kuna magari madogo

yanayokwenda majumbani mwa watu mitaani hayafiki, wanashusha kwenye *main road*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa aliyoisoma Mheshimiwa Naibu Waziri ipo kwenye Ilani. Sasa tunataka kujua kama wananchi wa Morogoro, ni lini watatekeleza ahadi hiyo ambapo hali ya kiuchumi katika Manispaa ya Morogoro ni mbaya kutokana na barabara hizo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro ni miongoni mwa mikoa ambayo ina urefu mkubwa wa barabara ambazo zinahudumiwa na *TARURA* kwa takribani kilometa zaidi ya 6,400. Serikali imekua ikitenga fedha kwa kadiri zinavyopatikana na kadiri ambavyo Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi imeahidi, na kwa kadiri mipango na bajeti ya Serikali zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aingie madarakani amekuta bajeti ya *TARURA* katika Mkoa wa Morogoro ikiwa na shilingi bilioni 8.7, leo tunavyozungumza bajeti ya *TARURA* kwenye Mkoa huo ni shilingi bilioni 26.7. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara zilizotajwa tutaendelea kuzitengea fedha kwa kadiri ambavyo mipango yetu ya Serikali inaruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa TAMISEMI kumwelekeza Meneja wa *TARURA* kipindi hiki ambacho tuko kwenye maandalizi ya bajeti, wazingatie vipaumbele vya Mheshimiwa Mbunge, ndugu yangu Abood, na nimpongeze sana kwa ufuatiliaji makini wa Barabara za Manispaa ya Morogoro. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini

Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Mogitu – Balang'dalalu kwa kuwa ni barabara muhimu kwa uimara wa uchumi katika nchi yetu na hasa Jimbo la Hanang? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge wa Hanang kwa kadiri ambavyo ipo kwenye mipango yetu na Ilani yetu ya uchaguzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joshua Nassari, swali la nyongeza.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona, nina swali moja tu kwa upande wa Serikali. Wilaya kongwe ya Arumeru Makao Makuu yake ni Halmashauri ya Mji Mdogo wa *Usa River*. *Fortunately,* kwa miaka yote Halmashauri ya Mji Mdogo ule haina hata kilometa moja ya lami katika Mji wa *Usa River*. Tulitenga kilometa tano, na wananchi wakafanyiwa *sensitization* na Wizara kwa ile teknolojia mbadala ambayo imefanyika kwenye maeneo mengine, lakini *unfortunately* ile ya kwetu ya Meru haikujengwa kilometa tano pale Mji wa *Usa River*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali. Ni lini jambo hili litakwenda kutekelezwa ili na yale maandamano ambayo mwaka 2025 kabla sijawa Mbunge yaliyowatoa wananchi wa *Usa River* kwenda kwa Mkuu wa Mkoa kwa sababu yasifanyike tena? Wananchi walishafanyiwa *sensitization* na kuachia maeneo yao na hakuna *component* ya fidia. Ni lini barabara hizi zitatekelezwa *(five kilometers)* kwenye Mamlaka ya Mji Mdogo wa *Usa River*? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri kwamba nimefika kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbunge, tuliambatana naye kwenda kufanya

ukaguzi kwenye barabara ambayo tunaijenga kwa kiwango cha lami. Hivyo hivyo, kama ambavyo tumefanya jitihada kwenye barabara ile tuliyoikagua, tutaendelea kufanya jitihada kama Serikali kuhakikisha tunatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo ili wananchi wa Arumeru na Makao Makuu ya Jimbo hilo *Usa River* waweze kupata huduma nzuri za barabara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine Kapoma, swali la nyongeza. Mheshimiwa Kunti Majala, Mheshimiwa Josephine ninaona hayupo.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nina swali dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahaa! Kumbe upo! Endelea.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Je, Wizara ina mkakati gani wa kuja na *solution* ya kudumu, na hata kama siyo ya kudumu japokuwa ya muda mrefu kwa zile barabara zinazozibwa viraka? Kwa mfano, kuna baadhi ya barabara unakuta zina mashimo, lakini zinazibwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa ninataka kujua kama tunaweza tukapata *solution* ya kuziba viraka ambavyo vitakaa kwa muda mrefu kwa ajili ya ku-*save* pesa ambazo zinatumika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mbunge wa Mkoa mzima wa Morogoro aliyetoka kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupa maelekezo sisi *TARURA* ndani ya Serikali kwa ajili ya kuanza mkakati wa kutumia teknolojia mpya ambayo itajenga barabara zetu kwa gharama nafuu na hivyo tutaweza kuyafikia maeneo

mengi na kujenga barabara zinazodumu kwa muda mrefu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa huu Mkoa wa Morogoro ambao Wabunge wake wameuliza maswali mengi hapa, Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana, tumejenga mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami na sasa tumefikisha karibia kilometa 125. Mradi wa *TACTIC* ambao tulitekeleza kwa awamu ya kwanza tulipeleka zaidi ya shilingi bilioni 19. Mheshimiwa Rais lengo lake ni kutaka kuona anaufungua Mkoa huu mkubwa ambao ni muhimu kwa uchumi ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa muda. Jimbo la Chemba, Barabara ya kutoka Kwa Mtoro – Sanzawa mpaka Mpendo, barabara hii imekuwa ikipangiwa fedha kila mwaka wa fedha, lakini utekelezaji wake umekuwa ni wa kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza, barabara hii mawasiliano yake ni ya shida sana kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha. Nini mkakati wa haraka na dharura kwa ajili ya kwenda kurejesha mawasiliano ya wananchi hawa ambao wanaendelea kupata adha kila mwaka na Serikali imekuwa ikitenga fedha hii kwa ajili ya kuwahudumia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mbunge wa Jimbo la Chemba, tangu amehamia Chama cha Mapinduzi, anatekeleza majukumu yake vizuri na kwa kweli hata swali aliloliuliza linazingatia Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Tutampa ushirikiano Mheshimiwa Mbunge katika kuijenga barabara hiyo kadiri fedha zitakavyopatikana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Barabara za Bunda ya kutoka na kwenda Mihingo na ya kutoka Kurusanga kwenda Mikomalilo, karibu barabara tano zote zimeharibika, lakini majibu tunayopata kutoka mkoa na Wilaya, wanasema vibali vya barabara hizo vimesimama mpaka wapate kibali kutoka Makao Makuu ya *TARURA*. Je, ni lini kibali hicho kitatoka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali haijasimamisha vibali vya ujenzi wa barabara ambazo tumeshazipitisha kwenye bajeti zetu. Tulichofanya ni tumetangaza zabuni kwa awamu na huo ni utaratibu wa kawaida wa kibajeti. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Getere, Mbunge wa Bunda, tutakamilisha kazi hiyo ya ujenzi kwa kadiri ambavyo tumezitangaza hapo awali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ninaomba kwanza sekunde chache. Majuzi niliomba Mwongozo hapa na kwa kuwa, nimeshawasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Madini tumekubaliana mambo yataenda sawasawa. Ninaomba niondoe maombi yangu ya Mwongozo ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba niulize swali dogo. Mheshimiwa Naibu Waziri anasema hawajazuia vibali. Jimbo la Tarime Vijijini Bajeti ya Mwaka 2025/2026 fedha zote za tozo na jimbo, mikataba haijasainiwa hata mmoja. Wamepitia *process* zote, mikataba haijasainiwa na mvua imenyesha hakuna mawasiliano. Ninaomba Kauli ya Serikali sasa hivi asubuhi hii. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Jimbo ambao upo kwa kila jimbo tumekuwa tunapeleka fedha kupitia Mfuko wa Matengenezo ambao upo kwenye kila jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunapeleka fedha kupitia Mfuko wa Tozo ya Mafuta ambapo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa maeneo haya ya barabara aliuleta hapa na tukaupitisha na hivyo kuifanya Bajeti ya *TARURA* nchi nzima ikatoka shilingi bilioni 275 na ikaenda zaidi ya shilingi trilioni moja. Lengo ni kwa ajili ya kuzifikia barabara kama hizi ambazo amezitaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, barabara hizi tunakwenda kuzijenga kwa kadiri ambavyo tumezitengea fedha kwenye bajeti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa *Engineer* Fadhili.

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwenye Jimbo la Tunduru Kusini, ninakotokea, kuna barabara kuu mbili ambazo ni muhimu sana kwa uchumi wa eneo lile. Barabara ya kwanza inaanzia Misechela – Namasakata – Tuwemacho mpaka Mjini; na ya pili inaanzia Mtina – Nasya – Tuwemacho mpaka Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye barabara hizi kila moja ina eneo korofi. Kwa mfano, hii inayoanzia Mtina – Nasya kuna eneo linaitwa Lamitado, pana kipande cha kilomita kama moja hivi ambayo mvua ikinyesha korosho hazipiti pale, magari yanalala pale hata siku tatu, siku nne. *The same* kwa upande wa Namasakata, kwenye Daraja linaloanzia Namasakata kwenda Chemchem, kuna kipande kina changamoto ambapo korosho ndiyo zinatoka nyingi, lakini huwa tunapata tabu kuzipitisha pale.

**MWENYEKITI:** Swali lako?

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kupata Kauli ya Serikali, ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba, maeneo yale yanapata suluhisho la kudumu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Tunduru Kusini, jana wakati anatoa hoja hapa alitoa elimu kubwa sana ya umeme kwa Mheshimiwa Ado Shaibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara hizi za Tunduru Kusini, maeneo yote korofi sisi tunayafahamu na tunakwenda kuyafanyia kazi. Tumefanya hivyo kwenye maeneo mengi ya nchi yetu kwa kutumia miradi mbalimbali, ukiwemo Mradi wa *Agri Connect,* pamoja na Mradi wa *Rise*. Vivyo hivyo, tutaangaza macho kwa ajili ya wananchi wa Tunduru Kusini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mko wengi sana ambao mnahitaji kuuliza maswali. Kwa hiyo, tusaidiane, ulizeni maswali kifupi ili wengi wapate kuuliza. Maswali kifupi na majibu ninaomba yawe mafupi.

Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Tarime ni miongoni mwa maeneo ambayo yanapata mvua ya mara kwa mara, na hivyo kusababisha barabara kuharibika na kuathiri shughuli za maendeleo na uchumi za Mji wa Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kujua, nini mkakati wa Serikali wa kulingana na mazingira ya Halmashauri ya Mji wa Tarime ya mvua ya mara kwa mara, kujenga barabara ambazo zitastahamili hali ya hewa ya Mji wa Tarime ili wananchi wa pale waweze kupita muda wote kwenye barabara zao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Barabara za Tarime ni kama ilivyo hali ya Barabara za Mji wa Morogoro. Mpango ambao tumeuweka kwenye Mkoa wa Morogoro, vivyo hivyo tutau-*extend* kwenda Tarime. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Mfaume, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona na kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Jimbo la Morogoro Kusini ni miongoni mwa majimbo ambayo yako katika hali mbaya sana ya miundombinu kwa sababu, sehemu kubwa ya jimbo hili ni milima, na hivyo, inaathiri hata *performance* yetu katika elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia takwimu za ufaulu, tuko chini na hali ya afya tuko hoi. Tuna changamoto ya Barabara ya Dakawa – Bwakila Juu, ambayo kwa kweli haipitiki kabisa. Tuna changamoto ya barabara ya Kolelo – Lukange...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali moja kwa moja.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, ni kwa kiasi gani tutapewa upendeleo maalumu kutokana na hali mbaya tuliyonayo, kwa ajili ya kuzikarabati barabara hizi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalipokea hili, na Serikali, tutalifanyia kazi kwa kadiri ya ambavyo tutapata taarifa za wataalamu wetu tukimshirikisha Mheshimiwa Mbunge. Pia ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yanayohusiana na barabara ni mengi sana na maombi yenu ni mengi hapa, na Mheshimiwa Waziri ameomba aweze ku-*clarify* zaidi. Mheshimiwa Profesa Mdoe.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuwa ndani ya Bunge hili na sote tukiwa wenye afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu, ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa Bungeni kwa kuniteua kuwa Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Pia, nawashukuru sana Wanalushoto kwa kunileta humu Bungeni na kuwa mwakilishi wao. Ninawashukuru sana na ninaahidi kwamba, sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia maswali mengi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kutoka kwenye maeneo yao ya uwakilishi. Ni kweli, hali ya mvua iliyonyesha, imeleta taharuki kidogo na kusababisha maeneo mengi ya barabara kuwa na shida kidogo ya kupitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara, tumewaelekeza wenzetu wa *TARURA* ambao wako ndani ya Wizara yetu wafanye *assessment* kwenye maeneo yote ambayo barabara zimekatika, ili kuhakikisha kwamba, tunapata kujua ni wapi hapapitiki? Hatuwezi kwenda kutengeneza barabara zote, lakini yale maeneo ambayo hayapitiki kabisa tutahakikisha kwamba, ndani ya muda mfupi tunapeleka fedha za *emergence* kuweza kurekebisha maeneo yale, ili Watanzania wenzetu waweze kupita kwenye maeneo hayo na shughuli za kiuchumi ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kutenga fedha kwenye bajeti ijayo kuhakikisha kwamba, yale maeneo korofi sana yanajengwa angalau kwa zege ili yaweze kupitika kwa mwaka mzima na kuhakikisha kwamba, shughuli zote za kiuchumi zinatekelezwa kwa wananchi na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Riziki Silas Shemdoe kwa maelezo hayo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Baada ya maelezo hayo nadhani maswali mengine mengi yamejibiwa tayari. Kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata. Namwita Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 52

**Fedha za Mafuta kwa Watu Wenye Ualbino**

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza: -

Je, Serikali inachukua hatua zipi kwa Halmashauri ambazo hazitengi fedha za kununua mafuta ya Watu Wenye Ualbino?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa upatikanaji wa mafuta kwa watu wenye ualbino kupitia halmashari zote nchini. Katika mwaka 2024/2025 Serikali ilitenga shilingi bilioni 8.74, kwa ajili ya huduma za ustawi wa jamii na shilingi bilioni 1.4 zilitengwa kwa ajili ya ununuzi wa mafuta maalum ya ngozi kwa watu wenye ualbino.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuzielekeza halmashauri kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya watu wenye ualbino. Katika mwaka 2025/2026 jumla ya shilingi bilioni 1.9 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya watu

wenye ualbino kwa kuzingatia sera, sheria na miongozo ya utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Ikupa, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishukuru na kuipongeza sana Serikali kwa majibu haya mazuri. Uhalisia wa *site* ni tofauti na fedha ambazo zimeelezwa kwenye jibu la msingi kwamba, zinatengwa. Nini Kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba, mafuta haya yanapatikana kwenye halmashauri na Manispaa zetu, sambamba/sawasawa na fedha zinazotengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya shilingi milioni 182 zimetengwa kwa wanufaika 14,695 waliopatiwa mafuta ya *lotion* na pia, utambuzi unaendelea kufanyika katika maeneo yote. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Stella, kwenye maeneo ambayo bado utambuzi haujafanyika, tuendelee kuwatambua. Ni maelekezo ya Serikali kwa Wakurugenzi wetu kuendelea kuwatambua wahitaji wa mafuta haya.

**MWENYEKITI:** Nilimwona Mheshimiwa Nyamizi Mhoja.

**MHE. NYAMIZI S. MHOJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa kwa kuwa, ni mara yangu ya kwanza kuongea katika Bunge hili, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kuwepo mahali hapa, Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniteua kuwa Mbunge, Viti Maalum, kundi la Wenye Ulemavu. Bila kuwasahau wapigakura wangu wote nchi nzima, ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la nyongeza ni kwamba, Wizara ina mpango gani wa kuajiri Madaktari wa Afya ya Ngozi, maalum kwa ajili ya watu wenye ualbino kwenye hospitali zote za halmashauri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa hawa watu kwenye halmashauri utasaidia kupanga bajeti ambayo wao watakuwa na idadi kamili ya mafuta na hata kufanyiwa *check-up,* siyo tu *lotion; check-up* kwa ajili ya watu wenye ualbino kwenye halmashauri zote, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Naibu Waziri, Mheshimiwa Nderiananga! Aah, samahani. Majibu kwanza, halafu Mheshimiwa Nderiananga.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita, kipindi cha kwanza na kipindi cha pili, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kundi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli tayari tumewaelekeza madaktari wote wa halmashauri ambako kuna uhitaji mkubwa wa wenye changamoto ya ngozi. Hivyo, pamoja na wataalamu wale 5,000 ambao tumewaajiri mwezi Januari, wamo ambao wanahusika na kufanya utambuzi wa changamoto hizi za ngozi, pamoja na kutoa ushauri katika matibabu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nderiananga.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA WENYE ULEMAVU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA)** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ninakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba niongeze jambo kwenye eneo la mafuta kwa watu wenye ualbino.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua uhitaji wa mafuta ya ualbino kwa watu wenye ualbino nchi nzima, lakini

ninamhakikishia dada yangu, Mheshimiwa Stella kwamba, Serikali kupitia ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya Waziri wetu, Mheshimiwa Wiliam Lukuvi, tunao Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu Tanzania ambao kwa sasa tayari tumetenga fedha. Kupitia kwenye mfuko, tuta-*push* fedha hiyo ndani ya wiki mbili, tangu sasa, ili iende *KCMC* ika-*produce* mafuta mengi zaidi yaweze kusambazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa pili kupitia wenzetu Wizara ya Elimu, tunasambaza mafuta haya kwa wanafunzi. Tunanunua, kama eneo la vifaasaidizi, moja kwa moja yanawafikia shuleni. Kwa hiyo, nawatoa wasiwasi wenzangu wenye ualbino.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema na hili la pili kidogo. Tuna hospitali ambazo ni teule, kama hospitali za kanda. Kwa mfano, kule Mwanza Bugando yanafanyika matibabu hayo ya kufanya *screening* tangu mwanzo, watoto wanapokuwa wadogo, kwa ajili ya kutambua *level* yao ya aina ya ngozi, mafuta na kila kitu ambacho wanatakiwa wapate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *KCMC,* tuna *Ocean Road* na tunaendelea kuhakikisha huduma hizi zinaendelea kusambaa hadi chini. Kwa hiyo, nawahakikishia watu wenye ualbino wasiwe na mashaka, tuko vizuri. Serikali ya Awamu ya Sita ya Mama Samia ya Kazi na Utu Tunasonga Mbele, tutaendelea kupeleka huduma kwao, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, bado tuko Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Namwita Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 53

**Ujenzi wa Zahanati Kata ya Nsalala, Shinyanga**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Zahanati Kata ya Nsalala Wilayani Shinyanga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, TAMISEMI kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetoa shilingi milioni 44.45 kwa ajili ya ukamilishaji wa boma la zahanati katika Kata ya Nsalala. Aidha, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026 imetenga shilingi milioni 22, kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, kwa ajili ya ukamilishaji. Ujenzi wa zahanati ya Nsalala utakamilika na kuanza kutoa huduma kabla ya mwezi Juni, 2026.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Esther Midimu.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la nyongeza.

**MWENYEKITI:** Aah *sorry,* swali la nyongeza. Mheshimiwa Daktari.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, nashukuru sana kwa majibu ya Naibu Waziri na kwa kazi ambayo Serikali imeanza kuifanya katika Kata ya Nsalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Shinyanga, kata zote 26, ni Kata ya Nsalala peke yake ndiyo ambayo haina hata zahanati. Kwa hiyo, kwa utaratibu huu ambao Serikali imeuanzisha, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kwa kuwa, Shinyanga *DC* ina maboma zaidi ya 56 ambayo yako katika *level* tofauti, nini mpango mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba yale maboma ambayo wananchi walijitolea nguvu na fedha zao kwa ajili ya kuyaanzisha yanakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, hata Halmashauri ya Shinyanga, majengo ya hospitali ya wilaya hayajakamilika, ni upi Mpango wa Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tupokee pongezi ambazo Mheshimiwa Mbunge Christina Christopher Mnzava amezitoa. Serikali inatambua idadi ya maboma iliyonayo katika utekelezaji wa kuyakamilisha. Tuna maboma ya vituo vya afya 341, lakini tuna maboma ya zahanati 1,841.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejipanga, kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma haya na tayari tumeanza kuyatengea bajeti pia. Kupitia fedha za ndani, tumewaelekeza Wakurugenzi wetu kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma hayo, lakini pia, fedha kutoka Serikali Kuu nazo zitakwenda kusaidia kukamilisha maboma

**MWENYEKITI:** Nilikuita Mheshimiwa Esther Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Buchambi, Wilaya ya Maswa ina wakazi wengi, lakini haina kituo cha afya. Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya kwa Kata ya Buchambi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa katika Bunge lako Tukufu tayari tulishapeleka fedha za kujenga vituo vya kimkakati katika Majimbo 120. Majimbo mengine 94 tumeshayaombea fedha Hazina, nayo yatapata kwa awamu ili kuweza kukamilisha ujenzi wa vituo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge Esther kwamba Wilaya ya Maswa ni wanufaika katika ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Nuru Issa Kashakari.

**MHE. NURU I. KASHAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, ni lini Serikali itakamilisha Kituo cha Afya cha Kazulamimba, Kituo cha Afya cha Kata ya Mwakinzega na ni lini pia Serikali…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge swali la nyongeza ni moja tu.

**MHE. NURU I. KASHAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge akiulizia kuhusu Kituo cha Afya cha Kazulamimba. Kituo cha Afya cha Kazulamimba ni pamoja na vituo vya afya 341 ambavyo tumeviainisha. Tutaendelea kutenga fedha za ndani za halmashauri na zile za Serikali Kuu ili kuhakikisha kituo hiki cha afya kinaanza kutoa huduma kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Kiza Mayeye.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Afya inataka kila Kata kuwa na kituo cha afya, lakini katika Jimbo la Kigoma Kaskazini mpaka sasa Kata za Mkongoro, Mkigo, Nyarubanda, Nkungwe, Mungonya, Kidahwe na Matendo hawana vituo vya afya na wakinamama wamekuwa wakitembea umbali mrefu kutafuta huduma ya afya. Ni lini Serikali itakamilisha sera hii kwa kuleta vituo vya afya katika Kata hizi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Kiza Mayeye, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kaskazini, kwa kazi kubwa anayoifanya hapa Bungeni ya kufuatilia maendeleo ya Jimbo la Kigoma Kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kujenga vituo vya afya katika Kata zote. Awali tulianza na zile Kata za kimkakati kulingana na mahitaji na vipaumbele. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Kiza Mayeye, ndani ya awamu hii tunakwenda kujenga vituo vya afya kulingana na vipaumbele katika Jimbo la Kigoma Kaskazini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Christina Mndeme.

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niulize swali la nyongeza. Katika Zahanati ya Imalakaseko iliyopo Kata ya Goweko, Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, Mkoa wa Tabora, Serikali ilitoa shilingi milioni 80 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya mama na mtoto lakini wodi hiyo bado haijakamilika. Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha ujenzi wa wodi hiyo ya mama na mtoto katika zahanati ya Imalakaseko, Kata ya Goweko, Halmashauri ya Wilaya ya Uyui? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amegusia hasa katika zahanati ya Imalakaseko, Halmashauri ya Uyui. Kwanza Serikali imeshatenga shilingi milioni 80 kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema. Pia, ninamwelekeza Mkurugenzi kuendelea kutenga fedha za ndani Halmashauri ya Uyui ili kuweza kukamilisha ujenzi wa zahanati hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Lukozi ni kati ya vituo vya kimkakati ambavyo vimetengewa fedha na Serikali. Ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa kituo hicho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunaipongeza Serikali kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kilipelekewa fedha shilingi milioni 250 za awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaombea wale Waheshimiwa Wabunge ambao hawajapata, yale Majimbo 94, lakini tumeshawaelekeza Wakurugenzi wote katika Halmashauri kuendelea kutenga fedha za ndani ili kuhakikisha huduma zinatoka katika vituo vyetu vya afya, na maeneo yote yenye upungufu tutayaombea fedha Hazina. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na Swali Na. 54, ninamwita Mheshimiwa Enock Zadock Koola, Mbunge wa Vunjo, sasa aulize swali lake.

Na. 54

**Kuimarisha Kingo za Mto Rau – Vunjo**

**MHE. ENOCK Z. KOOLA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaimarisha Kingo za Mto Rau na Ghona ili kudhibiti mafuriko kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Enock Zadock Koola, Mbunge wa Jimbo la Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mto Ghona na Mto Rau ni mito midogo iliyopo katika Bonde la Pangani katika kidakio cha Mto Ruvu inayoanzia kwenye mteremko wa Mlima Kilimanjaro na inapeleka maji Mto Ruvu ambao huyasafirisha na kuyafikisha katika Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za usimamizi wa mazingira kwa kulinda uharibifu wa kingo za mito hiyo ambapo mwaka 2021/2022 jumla ya shilingi milioni 552 zimetolewa kwa ajili ya kuondoa mchanga katika mito hiyo urefu wa mita 12,642. Kazi hiyo imefanyika katika Kata za Msaranga, Mjimpya, Kiboriloni, Mfumuni mpaka Kata za Kahe Magharibi na Kahe Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bonde la Mto Pangani itaendelea kuimarisha kingo za Mto Rau na Mto Ghona kwa kupanda miti, kutoa elimu ya jamii pamoja na kuweka zuio kwa wanachi wanaolima na kujenga karibu na mito

hiyo, ili kuepuka madhara yatokanayo na mafuriko wakati wa mvua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Enock Koola, swali la nyongeza.

**MHE. ENOCK Z. KOOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa kuwa changamoto kubwa iliyobainika ni upungufu wa rasilimali fedha ambapo inakadiriwa kuwa takribani shilingi bilioni moja inahitajika kukamilisha mradi huu na kwa kuzingatia umuhimu wa mradi huu kwa kulinda maisha na mali za wananchi wa Jimbo la Vunjo hususan Kata za Kahe Mashariki na Kahe Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi na muda mrefu ikiwemo utaratibu wa upatikanaji wa fedha ili kuhakikisha tatizo hili linapatiwa ufumbuzi wa kudumu tukizingatia kwamba mvua za masika zinakaribia? *(Makofi)*

Pili, je, Mheshimiwa Naibu Waziri upo tayari baada ya vikao vya Bunge tuongozane pamoja kwenda kutembelea maeneo haya yaliyoathirika ili tuweze kuchukua hatua stahiki? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge Koola, ndani ya siku 100 za Dkt. Samia Suluhu Hassan tayari ameshakwenda kwenye Mto Rau na niliona wakifanya utoaji wa mchanga zaidi ya mita 2,001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inatambua na tayari imeshaanza tathmini katika mto huo na tathmini ya awali inaonyesha uhitaji wa shilingi bilioni moja ili kuweza kujenga kingo

na kuondoa kabisa changamoto ya mafuriko katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Bonde la Pangani pamoja na wadau wa maendeleo na Halmashauri ya Moshi Vijijini wanaendelea kuzitafuta fedha hizo ili sasa tuweze kuanza kujenga mto huu kwa *phase*. Tutaanza kwa *phase* ya kwanza hasa kwenye maeneo ambayo yana maporomoko na mafuriko kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa awali ni huo na mpango wa pili wa kudumu ni kuhakikisha elimu inatolewa kwa wananchi wetu ili wasiweze kutupa taka katika mito hii na pia kupanda miti ambayo itazuia mafuriko katika maeneo yote. Pia, wananchi wamepewa elimu ya kutofanya shughuli za kilimo ndani ya mita 30 kukaribia mto huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine ni kuhusu kwenda kutembelea. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, baada ya Bunge hili tutapanga ratiba mimi na yeye twende kule kuona, lakini ninaendelea kumwelekeza Mkurugenzi kutenga fedha kwa ajili ya kufanya usafi katika mto huu, kwenda kutoa mchanga ili tusiweze kupata madhara baadaye, na kusababisha kutumia bajeti kubwa katika kuokoa majeruhi.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Simon Songe.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninaomba kuuliza swali la nyongeza. Kumekuwa kukitokea mafuriko sana katika Kijiji cha Lamadi ambacho ni mji mkubwa, na ni kwa sababu ule mto umejaa magugumaji ambayo yanasababisha mvua ikinyesha, maji hurudi kwa wananchi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta fedha ili kuyatoa magugumaji ili tuwaokoe wananchi wa Lamadi kutokana na mafuriko yanayowapata mara kwa mara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge hasa akiangazia maeneo ya Kijiji cha Lamadi. Tumewaelekeza wataalam wetu na Wakurugenzi kuweza kubainisha maeneo yote yenye changamoyo na tuweze kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua maoni na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ili kuweza kuhakikisha kwamba eneo hili tunawahi kuweka hatua ya dharura kabla hatujaenda kwenye maafa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Jamii. Ninamwita Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala, Mbunge wa Ndanda, sasa aulize swali lake.

Na. 55

**Kuanzisha Baraza la Taifa la Vijana**

**MHE. FARAJI B. NANDALA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Baraza la Taifa la Vijana?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala, Mbunge wa Jimbo la Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Vijana la Taifa linaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Taifa la Vijana, Sura ya 441. Sheria inayounda Baraza hilo, kuanzia ngazi ya Kata hadi ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mujibu wa Sheria hii, Waziri mwenye dhamana ya maendeleo ya vijana nchini amepewa mamlaka ya kutunga Kanuni chini ya Kifungu cha 27(1) kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa sheria husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni hizi pia tayari zimeshatungwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 348 la Tarehe 15 Septemba, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la uundwaji wa Baraza lilisitishwa ili kutoa nafasi ya kukamilishwa kwa Mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ambayo imekamilika na kuzinduliwa mwezi Agosti, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa mapitio ya sera hiyo, Serikali inaendelea na hatua mbalimbali za uundwaji wa baraza ikiwa ni pamoja na kuomba ushauri na mwongozo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuanza kutekeleza sheria hiyo kwa mafanikio.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Faraji Nandala, swali la nyongeza.

**MHE. FARAJI B. NANDALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa ninampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuanzisha Wizara hii ambayo ina-*deal* na maendeleo ya vijana na kumteua kaka yangu, Mheshimiwa Joel Arthur Nanauka kuwa Waziri ambaye amebeba dhamana ya vijana wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua sheria ya kuanzishwa kwa Baraza la Vijana la Taifa ni miaka 11 sasa tangu imeanzishwa. Ni miaka mingi imepita na mambo mengi yameongezeka. Ni upi msimamo wa Serikali kuhakikisha kwamba inafanya mapitio ya sheria hii upya ili tuweze kuifanyia marekebisho? Iletwe hapa Bungeni na iweze kuendana na kasi na maendeleo ya vijana ambayo sasa hivi wanayataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili kwa Mheshimiwa Waziri. Ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba Wizara hii ya vijana inakuwa na taasisi zake maalum ili iweze kukidhi matakwa ya vijana badala ya kuendelea kutegemea taasisi kutoka katika Wizara nyingine za kisekta? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maswali mazuri ya Mheshimiwa Faraji Nandala. Swali la kwanza kuhusiana na muda kuwa umepita tangu sheria hii imetungwa, Mheshimiwa Rais baada tu ya kuingia madarakani, tarehe 15 Juni, miezi mitatu baada ya kushika nafasi ya Urais, akiwa Mkoani Mwanza alitoa maelekezo mahsusi ya upitiwaji wa sera na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia maelekezo yake kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi, ni kwamba sera ya mwaka 2007 ilirejewa, na tayari imepatikana sera mpya ya maboresho ya mwaka 2024 ambayo yenyewe imezingatia mabadiliko makubwa ambayo yamejitokeza tangu sheria na sera imetungwa kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kuhusiana na taasisi, kwa sasa Wizara yetu ina vituo vitatu vya vijana ambavyo tunaamini katika bajeti ijayo vitakuwa ni sehemu ya malengo yetu ya kuvifufua. Pia, ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa sababu Serikali ni moja, tutafanya kazi kupitia Wizara na taasisi nyingine za Serikali ambazo zinabeba maslahi ya vijana sawasawa na maelekezo aliyotupatia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa *Advocate* Edwin Enosy Swalle.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Jimbo la Lupembe ambalo mimi ndiye Mbunge wake, kuna vijana zaidi ya 55% wamenituma nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo unaifanya kwenye Wizara hii ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anafanya bidii kuanzisha baraza la vijana, ni lini stakuja Jimbo la Lupembe aweze kuongea na vijana wangu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa swali zuri la *advocate* Swalle. Ninapenda kujibu na kueleza kwamba dhamira ya Serikali sawasawa na ambavyo sera ya vijana inaeleza, ni kushirikisha vijana wa kila ngazi kuanzia Taifa, Mkoa pamoja na Wilaya na Kata. Sehemu ya 2(8) ya sheria hii imetueleza kwamba kila kijana wa nchi hii anapaswa kushiriki, kusikilizwa na kutoa maoni yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba katika ukurasa wa 13 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais ameelezea umuhimu wa vijana kushirikishwa katika masuala ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumhakikishia kwamba tarehe 10 Januari, mwaka huu tulizindua *program* maalum ya kuwashirikisha vijana inaitwa *Vijana Platform* ambayo imekuwa ikizunguka katika Mikoa mbalimbali. Siyo muda mrefu nitafika Mkoani kwake na vijana wanaopatikana katika eneo lake pia watashiriki katika kutoa maoni ili kuijenga nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Jasmine Ng'umbi.

**MHE. JASMINE C. NG'UMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni upi mpango wa Serikali katika kuwasaidia vijana waliopo katika maeneo yao kutambua fursa zilizopo ili kuondokana na dhana ya kusubiri ajira? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mtandao kuanzia ngazi ya Taifa, Wilaya mpaka Kata. Tunatumia fursa zilizoko katika

Halmashauri zetu kwa kushirikiana na uongozi wa maeneo husika kuwapatia vijana taarifa hizo kupitia *program* mbalimbali ambazo zinaendeshwa na Serikali katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa kuzingatia kwamba vijana wengi wanapatikana katika mitandao ya kijamii na wanatumia teknolojia, Wizara tayari tumeshazindua mpango maalum wa kutumia teknolojia kuwafikia vijana wetu ili kuhakikisha kila kijana ambaye anaweza kupata nafasi ya kutumia teknolojia aweze kupata taarifa kwa wakati na pia kupewa usaidizi wa namna ya kuzitumia fursa hizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Sigrada Mligo.

**MHE. SIGRADA W. MLIGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu linaenda kama ushauri. Mheshimiwa Waziri kwa sasa hata hilo baraza analolitaja Mheshimiwa Waziri analijua yeye na *level* fulani huku Taifani. Ukifika kule vijijini hakuna anayejua kwamba kuna huo mkakati wa baraza. Mpango wake ni nini katika kuhakikisha hadi watu wa vijijini wanapata hiyo taarifa kwamba kuna huo mchakato unakuja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Mheshimiwa Waziri ana jitihada za kuunda hayo mabaraza ya *WhatsApp,* lakini ninamwambia ukweli, watu wengi wamejiunga kwenye hayo ma-*group* ya jukwaa sijui ya vijana na nini, lakini vijijini hawana taarifa na hawana hizo *smartphone*.

**MWENYEKITI:** Swali.

**MHE. SIGRADA W. MLIGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba hizo *program* na *project* za Mheshimiwa Waziri, taarifa zinawafikia watu wa vijijini na siyo zinapita kwenye mlengo mmoja wa kupitia UVCCM. Ahsante?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza ninapenda kutoa taarifa kwamba baraza linalozungumziwa hapa kwa mujibu wa sheria, bado halijaanza kufanya kazi. Kilichoanza ni majukwaa ya vijana ili kuendelea kupata maoni yao na kusikia mawazo yao katika ujenzi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria ya uanzishwaji wa baraza hili kama nilivyotangulia kusema katika sehemu ya 2(8) kinaelekeza kwamba vijana wa ngazi zote, kutakuwa na *level* ya Kitaifa, Mkoa, Wilaya mpaka Kata. Kwa hiyo, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba baraza hili litakapoanza, halitakuwa baraza la kutumia *WhatsApp* wala *Facebook*, ni baraza litakalogusa maisha ya kila kijana wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bila kujali kwamba kijana wa nchi hii anaweza kupata *smartphone* au hawezi kupata *smartphone,* maono ya Mheshimiwa Rais, kama alivyoeleza katika hotuba yake, ni kuhakikisha kila kijana bila kujali historia, kipato chake au anakopatikana, anahusika na kuwa sehemu ya msingi katika kutengeneza mustakabali wa Taifa letu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswal ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali, Mbunge wa Ilongero, sasa aulize swali lake.

Na. 56

**Ujenzi wa Barabara ya Igauri – Manyara**

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa barabara ya kutoka Igauri – Ilongero – Hydom Manyara kilometa 11.5 kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Naibu Waziri, Godfrey Kasekenya.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Igauri – Ilongero kwenda Hydom yenye urefu wa kilomita 93.77. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Igauri hadi Ilongero yenye jumla ya urefu wa kilometa 11.5 upo kwenye hatua za manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi atakayetekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za ujenzi zitaanza baada ya hatua ya manunuzi kukamilika na mkandarasi kupatikana. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gulamali, swali la nyongeza. Sasa ukiuliza swali, ukiwa na swali la msingi unatakiwa usimame kama una swali la nyongeza, kwa hiyo usikae.

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimeyapokea hayo; na nitakuwa na maswali ya nyongeza mawili. Ninaomba kuuliza yafuatayo: Ifahamike kwamba barabara hiyo ya kutoka Igauri kuelekea Haydom ilishatangaza zabuni miaka mitano iliyopita. Wananchi wa Ilongero walikuwa wastahimilivu sana kwa miaka yote hiyo, lakini hakuna mkandarasi aliyepatikana. Tunachoomba Wanasingida, umuhimu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gulamali, usitoe maombi, uliza swali.

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali ni kwamba, je, ni lini sasa tutaona karandinga zimepaki pale ili tuuone ujenzi kwa vitendo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ya kutoka Igauri kwenda Ilongero kilometa 11.5 ilitangazwa, na mkandarasi aliyepatikana, bahati mbaya akawa ame-*bid* kwa bei ya juu sana. Katika majadiliano ilionekana kuwa Serikali haiwezi kwenda na mkandarasi huyo mpaka tuhakikishe kwamba tunapata mkandarasi ambaye anaweza kwenda kufanya kazi kwa mujibu ama kwa bei ambazo ziko kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, ndiyo maana tumesema tutaitangaza tena hiyo barabara kilometa 11.5 ili iendelee kujengwa kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwenye ujenzi maswali ni mengi. Kuna maombi ya maswali zaidi ya 25 ya suala hili, hatuwezi kwenda hivyo. Kwa hiyo, nitatoa nafasi kwa wachache ambao nina uhakika hawajaongea au hawauliza maswali. Tunaanza na Mheshimiwa Lutengano Mwalwiba.

**MHE. LUTENGANO G. MWALWIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo kwamba Barabara ya kutoka Mbambo katika Jimbo la Busokelo kuelekea Ipinda katika Jimbo la Kyela ijengwe kwa kiwango cha lami. Barabara hii ndiyo inayounganisha Wilaya ya Rungwe na Wilaya ya Kyela kutokea Jimbo la Busekelo. Wenzetu Wakala wa Barabara *(TANROADS)* wamekamilisha upembuzi pamoja na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu, je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami, ukizingatia umuhimu wake kiuchumi kwa Wilaya ya Rungwe na Kyela?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema, Barabara ya kutoka Ipinda – Mbambo inakwenda

Tukuyu, lakini pia inakwenda Katumba. Kuanzia Mbambo kwenda Tukuyu atakubaliana nami kuwa tayari ipo kwenye hatua za ujenzi, lakini pia kuanzia Mbambo – Busokelo kwenda Katumba ipo kwenye hatua ya ujenzi na mkandarasi yuko *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kipande kilichobaki cha kutoka Mbambo kwenda Ipinda tutaiweka kwenye mpango ili iweze kujengwa, kwa sababu tayari tumeshakamilisha usanifu wa kina, ili sasa kuiunganisha Kyela na Wilaya ya Tukuyu kupitia Ipinda – Mbambo ama Katumba – Ipinda – Mbambo ama kwenda Tukuyu.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Wilson Mahera.

**MHE. DTK. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Nyankanga – Rung'abure ni barabara inayounganisha Wilaya ya Butiama na Serengeti. Je, Serikali ina mpango gani wa kuijenga kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa swali fupi. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Nyankanga Sirori - Simba kwenda Rung'abure tuko hatua za mwisho kukamilisha usanifu. Bado hatujakamilisha usanifu, lakini tuko kwenye hatua za mwisho kabisa, na baada ya hapo ndipo Serikali itajua sasa gharama ya hiyo barabara ili uweze kuitangaza kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dickson Villa.

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na mimi kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Mafinga – Mgololo katika mkoa wetu wa Iringa ndiyo barabara pekee inayounganisha majimbo matatu, yaani Jimbo la Mafinga Mjini, Jimbo la Mufindi Kaskazini na Jimbo la Mufindi Kusini. Tayari barabara hii tulishatangaziwa, mkandarasi amepatikana kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha za awali *(advance payment)* kwa ajili ya mkandarasi kuanza ujenzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia barabara…

**MWENYEKITI:** Swali ni moja, na mradi ni mmoja tu. Mheshimiwa Waziri majibu.

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara hii ni moja ya barabara muhimu za kiuchumi ambayo inatoka Mafinga kwenda Kiwanda cha Mgololo. Ni kweli kwamba ndiko ambako mbao nyingi na magogo mengi yanatoka. Hii ni moja ya barabara zile zilizokuwa kwenye Mpango wa *EPC+F* yenye urefu wa kilometa 81. Barabara hii imechukuliwa yote. Mkandarasi aliyekuwa amepatikana, ndiye huyu ambaye ataendelea kuijenga, na yuko kwenye maandalizi ya mwisho kuanza kuijenga. Kwa hiyo, tunachosubiri ni kumlipa malipo ya awali ili aanze kuijenga hiyo barabara ambayo ni muhimu sana kiuchumi.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka.

**MHE. KASSIMU A. MBARAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani sana. Barabara ya Tanga – Pangani kilometa 50 kuna kipande cha kutoka Tanga mpaka eneo la Kirare. Je, ni lini ujenzi utaanza kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga – Pangani inaendelea kujengwa na hicho kipande anachokisema tutaendelea kutafuta fedha ili tuweze kukijenga pia kwa kiwango cha lami baada ya kukamilisha barabara hiyo ya Tanga hadi pale Pangani, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mkandarasi anayejenga Barabara ya Mnivata – Nanyamba – Tandahimba – Masasi anajenga kwa kusuasua sana ilhali barabara ile ina ufadhili wa fedha kutoka Benki ya Afrika. Je, Serikali ina mpango gani wa kumsimamia mkandarasi huyo akamilishe kazi kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Tandahimba kwenda Mitesa, huyo mkandarasi tayari tumeshakutana naye kwenye vikao vya juu kujua changamoto gani ipo, kwa sababu *cashflow* haina shida. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tuna hakika mabadiliko yatatokea makubwa sana. Pamoja na kwamba tumemwelekeza kwamba, kama kuna changamoto ya menejimenti kwenye kandarasi yake, basi aweze kuwaondoa hao watu. Tunataka twende na kasi kwa sababu *cashflow* ya huo mradi haina shida kabisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Eric Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona. Barabara ya Sengerema – Nyehunge kilometa 54 imepata mkandarasi lakini bado hajapewa *advance*. Kwa sababu hiyo, hajaingia kazini, na barabara ni mbovu sana kwa hivi sasa, haipitiki vizuri. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutoa maelekezo kwa Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Mwanza ili aweze kuitengeneza kabla mkandarasi hajaingia kazini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, barabara hii ilikuwa imepata mkandarasi, lakini aliondolewa, tukatangaza tena na huyo mkandarasi amepatikana. Kwa taratibu tulizonazo mara nyingi, barabara ikiwa na mkandarasi, inakuwa yule mkandarasi ndiye anayefanya *maintenance,* kwa maana ya matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kazi ilikuwa imesimama, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama Wizara na *TANROADS* Makao Makuu waone namna ya kuhakikisha kwamba, kwa sababu ilikuwa haina mkandarasi muda mrefu, fedha itafutwe ili barabara hii iweze kufanyiwa matengenezo wakati mkandarasi anasubiriwa kuanza kazi.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Martha Mariki.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ujenzi wa Barabara ya Kibaoni – Salike yenye urefu wa kilometa 71.7 unasuasua, na barabara hiyo ni muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi na Taifa kwa ujumla. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba ujenzi wa barabara hii unakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ilikuwa inasuasua, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa tunategemea kwamba huyo mkandarasi ambaye alikuwa na vipande vingi na sehemu nyingi za ujenzi, tumeshakaa naye na kuhakikisha kwamba anaongeza kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge, kwamba tumeanza na kilometa 50 ambazo ndizo tayari mkandarasi yupo, kilometa 21 bado mkandarasi hajaanza kazi, japo ipo kwenye mpango wa kuikamilisha katika awamu hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Masanja.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Ninaomba niulize swali la nyongeza. Je, ni lini mkandarasi aliye kwenye barabara ya kutoka Hungumalwa - Ngudu hadi Magu ambaye tayari yuko *site*, ataanza kulipwa ili aendelee na kazi?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingi ambazo zilikuwa zinasubiri malipo ya awali Serikali, sasa hivi ipo kwenye maandalizi ya kuhakikisha kwamba wakandarasi wote waliokuwa *site* wakisubiri malipo ya awali wanalipwa na kazi zinaanza haraka, ikiwa ni pamoja na barabara yake ya Magu – Ngudu – Hungumalwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tutamaliza na Mheshimiwa Zacharius Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kuna wananchi wa Kata ya Mawengi na Mlangali, wakati Barabara ya Itoni – Lusitu – Manda inajengwa walikuwa hawajalipwa fidia. Je, Mheshimiwa Waziri ana maelekezo gani kwa watu wa *TANROADS* ili wakutane na mimi pale ili tuweze kuwahakiki wananchi wale na taratibu za kuwalipa fidia ziendelee?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba tu Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu barabara ile kimsingi watu wengi walikuwa wameshalipwa, sasa kama kuna changamoto, ninaomba kwanza tuanze na mimi. Baada ya hapa tukae mimi na yeye Mheshimiwa Mbunge. Pia nitamwelekeza ama ninamwelekeza Meneja wa Mkoa wa Njombe atuletee taarifa sahihi, ni kwa nini hawa hawajalipwa fidia tuweze kuwalipa kama kweli wanastahili kulipwa?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, muda wetu ni mfupi, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Tabora Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 57

**Ujenzi wa Makazi ya Askari Tabora Mjini**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga makazi ya Askari Polisi katika Jimbo la Tabora Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mambo ya Ndani, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Tabora Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi Wilaya ya Tabora Mjini ina maeneo mawili yaliyotengwa na Serikali kwa ajili ya kujenga nyumba za makazi ya Askari Polisi katika Kata ya Itonjanda lenye ukubwa wa mita za mraba 85,495 na Kata ya Ndevelwa lenye ukubwa wa mita za mraba 24,276.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosubiriwa ni kupatiwa hati za umiliki wa maeneo hayo kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, ili Serikali iweze kutenga fedha kupitia bajeti yake kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi ya Askari Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo amenipa, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Jimbo la Tabora Mjini lina nyumba za Askari lakini nyumba hizo hazina hadhi ya kuishi watu kwenye eneo hilo. Serikali inapotaka kupeleka tena ujenzi wa nyumba katika Kata ya Itonjanda na Kata ya Ndevelwa, ninadhani ni upotevu wa fedha tu, wakati kuna eneo zuri na kubwa na ni eneo ambalo ni la gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni sasa kwamba ina uwezo wa kujenga nyumba nyingine za Askari Polisi katika eneo lile lile walilokuwepo sasa ili kuendeleza makazi yake na kuonekana makazi bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Serikali badala ya kusubiri wapate hati katika maeneo hayo mawili, ambapo inaweza ikachukua muda mrefu na kufanya Askari hao waendelee kuishi kwenye mazingira duni, je, ni kwa nini maeneo hayo yasifanye shughuli nyingine za kiserikali kwa sababu tayari Askari wetu wa Tabora wana eneo rafiki kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Polisi Tabora Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, na nimpongeze sana kwa kuwa karibu na Wizara ya Mambo ya Ndani, hasa Jeshi la Polisi, na kuendelea pia kutoa ushirikiano mkubwa katika kuhakikisha kwamba maendeleo ya walinzi wetu hawa yanaendelea kuimarika hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali lake la kwanza la nyongeza, niseme tu kwamba ni kweli analolisema kwamba hilo eneo ni vyema tungelianza hapo, lakini wakati tunataka kuanza hapo vilevile tuelewe kwanza Askari hao wangelihitaji eneo mbadala la kuishi ili wakiwa wanasubiri ujenzi huo kuanza kwenye eneo walipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza jana katika maelezo yangu ya jumla kwamba Serikali inaendelea na mkakati wa kuboresha Jeshi letu la Polisi katika nyanja tofauti ikiwemo makazi, vituo katika ngazi mbalimbali. Kwa hiyo, kadhalika na kwenye eneo hili, Serikali inaendelea na kazi hiyo kwenye maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa eneo hilo ambalo amelitolea ushauri Mheshimiwa Mbunge, nasema tu kwamba tunachukua ushauri wake na tutaweza kuona namna ya kuzungumza na

wenzetu wa Jeshi la Polisi Wilaya husika ili tuone namna gani nzuri ya kuweza kuanza ujenzi mahali hapo badala ya maeneo ambayo Serikali imependekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la pili, la kwamba je, hatuoni umuhimu wa maeneo yale kuyapatia sekta nyingine kwa ajili ya kutumika kwa shughuli nyingine za Kiserikali; nilieleza pia jana kwenye maelezo yangu ya jumla, kwamba kadri ya hali ya uchumi unavyokuwa, ndivyo vilevile uhitaji wa kuimarisha ulinzi kwenye maeneo hayo unavyohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, bado ninaomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kukubaliana na Serikali kwamba maeneo hayo yaendelee kubaki kuwa Serikalini kwenye Jeshi la Polisi ili hali itakavyoendelea kupanuka kwenye shughuli za kiuchumi, basi na shughuli za ulinzi ziweze kupata maeneo ya kujenga.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo na makazi ya Askari Polisi cha Kata ya Mahore ambacho kiko ndani ya Jimbo langu la Same Mashariki, kituo hiki cha Polisi pamoja na makazi ya Polisi, vyote viwili vina hali mbaya sana. Swali hili nimekuwa naliuliza mara kwa mara, napewa majibu, lakini hakuna utekelezaji wowote.

Mheshimiwa Mwneyekiti, ninamwomba sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, ili nisiendelee kuuliza swali hili na nisiendelee kuisumbua Serikali, yeye mwenyewe aje aone hicho Kituo cha Polisi na makazi ya Polisi wa Kata ya Mahore ili tusiendelee kugombana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Malecela swali lake la

nyongeza kuhusu kituo chake cha Polisi pamoja na makazi Same Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwahidi tu kwamba, kwa sababu ombi lake ni kwamba niende nikaone, na ingawa hoja yake ya msingi ni kuhakikisha kwamba tunafanya ukarabati, kwenye suala la ukarabati namwomba aniridhie, kwani ninalo swali la msingi linalohusu ukarabati, sasa ili nisim-*pre-empty* yule ambaye nitamjibu hoja hiyo, basi asubiri majibu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mimi kwenda na yeye katika eneo lake, nimeridhia, na baada ya Bunge hili nipo tayari kupanga naye niende nikalione.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Yohana Msita.

**MHE. YOHANA S. MSITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nina swali la nyongeza. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Itigi, Makao Makuu ya Halmashauri Itigi hatuna kituo cha Polisi tangu tulipopata uhuru. Askari wetu wamejiegesha tu kwenye jengo la reli tangu miaka hiyo mpaka sasa. Je, Serikali haioni umuhimu sasa kujenga kituo kikubwa cha Polisi kwenye Halmashauri ya Itigi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Msita Mbunge wa Jimbo la Itigi na nimpongeze pia kwa kazi kubwa anayoifanya, ingawa swali la msingi kwa siku ya leo lilikuwa ni makazi ya Askari lakini hoja yake ya suala la vituo nilikuwa nimejibu jana, na jana nilitoa maelezo ya jumla…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi kwa sababu ulishalijibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa maelezo ya jumla kwamba, vituo vya polisi vya daraja C tunahitaji zaidi ya 3571 nchi nzima, lakini Serikali kupitia

Jeshi la Polisi imefanya tathmini na kuweza kubaini zaidi ya maeneo 658 ambayo yana umuhimu kutokana na hali ya usalama kwenye maeneo hayo kuweza kujengwa vituo kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza kwamba, kati ya maeneo hayo tutaanza na maeneo 196 ambapo yatakwenda kwa awamu ya kwanza halafu maeneo 213 awamu ya pili na maeneo 212 awamu ya tatu na wastani wa shilingi bilioni 79 zitatumika kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nimwombe Mheshimiwa Msita kwamba aje tukae ili tuone ikiwa hilo eneo lake lipo kwenye maeneo 658, basi tuko tayari kuliingiza kwenye mpango wa awamu ya kwanza wa utekelezaji.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Kija Ntemi.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona, hii *angle* siyo sawa sana kutuona, uwe unageukageuka kidogo na sisi unatuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru na nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi Katoro ametujengea kituo cha Polisi kikubwa sana na kiko hatua za mwisho kukamilika, tunawapongeza sana Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali inapata changamoto sana kutupatia eneo la kujenga kituo cha zimamoto? Sisi pale Katoro tumeunguliwa na majengo mengi, hata mara ya mwisho tumeunguliwa, juzi juzi tu hapa, na tuliomba eneo tujenge kituo cha zimamoto, wafanyabiashara wa Katoro wako tayari kuchangia, nami niko tayari kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri magari yanatoka Geita kuja kuzima moto, na ndiyo maana kuna siku moja niliona gari sijui lilikuwa wapi, lilipofika kwenye eneo la

kuzima moto lilichomwa moto na wananchi kwa sababu ya kuchelewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, uliza swali moja kwa moja.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je ni lini Serikali itatupatia eneo la kujenga kituo cha zimamoto ili mimi Mbunge wa Jimbo la Katoro na wafanyabiashara tuchangie kujenga kama Serikali haiwezi kutupa fedha kwa sasa, tujenge sisi wenyewe ili magari yawepo Katoro kwa ajili ya kuzima moto? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nadhani Mheshimiwa Waziri ameelewa swali liko nje, lakini ni uamuzi wako kama unaweza kujibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwa ruhusa ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge wa Katoro swali lake ambalo kama ulivyoeleza, liko nje hata ya hilo eneo, lakini nitaweza kumjibu kwa kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni kupata eneo la ardhi kwa ajili ya kuweka kituo cha zimamoto. Wizara yetu ya Mambo ya Ndani ya Nchi siyo Wizara yenye dhamana ya ardhi. Kwa hiyo, isingelikuwa mahali sahihi kuweza kujibu suala la upatikanaji wa ardhi, ila nimpongeze sana kwa jinsi ya utashi alionao wa kushirikiana na Wizara yetu kuhakikisha maendeleo yanapatikana kwenye jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nimuahidi kuwa tuko tayari kumpa ushirikiano wa kushiriki pamoja kwenda kupata hilo eneo, hatimaye tuweze kuweka kituo cha zimamoto. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Regina Malima.

**MHE. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru

**MWENYEKITI:** Samahani ulishauliza swali, nikakupa nafasi ya kuuliza swali kabla, kwa hiyo tuendelee.

**MHE. JOSEPH C. ISACK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona. Nina swali moja. Monduli ni kati ya wilaya kongwe na ukijua fika kwenye mkakati wa Serikali imeweka mkakati wa kukarabati vituo vikongwe vya Polisi, je, ni lini Serikali itapeleka fedha Monduli kwa ajili ya kukarabati makazi ya wakazi na Kituo cha Polisi Monduli?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza kwenye maelezo ya awali kwamba kuhusu suala la ukarabati wa vituo niombe nimpe haki ya mwulizaji wa awali kwa maana ya mwenye swali la msingi na ninalichukua swali lake, nitalijibu kwa pamoja na swali la mwulizaji wa awali ambaye tayari lipo Mezani na tutakuja mbele yako kulijibu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata, nimwite Mheshimiwa Adonis Bitegeko Mbunge wa Muleba Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 58

**Upatikanaji wa Vitambulisho vya NIDA - Muleba Kaskazini**

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuharakisha upatikanaji wa vitambulisho vya NIDA - Muleba Kaskazini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Adonis Alfred Bitegeko Mbunge wa Muleba Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA),* inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha upatikanaji wa vitambulisho kwa wananchi ikiwemo wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini. Hadi kufikia Disemba, 2025, jumla ya watu 254,284 wamesajiliwa sawa na 79.47% ya watu 319,972 wenye umri wa miaka 18 na kuendelea kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kipindi hicho, pia jumla ya Namba za Utambulisho (NINs) 158,547 sawa na 62.4% ya watu waliosajiliwa zimezalishwa na kugawiwa kwa wananchi pamoja na kuzalisha vitambulisho 149,920 sawa na 94.5% ya Namba za Utambulisho zilizozalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA),* inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha upatikanaji wa vitambulisho ikiwa ni pamoja na kutenga bajeti kwa ajili ya usajili wa wananchi, usambazaji na ugawaji wa vitambulisho kupitia Ofisi za Usajili za Wilaya, Kata, Shehia, Vijiji na Mitaa kwa lengo la kusogeza huduma ya usajili na utambuzi karibu na wananchi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, zipo changamoto ya baadhi ya wananchi kutochukua vitambulisho vyao na hivyo kuathiri mpango wa Serikali wa kuwapatia vitambulisho wananchi wote waliokidhi vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mathalan, katika Mkoa wa Kagera kuna vitambulisho 15,520 ambavyo havijachukuliwa na wananchi pamoja na kutumiwa ujumbe mfupi wa simu *(SMS)*. Hivyo, Nitoe Wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuwahimiza wananchi katika majimbo yao kwenda kuchukua vitambulisho vyao katika ofisi za *NIDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bitegeko hakuna swali la nyongeza, tunaendelea kwenye maswali yanayofuata. Tunakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda sana, bado tunayo maswali ya kukamilisha, Wizara ya Nishati Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly Mbunge wa Lindi Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 59

**Ujenzi wa Mradi wa *LNG* Lindi Mjini**

**MHE. MOHAMED M. UTALY** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Mradi wa *LNG* utaanza na ni hatua zipi zilizokamilika hadi sasa ili kuhakikisha Mradi huo unaanza kama ulivyopangwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati kwa niaba ya Waziri wa Nishati.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(LNG)* kwa kushirikiana na Kampuni za Kimataifa za Nishati *(International Energy Companies - IECs)*. Kwa sasa mradi upo kwenye hatua za mwisho za ukamilishaji wa majadiliano ya mikataba mbalimbali ya utekelezaji. Utekelezaji Mradi utaanza mara baada ya kukamilika kwa majadiliano hayo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED M. UTALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Je, Serikali imejipanga vipi kuanzisha ofisi ya uratibu wa mradi katika Mji wa Lindi itakayohusisha viongozi wa Serikali na mitaa na wadau wa jamii ili kuboresha mawasiliano na wananchi wa Lindi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa wananchi wa Lindi wanatarajia kunufaika moja kwa moja na mradi huu. Je, Serikali tayari imeandaa mpango maalum wa mafunzo, ajira na kutambulisha fursa za kiuchumi kwa wakazi wa Lindi kabla ya kuanza kwa hatua za ujenzi wa mradi huu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NISHATI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Utaly kwa kazi nzuri anayoifanya kwa wananchi wake wa Lindi Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ofisi ya uratibu pamoja na mpango maalum wa fursa na ajira kwa ajili ya wananchi wa Lindi Mjini, masuala yote haya yako tayari katika utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kubwa ambayo ni ya umuhimu sana katika utekelezaji ni kukamilisha majadiliano, lakini masuala yote yanayohusiana na utekelezaji yamesharatibiwa vizuri na yatafanyika ikiwemo masuala ya uratibu pamoja na mpango wa fursa na ajira hususan kwa wananchi wa Lindi Mjini pale ambapo mradi huu unaenda kutekelezeka mradi mkubwa wa zaidi ya miaka 40. Ni mradi ambao una fedha nyingi zaidi ya dola za Kimarekani bilioni 42. Kwa hiyo, wanufaika wa kwanza tunategemea wawe wananchi wa Lindi Mjini, na Serikali imejipanga kwa ajili ya suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe mashaka Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Lindi Mjini, watanufaika na mradi huu ambao una maslahi makubwa sana kwao, na pia kwa Taifa letu la Tanzania, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Wananchi wa Mkoa wa Lindi ambao ndio walengwa wa mradi huu mkubwa wa *TLNG* wana shauku ya kujua mradi huu utakapoanza utazalisha ajira ngapi kwa makadirio? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ni suala la takwimu. Kama una majibu, na sidhani kama utakuwa na majibu, lakini kwa kawaida masuala ya takwimu tunaomba sana yaje kwa maandishi au kabla.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa makadirio tu.

**MWENYEKITI:** Bunge linatakiwa litoe taarifa za ukweli na uhakika kwa mujibu wa kanuni zetu. Kwa hiyo, hatuwezi kujibu hilo swali. Tunaendelea na swali linalofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwite sasa Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando, Mbunge wa Kilindi aweze kuuliza swali lake.

Na. 60

**Kukatika kwa Umeme Jimbo la Kilindi**

**MHE. SALEHE M. MHANDO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya kukatikakatika kwa umeme katika Jimbo la Kilindi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua ya kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme katika Wilaya ya Kilindi, Serikali kupitia *TANESCO* inajenga Kituo cha Kupoza Umeme cha Kilindi na njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovolt 132 kutoka Mkata

mpaka Kilindi. Hadi kufikia Januari, 2026 ujenzi wa kituo hicho umefikia 35.9% na 30.91% kwa njia ya kusafirisha umeme na ujenzi huo umepangwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2026 kulingana na fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi hiyo, *TANESCO* inaendelea na ukarabati wa miundombinu iliyochakaa katika maeneo hayo sambamba na ubadilishaji wa nguzo za miti na kuweka za zege ili kupunguza ukatikaji wa umeme unaosababishwa na kudondoka kwa nguzo za miti kwa sababu ya mvua au kuchomwa moto.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salehe Mhando, swali la nyongeza.

**MHE. SALEHE M. MHANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa huu mradi mkubwa wa gridi imara pamoja na ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme. Pamoja na majibu hayo, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali ilivyo sasa, na kama alivyoeleza kwamba mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mw mwaka huu 2026, na hali ilivyo, kule ni hali ambayo kidogo ina changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini hatua ya muda mfupi ambayo inaweza Serikali ikachukua walau kupunguza changamoto iliyopo sasa iweze kurejea angalau iwe sawa na miezi mitatu iliyopita tofauti na hali ilivyo sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kuona ni kuamini. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuongozana nami baada ya vikao hivi vya Bunge kwenda Jimbo la Kilindi kuweza kuona na kuweka msukumo kwa ajili ya kutatua changamoto hii ya kukatikakatika kwa umeme? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ujibu swali la kwanza. Hilo la pili huwezi kum-*commit* Waziri mwenzio, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge na nimpongeze sana kwa kazi nzuri anayoifanya. Kuhusiana na hatua za muda mfupi ambazo *TANESCO* inafanya, kwanza niwape pole sana kwa kadhia ambayo wanapitia, na ni kweli Kilindi inapata umeme kutoka *substation* ambayo iko Korogwe, *substation* ya Hale, vilevile umeme mwingine wanapata kutoka Handeni, na ni laini ambayo ni ndefu sana zaidi ya kilometa 220.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Serikali ikaona umuhimu wa kujenga Kituo cha Kupoza Umeme pale ili wananchi wa Kilindi waendelee kupata umeme wa uhakika na ahadi ya Mheshimiwa Rais alivyoenda Kilindi miaka miwili iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua za muda mfupi, tayari *TANESCO* inafanya ukarabati kwenye njia ya kusafirisha umeme kuhakikisha kama ni maeneo ambayo yana majimaji, basi nguzo zile za miti zinatolewa na kuwekwa zile za zege, kwa sababu na *TANESCO* na wenyewe wamesikia, basi nina uhakika wataenda kupitia upya laini ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni ndefu sana, basi wataweka vikata umeme na kuchukua tahadhari zozote zile kuhakikisha kwa muda huo ambao tunasubiri Kituo cha Umeme kikamilike na njia ile ya kusafirisha umeme ikamilike, basi wananchi waendelee kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kilindi. Serikali inayo mikakati mizuri sana ya kuhakikisha wanapata umeme wa uhakika, na kwa hilo tutaendelea kulifanyia kazi na kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa akiwa Kilindi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nnauye, swali la nyongeza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa mikoa peke yake iliyobaki kwa nchi nzima; bara na visiwani ambayo haijaunganishwa na gridi ya Taifa, ni Mikoa ya Lindi na Mtwara, pamoja. Jitihada za Serikali kuongeza mashine za kuzalisha umeme kusini na tukizingatia kwamba sehemu ya umeme unaozalishwa katika nchi hii, gesi inatoka kusini, lakini umeme wa kusini unaweza kukatika kwa siku zaidi ya mara kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itawatoa wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara kwenye kadhia hii ambayo inaathiri maisha yetu na uchumi wetu Wanakusini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NISHATI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali zuri sana la Mheshimiwa Mbunge na nimpongeze kwa kazi nzuri anayoifanya katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mikoa ya Lindi na Mtwara ni mikoa ambayo haijaunganishwa kwenye gridi ya Taifa, na kwa sababu hiyo, Serikali iliweka mradi pale wa kuunganisha Mtwara na Lindi kwenye gridi ya Taifa kwa kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka Songea kwenda Tunduru, Mtwara hadi kufika Lindi. Mkandarasi anaitwa Kalpataro, yupo *site* na kipande cha Songea mpaka Tunduru kinaendelea vizuri na alikuwa ameshalipwa malipo ya awali kwa kipande kinachotoka Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, suala la kupeleka umeme Mtwara na Lindi lilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais alivyotembelea yeye mwenyewe katika mikoa hii wakati anafanya ziara. Tunafanya jitihada zote zinazowezekana kuhakikisha mkandarasi anaendelea kuwepo *site,* anafanya kazi kwa haraka kama tulivyokubaliana Septemba mwaka huu 2026 mradi ukamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawahakikishia wananchi wa Mtwara na Lindi, ni kipaumbele kupeleka umeme wa gridi na kuunganisha Mtwara na Lindi katika gridi ya Taifa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Waziri wa Nishati. Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 61

**Ujenzi wa Uwanja wa Ndege – Moshi**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, ni lini Uwanja wa Ndege wa Moshi utakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanja cha Ndege cha Moshi ni Kiwanja muhimu katika kuchochea uchumi wa Mkoa wa Kilimanjaro, hasa ukizingatia umuhimu wa mkoa huo katika nyanja za utalii, kilimo, na masuala ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo hayo, na kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Usafirishaji, Serikali ilianza ukarabati wa miundombinu ya kiwanja hicho, na mpaka sasa mradi umekamilika kwa 69%. Mpango wa Serikali ni kuendelea na taratibu za kutafuta fedha ili kuhakikisha mradi huo unakamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuena Bushiri.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa umuhimu wa uwanja huu katika kukuza uchumi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Taifa, je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka hizi 31% zilizobaki katika bajeti ya 2026/2027? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Zuena kwa swali lake na ufuatiliaji wake mkubwa wa Uwanja wa Ndege wa Moshi, ameuliza je, Serikali haioni umuhimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye majibu ya msingi, Serikali inatambua na kuzingatia umuhimu wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi kwa uchumi, kwa masilahi ya wananchi na nchi yetu, na ndiyo maana imeshaanza ujenzi tuko 69%. Kuthibitisha hilo, Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo kwamba miradi yote ambayo tumeshaanza kuitekeleza ikiwemo na huu lazima ikamilike, na kwenye Ilani ya CCM tumeshazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ninataka nimhakikishe Mheshimiwa Zuena ambaye anatimiza jukumu lake la msingi la Kikatiba la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 62 la kuisimamia na kuishauri Serikali kwamba, tunabeba jambo hilo tunaliingiza kwenye bajeti ijayo ili liweze kukamilika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Jacqueline Mzindakaya.

**MHE. JACQUELINE C. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia nafasi hii ikiwa ni awamu yangu ya kwanza katika Bunge hili Tukufu. Kwanza kabisa, ninaomba ridhaa yako nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia kibali kuwepo mahali hapa, lakini vilevile, kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline nenda kwenye swali. Siku ya kuchangia utasema yote hayo.

**MHE. JACQUELINE C. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Rukwa ulipatiwa shilingi bilioni 60 kwa ajili ya kujenga uwanja wa ndege. Uwanja huo utakwenda kukuza fursa mbalimbali za kiuchumi na kuwainua wakazi wa Mkoa wa Rukwa katika kipato wakiwemo wanawake pamoja na vijana. Vilevile,

utapunguza adha ya kusafiri mikoa ya jirani kwa ajili ya kupata usafiri wa ndege ikiwemo Mkoa wa Katavi na Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, ninauliza, je, ni lini uwanja wa ndege wa Mkoa wa Rukwa utaanza kufanya kazi? Ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Jacqueline Mzindakaya, Mbunge mpya, kwa ufuatiliaji wake mkubwa wa Kiwanja hiki cha Sumbawanga. Nimhakikishie, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeshaonesha nia, imeshaanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshakamilisha *Runway* (njia ya kuruka na kutua ndege), na kwa sasa tupo kwenye hatua za mwisho za kukamilisha majengo mengine, miundombinu iliyobakia ikiwemo pamoja na majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari ni mpango wa sekta ya uchukuzi chini ya Mheshimiwa Waziri wetu Mheshimiwa Prof. Mbarawa kuanza kufanya majaribio, kama siyo mwezi ujao, basi mwezi unaofuatia ili wananchi wa Rukwa, Sumbawanga waweze kunufaika na usafiri huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo tu, ninajua pia wamesimama na wa maeneo mengine. Mpango huu unakwenda pia kwenye Uwanja wa Musoma ambao nao tumeshakamilisha *Runway*, inakwenda kwenye Uwanja wa Shinyanga ambako tumeshakamilisha *Runway*. Kwa pamoja tutafanya *Testing* ili kuona tuanze kupeleka ndege yetu ya *ATCL* ianze kufanya kazi katika maeneo yote hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Tuna muda mfupi, tuna maswali saba na muda wetu ni mfupi uliobaki. Kwa hiyo, tutaendelea na maswali ya msingi.

Tunakwenda Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, nimwite Mheshimiwa *Eng.* Ramadhani Hamza Singano, Mbunge wa Bumbuli, sasa aulize swali lake.

Na. 62

**Kuanzisha Chuo cha *VETA* – Bumbuli**

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanzisha Chuo cha *VETA* Bumbuli ili kuwaongezea vijana ustadi na ubunifu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri; Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba yake.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, na Teknolojia na kwa ruhusa yako, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa *Eng.* Ramadhani Hamza Singano, Mbunge wa Jimbo la Bumbuli, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuwa na Chuo cha Ufundi Stadi *(VETA)* katika kila mkoa na wilaya. Kwa sasa Serikali inaendelea kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi katika Mkoa wa Songwe na wilaya 64 ambazo zilikuwa hazijajengewa. Halmashauri ya Bumbuli ni sehemu ya Wilaya ya Lushoto ambayo tayari ina Chuo cha *VETA* kinachoendelea kutoa mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kuendelea na ujenzi wa vyuo hivyo, Serikali pia inaendelea kutekeleza Mpango wa Ujenzi wa Shule za Amali katika halmashauri ambazo hazina Vyuo vya *VETA*. Halmashauri ya Bumbuli ni miongoni mwa halmashauri zinazojengewa shule hizo za amali ambapo shule hiyo inajengwa katika Kata ya Vuga. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Singano, swali la nyongeza.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niulize tena swali la nyongeza lenye vipengele viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Lushoto ni wilaya ambayo ina changamoto ya kijiografia, ndiyo maana ina majimbo matatu ya kiuchaguz,i lakini ina kata 51. Kulingana na changamoto hiyo ndiyo inayotupelekea tuone namna ya kuwagusa vijana wa Kitanzania ambao ni 61% kama walivyoainishwa katika hotuba ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na changamoto hiyo, watu wa Bumbuli wako tayari kutoa majengo yao ya halmashauri ambayo yalikuwa ni ya zamani sasa hayatumiki, ili Serikali isipate gharama kubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali. Bahati mbaya nilikuwa ninaongea huku, sikukuona. Uliza swali.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni sasa kwamba kuna haja ya kuwafikiria tena Wana-Bumbuli kwa changamoto hiyo ya kijiografia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jambo hili ni kilio cha Wanabumbuli, Ofisi ya Waziri iko tayari muda gani ili niambatane nayo wakaone changamoto hiyo ya kijiografia ambayo inawagusa Wanabumbuli? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi hii. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi, na Teknolojia, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake mahiri kwa wananchi wake wa Bumbuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ina azma ya kuwa na Taifa lenye maarifa, lililoelimika, lenye ujuzi, stadi, na stadi za kazi, kwa kadiri bajeti itakavyoturuhusu, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba inaendelea kujenga vyuo hivi vya *VETA* kila

wilaya, na pia katika yale maeneo ambayo hayafikiki kijiografia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Bumbuli ni moja ya maeneo hayo ambayo yamekaa vibaya kijiografia, kwa kadiri bajeti itakavyoruhusu tutaangalia namna gani ya kuweza kuyabadilisha majengo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja kuona kwamba tutaweza kuweka tawi la *VETA* katika Jimbo la Bumbuli. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Mama Salma Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninawapa pole Wana-Mchinga kwa kadhia iliyotokea jana. Kwenye Shule ya Mkwajuni madarasa mawili yameezuliwa na upepo na wanafunzi sasa hivi hawapo madarasani. Nyumba mbili za walimu zimeharibika, halikadhalika na ofisi ya Mkuu wa Shule imeezuliwa. Nini kauli ya Serikali, na nini mkakati wa haraka kuhakikisha kwamba wanafunzi wanarejea shuleni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi hii. Kwanza ninaungana na Mbunge wa Mchinga, Mama yangu Mheshimiwa Salma Kikwete katika kuwapatia pole waathirika wa maafa haya ambayo yametokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni jambo la dharura, Wizara ya Elimu itakaa pamoja na Wizara ya TAMISEMI kuona ni namna gani tutaweza kurudisha hali ya majengo haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa. Kwa kuwa Halmashauri ya Mji wa

Bagamoyo imetenga eneo na ikaikabidhi *VETA* eneo la Fukayosi Kijiji cha Mwavi kwa ajili ya ujenzi wa *VETA*, na kwa kuwa jamo hili lipo kwenye Ilani, je, Serikali ipo tayari kutenga fedha kwenye mwaka wa fedha huu 2026/2027 ili vijana wa Bagamoyo wapate stadi mbalimbali kwa ajili ya miradi ya kimkakati inayokwenda kutekelezwa ikiwemo ujenzi wa bandari?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilitenga shilingi bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa awali wa vyuo hivi vya *VETA*, lakini kwa mwaka 2025/2026 tayari Serikali imeshatenga shilingi 21,262,000,000/= kwa kwenda kumalizia ujenzi wa awamu ya kwanza, lakini pia kwa kuanza ujenzi kwa maeneo ambayo hayana vyuo hivi vya *VETA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimjibu Mheshimiwa Mbunge kuwa tayari fedha hizo zimeshatengwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwona Mheshimiwa Waziri akitaka ku-*clarify*. Bado unataka ku-*clarify* Mheshimiwa Waziri? Kwa kifupi twende, muda umeisha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi, niwape pia pole Wanamchinga hasa wale wa Kijiji cha Mkwajuni. Baada ya kupata taarifa ya kuezuliwa kwa majengo yale, nilimwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi na amekwenda pale na wanaenda kupeleka kiasi cha shilingi milioni 96 ili kurekebisha madarasa yale ambayo yameharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeshalichukulia hili tayari na ninamshukuru sana Naibu Waziri wa Elimu kwa namna alivyoliweka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Nimwite sasa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga aulize swali lake.

Na. 63

**Ujenzi wa Chuo cha *VETA* Songwe**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Songwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, na Teknolojia ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Songwe ni miongoni mwa vyuo 65 vya *VETA* vinavyojengwa na Serikali katika kila mkoa na wilaya ambazo zilikuwa hazijajengewa vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ya ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Songwe unatarajia kukamilika mwezi Juni, 2026. Hadi sasa Serikali imepeleka kiasi cha shilingi bilioni 4.140, kati ya shilingi bilioni 6.484 zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi huo. Kwa sasa ujenzi huo umefikia 70%.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianze kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana ambayo nina imani kwamba wananchi wa Jimbo la Vwawa watakuwa wamefurahi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninayo maswali mawili mafupi ya nyongeza. Kwa kuwa muda ambao umebaki kufikia mwezi Juni ni mfupi, je, Serikali sasa iko tayari kupeleka hizo fedha zilizobaki ili kusudi iweze kukamilisha hiyo awamu ya kwanza ya ujenzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, baada ya kukamilisha hiyo awamu ya kwanza ya ujenzi, ni wazi kwamba chuo sasa kitaanza. Je, ni kozi zipi ambazo zinatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2026?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, na Teknolojia ninaomba nijibu swali la ziada la Mheshimiwa Hasunga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutoa fedha hizi kama nilivyosema kwamba shilingi 21,262,000,000/= zimeshatengwa. Kwa hiyo, muda wowote kuanzia Februari, 2026 fedha hizi zitaanza kutoka ili ziende zikamalizie vile vyuo vya awamu ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ameuliza, ni kozi gani ambazo zitatoka katika chuo hicho? Kozi ambazo tunashajiisha vyuo vyetu vya *VETA* vitoe kwa maeneo ambayo vyuo hivi vinajengwa, ni kozi ambazo zinahusisha shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mkoa wa Songwe, kozi ambazo zitatolewa pale ni kozi zinazohusiana na kilimo na kuongeza thamani mazao ya kilimo. Pamoja na kozi hizo, kutakuwa na kozi mbalimbali ikiwa ni pamoja na umwagiliaji, ufugaji, ufundi magari, ufundi umeme, na kozi nyingine zote ambazo zitawezesha vijana wetu kupata ujuzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Maji. Bado tuna maswali manne, tuyamalize. Mheshimiwa Cosmas Mtesigwa Bulala, Mbunge wa Kwimba, sasa aulize swali lake.

Na. 64

**Ujenzi wa Mfumo wa Usambazaji Maji Ngudu**

**MHE. COSMAS M. BULALA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa Mfumo wa Usambazaji Majisafi katika Mji wa Ngudu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, kwa niaba yake Naibu Waziri, Mheshimiwa *Eng.* Kundo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Cosmas Mtesigwa Bulala, Mbunge wa Jimbo la Kwimba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji katika Mji wa Ngudu Wilayani Kwimba kwa kulaza bomba la kusafirisha maji kutoka Muhalo – Mwamashimba – Runele lenye umbali wa kilometa 25.4. Utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 15% na unatariajiwa kukamilika mwezi Juni, 2026. Mradi utaongeza upatikanaji wa majisafi na salama katika maeneo 14 ukiwemo Mji wa Ngudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakamilisha maandalizi ya Mradi wa Usambazaji Maji Ndani ya Mji wa Ngudu, ambapo utahusisha ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 17 na utanufaisha zaidi ya wananchi wapatao 32,000 waishio katika

mitaa 11 ya Mji wa Ngudu. Maeneo yatakayonufaika ni pamoja na Ngumo A, Ngumo B, Nguduruguru, *Stand* Mpya, Chamera, Bugakama, Iramba B, Iramba A, Ichefu, Majengo Mapya na Budula. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulala, swali la nyongeza.

**MHE. COSMAS M. BULALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali yaliyoletwa na kaka yangu, Nsumbantale wa Somanda, Mheshimiwa *Eng*. Mathew Kundo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, mahitaji ya mtandao wa bomba katika Mji huu wa Ngudu ni kilometa 72. Kwa sasa mtandao uliopo ni kilometa 33 tu ambao ni sawa na 46%. Je, ni upi mpango wa Serikali kuongeza mtandao wa usambazaji maji katika mji huu ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Kwimba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, uchakavu wa miundombinu iliyopo zikiwemo mita unasababisha upotevu wa maji pamoja na kukosa usomaji sahihi wa mita. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuboresha miundombinu ili kuzuia upotevu wa maji ambao kwa sasa unafikia 25%?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mtesigwa Bulala Cosmas, Mbunge wa Kwimba, kwa kazi kubwa na kwa kasi kubwa ambayo ameanza nayo kwa kuwatumikia wananchi wake wa jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa mtandao uko 46% ambayo ni sawasawa na kilometa 33. Ni mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba kila panapokuwa na mahitaji ya maji, na kila panapokuwa na wananchi wanajenga katika maeneo mbalimbali, Serikali itahakikisha inajenga miundombinu ili kuwafikia wananchi walipo na kutoa huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusu uchakavu wa miundombinu. Upotevu wa maji hauwezi kuchangiwa na uchakavu wa miundombinu pekee. Upotevu wa maji unaweza ukatokana na:-

(i) Uchakavu wa miundombinu, mabomba ama matenki kuwa yana-*leak;*
(ii) Mita ambazo zimechakaa;
(iii) Usanifu usiozingatia ubora na viwango; na,
(iv) Wizi wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili kupambana na jambo hili kwa sababu upotevu wa maji Kimataifa unaokubalika ni kuanzia 15% mpaka 20%. Sasa, hapa tumeshafikia 25%. Mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kubainisha maeneo ambayo tayari yameanza kusababisha upotevu wa maji na kudhibiti wizi wa maji na kufunga *Prepaid Water Metre* ambazo zitapunguza *Non-Revenue Water.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza, tumeanza na Chuo chetu cha Maji. Tumeandaa mfumo mahususi wa kiteknolojia wa kuendelea kubainisha maeneo ambayo kuna upotevu wa maji, ili tuweze kuchukua hatua stahiki. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Swali linalofuata, Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga, Mbunge wa Katavi, aulize swali lake.

Na. 65

**Ujenzi wa Miundombinu Bwawa la Nsenkwa - Katavi**

**MHE. THOMAS K. MAGANGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha za kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya kuchuja maji Bwawa la maji Nsekwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga, Mbunge wa Jimbo la Katavi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza ujenzi wa mradi wa miundombinu ya kutibu maji yanayotokana na Bwawa la Nsenkwa lililopo Wilayani Mlele, Mkoani Katavi. Utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa asilimia tano, ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2026 na kunufaisha wananchi wapatao 68,426 waishio katika vijiji 16 vya Wilaya ya Mlele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itahakikisha fedha za utekelezaji wa mradi zinapelekwa kadiri zinavyopatikana, ili kuhakikisha mradi huo unakamilika na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na ninawapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya. Kwa kuwa, wananchi wa Jimbo la Katavi wamesubiri mradi huu kwa muda mrefu na *speed* ya mkandarasi hairidhishi. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuongozana na mimi kwenda kuona uhalisia wa mradi na *speed* ya mradi, kama kweli utakamilika kwa wakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ni lini gridi ya Taifa ya Maji itaanza na Mkoa wa Katavi utanufaikaje?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninampongeza sana kaka yangu, Mheshimiwa Kampala Maganga, Mbunge wa Katavi kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatetea wananchi wake na hasa kwenye miradi ya maji, ili awatue akinamama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Serikali muda wote ipo tayari kuambatana na Waheshimiwa Wabunge kwenda kuangalia utekelezaji wa miradi, kwani ndiyo jukumu letu kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata huduma ya majisafi na salama. Nipo tayari, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Gridi ya Taifa ya Maji *(National Water Grid)* ni mradi ambao tunaweza kusema kwamba, tayari kama Tanzania, tumeanza. Mradi huu unatokana na matumizi ya maji yaliyo mengi sehemu moja na sehemu nyingine ni machache. Kwa hiyo, unachukua maji kutoka eneo moja kuyapeleka eneo lingine. Sasa kinachofanyika ni kwamba tunatumia vyanzo vyetu vya uhakika, tunatumia mabwawa kama nyumba ya Mungu, Mwalimu Nyerere na Kidunda, pia tunatumia Mito kama vile Pangani, Rufiji, Ruvuma na mito mingine mikubwa kama Malagarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunatumia Maziwa kama Tanganyika, Nyasa, Victoria pamoja na Rukwa. Lengo ni kuhakikisha kwamba, maji haya tunapoyakusanya yanatibiwa, yakishatibiwa yanasafirishwa kwenye mabomba kuyapeleka sehemu ambazo kuna uchache wa maji ili kuhakikisha kwamba, kila Mtanzania aweze kupata *access* ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa upande wa Katavi, tayari Serikali imeanza upembuzi yakinifu wa kutumia maji kutoka Ziwa Tanganyika ambao utasaidia katika Mikoa ya Kigoma, Katavi pamoja na Rukwa. Hivyo basi, ukishakamilika mradi huo, kwa namna moja au nyingine gridi ya Taifa itakuwa imewanufaisha katika kanda ya Katavi, Kigoma pamoja na Rukwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilisema muda umeisha.

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Namwita sasa Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, aulize swali lake.

Na. 66

**Kufufua  Kiwanda cha Korosho Tunduru**

**MHE. ADO S. ADO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais ya kufufua Kiwanda cha kubangua Korosho Wilayani Tunduru?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri. Mheshimiwa Londo.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kujibu maswali, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake. Pia, natumia nafasi hii kumshukuru Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa imani yake na kuniteua mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Mikumi. Pia naliahidi Bunge lako kwamba, nitalipa ushirikiano wa kutosha kwa kadiri ya uwezo wangu. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba sasa nijibu Swali Na. 66, la Mheshimiwa Ado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwekezaji wa Kiwanda cha Kubangua Korosho ambacho kinafahamika kama *Korosho Africa Factory* kilichopo Wilayani Tunduru aitwaye Bw. Sunil Kamath, kwa sasa yupo katika hatua za awali za maandalizi ya kufufua kiwanda hicho. Wizara inaendelea kushirikiana kwa karibu na mwekezaji ili kiwanda hicho kirudi katika uzalishaji na kuendelea kulingana na mahitaji yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado, swali la nyongeza.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Awali ya yote, napenda kutambua jitihada za Serikali kupitia Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Judith Kapinga, kufufua viwanda ambavyo vimekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kwa kuwa, ahadi hii ya mwekezaji huyu kufufua Kiwanda cha Korosho Tunduru imekuwa ni ya miaka mingi na ameendelea kutumia kiwanda kile kama ghala la kuhifadhi Korosho, kinyume na Mkataba wa Kubangua Korosho; na kwa kuwa, ndani ya Bunge hili Mheshimiwa Rais aliahidi kufufua viwanda kwa kushirikiana na vyama vya ushirika: Serikali haioni umuhimu wa kuvunja mkataba ule na kukikabidhi kiwanda kile kwa Chama Kikuu cha Ushirika Tunduru kwa maana ya *TAMCU*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, katika nchi ambazo zimepiga hatua kubwa katika tasnia ya ubanguaji wa korosho, *model* ambayo imefanya kazi vizuri sana, kama vile Vietnam na kule India, ni ya kuwawezesha wabanguaji wadogo wadogo; Wizara haioni ni wakati muafaka sasa kuwawezesha wabanguaji wadogo wadogo Wilayani Tunduru, hasa kwa kushirikiana na vyama vya ushirika vya msingi, kwa maana ya *AMCOS*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri, ni kweli Mheshimiwa Rais, ametoa ahadi ya kufufua kiwanda cha kubangua Korosho Wilayani Tunduru. Pia, naomba nizungumzie Dira ya Maendeleo, kwa maana ya *Vision 2050.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi ndio msingi, tunaenda kuimarisha mnyororo wa thamani, lakini nguzo kuu ni uchumi imara, jumuishi na shindani. Katika hilo, ahadi ya Mheshimiwa Rais tumeanza kusimamia utekelezaji wake, hivi tunavyozungumza, mwekezaji ameahidi ndani ya msimu huu wa 2026 anaenda

kuanza shughuli za uzalishaji, na pia, tumekuwa tunatoa hamasa kwa sekta binafsi, hasa vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kule Tunduru *TAMCU* wameonesha njia kwa vyama vingine vya ushirika, wameweza kununua eneo la ekari 4.5 katika Kijiji cha Kidewele pale katika Wilaya ya Tunduru kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kwa kuwa, mnyororo wa thamani ndiyo msingi wa uchumi imara na jumuishi, kama Dira ya 2050 inavyosema, Ilani ya Chama cha Mapinduzi inazungumzia kwenye Mkoa wa Ruvuma pale, kwenye Ibara ya 46, kuhusiana na nia ya Serikali kufufua viwanda na kuweka uchumi jumuishi, kwa maana ya kuwekeza kwenye viwanda vidogo vidogo na hivyo *model* ya Vietnam ndiyo ambayo sisi tunaenda kuisimamia kuhakikisha kwamba mwananchi, hasa mkulima wa korosho, anaingia kama mmiliki katika mnyororo wa thamani kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa *Eng.* Johnston Johansen Mutasingwa, Mbunge wa Bukoba.

Na. 67

### Hitaji la Masoko na Vifaa vya Kutegea Senene

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wauza Senene Masoko na vifaa bora vya kutegea Senene?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu Swali Na. 67 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutafuta na kufungua masoko ya uhakika kwa bidhaa za senene. Hii inajumuisha kuwaunganisha wafanyabiashara wa senene na masoko ya miji mikubwa nchini na Kimataifa, kuwashirikisha katika maonesho ya biashara za Kimataifa na kikanda na kutangaza senene kama bidhaa ya kipekee katika Kanda ya Ziwa Victoria yenye uwezo wa kuingia kwenye masoko mapana ya Afrika Mashariki na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo *(SIDO)* na kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)*, pamoja na *VETA*, imeendelea kufanya tafiti mbalimbali, ili kuendeleza na kuboresha biashara ya senene katika Mkoa wa Kagera. Mpaka sasa teknolojia rahisi ya mfano *(prototype)* itakayosaidia katika uvunaji wa senene imebuniwa na kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen Mutasingwa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ambayo yameonesha dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwajali na kuwathamini wafanyabiashara wadogo, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa wauza senene wapatao zaidi ya 1,000 katika Jimbo la Bukoba Mjini hawana eneo mahususi la kufanyia shughuli zao, na pale pembeni yao wanapofanyia hii shughuli kuna jengo la *bus terminal* ambalo linaenda kujengwa kwa sasa. Je, Serikali haiwezi kutenga fedha kidogo na kuongeza kwenye jengo hilo ili hawa wafanyabiashara

wa senene waweze kupata sehemu sahihi ya kufanyia shughuli zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ni lini Mheshimiwa Waziri utaambatana na mimi kwenda Bukoba ili kuona hayo maeneo na kupata fursa ya kuongea na wafanyabiashara wa Jimbo la Bukoba Mjini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maswali mawili mazuri ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa *Engineer* Johnston Mutasingwa, Mbunge wa Bukoba Mjini, kuhusiana na suala la mazingira wezeshi. Serikali ikishirikiana na Manispaa ya Bukoba tumeweza sasa hivi kuendeleza Mradi wa Ujenzi wa Soko la Senene pale kwenye soko la mjini ambalo kuna wanaozungumza kuhusiana na *Senene Complex*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kuwaweka wafanyabiashara wote wa senene pale na kutengeneza mazingira rafiki ambayo yatasaidia katika suala zima la biashara ya senene kuhusiana na suala la uwezeshwaji, kupitia Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, sasa hivi tunaenda kwenye bajeti, ni imani yangu kwamba, suala hilo litaingizwa kama ombi maalumu, kwa ajili ya Bajeti ya 2026/2027 na sisi, kama Wizara ya Viwanda na Biashara, tutashirikiana naye katika kuhakikisha kwamba, Serikali inaweka msukumo kwenye hilo. Suala la kuambatananaye kwenda kule, naomba niliahidi Bunge lako, baada ya Bunge hili nitaongozananaye.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tumalizie na swali Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Charles Jacob Sungura, Mbunge wa Handeni, aulize swali lake.

Na. 68

**Changamoto ya Tembo, Handeni**

**MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani kutatua changamoto ya tembo wanaoharibu mazao na kuhatarisha maisha maeneo ya Mzeli, Sindeni na Kwamatuku, Handeni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Waziri, Mheshimiwa Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Serikali imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kusimamia Utatuzi wa Migongano baina ya binadamu na wanyamapori kwa kuchukua hatua mbalimbali ili kuimarisha ulinzi wa maisha ya wananchi wetu na mali zao kwenye maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Mzeli, Sindeni na Kwamatuku katika Wilaya ya Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuweka Kituo cha Kudumu cha Askari Wanyamapori katika eneo la Handeni kwa ajili ya mwitikio wa haraka kwenye matukio na kuendelea kuimarisha doria za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu, kuendelea kutumia teknolojia za kisasa katika kudhibiti ikiwemo matumizi ya ndege nyuki *(drones),* sambamba na kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mbinu rafiki za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Sungura, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali haioni ipo haja ya kuweka *electric fence* ama fensi ya umeme, ambayo ni ya *solar,* hasa kwenye zile njia za tembo kwenye maeneo haya ya Mzeli, Sindeni na Kwamatuku, kama ile

iliyowekwa *Ikorongo Game Reserve* Mkoani Mara, yenye kilometa 33 ambayo inasaidia takribani vijiji sita dhidi ya tembo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Sungura, amekuwa naye ni sehemu ya wahifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, teknolojia hii ambayo ameitaja ya kutumia uzio wa umeme wa jua ni muhimu sana na imeonekana ina ufanisi mkubwa katika kuzuia au kudhibiti wanyamapori ambao ni wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mwaka wa fedha ujao, 2026/2027, Serikali tayari imekaa na kuandaa mwongozo wa kwenda kuweka taratibu nzuri katika kujenga miundombinu hiyo ambayo itadhibiti wanyamapori wakali na waharibifu, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, kwa kifupi sana.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Jimbo la Bunda Mjini, wananchi wangu ni miongoni mwa wananchi wa Tanzania hii walioathirika na wanyama wakali. Kuna jumla ya ekari 5,398 na mifugo walioathirika na tembo ni 355 na wananchi wanaodai kwa miaka mitatu mfululizo ni 1,483. Ni lini wananchi wangu watapatiwa fidia? Jana wametoka kunikumbusha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwanza niseme hakuna fidia ya kumlipa mwanadamu. Kwa hiyo, hiki ni kifuta machozi na kifuta jasho. Nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, sasa hivi mfumo umekamilika na fedha tunazo. Wewe kaa tu mkao wa kula. Kama siyo leo, kesho fedha hiyo itapatikana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako.

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza kipindi cha maswali, na kama mnavyoona, maswali yalikuwa mengi, waulizaji ni wengi na wengine hawakupata nafasi. Ushauri tu ni kwamba, tupeleke na tuombe maswali ya msingi kupitia vishikwambi vyetu. Maswali ya nyongeza ni kama hisani tu. Kwa hiyo, nawaomba sana.

Nina matangazo machache kutoka kwa Ofisi ya Mheshimiwa Spika. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Kwanza tunao wageni wa Mheshimiwa Omari Juma Kipanga, Mbunge, ambaye ni Ndugu Husna Mohammed, dada yake kutoka Mafia, Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge, Ndugu Sara Agustino, ambaye ni ndugu yake kutoka Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, ambao ni ndugu zake kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni muwe mnasimama mkisikia majina yenu.

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge. Hawa ni wafanyabiashara *Chap-Chap Financial Services* kutoka Nyamagana, Mkoa wa Mwanza, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge. Hawa ni viongozi wa Chama kutoka Mkoa wa Njombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 10 wa Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali, Mbunge. Ni Madiwani na Viongozi wa CCM, Mkoa wa Ilongero, Mkoani Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, Mbunge. Hawa ni watendaji wa Baraza la Manispaa kutoka Unguja, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge. Hawa ni Madiwani, Viongozi wa Chama na Watumishi wa Halmashauri kutoka Momba, Mkoani Songwe, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 13 wa Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge, ambao ni Walimu kutoka Wilaya ya Chemba, Mkoani Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo. Yupo Ndugu Hafidhi Muharani Abdully kutoka Dar es Salaam, Ndugu Stella Wiga na ndugu zake kutoka Jijini Dodoma na Ndugu Shabani Kipindura na familia yake kutoka Ubungo Jijini Dar es Salaam. Ninyi nyote karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanachama 10 wa kikundi cha kijamii *Sisterhood* kutoka Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Pia, tunao wanafunzi 90 na walimu tisa Shule ya Msingi St. Monica ya Jijini Arusha. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika anawakumbusha kwamba kutakuwa na bonanza litakalofanyika kesho Jumamosi, tarehe 31 Januari, 2026. Bonanza hili litafanyika katika viwanja vya Shule ya Sekondari John Melin iliyopo Miyuji Jijini Dodoma.

Bonanza litahusisha michezo mbalimbali ya burudani na mashindano ya timu za watani wa jadi Simba na Yanga na litaanza kwa maandamano yatakayoanzia Chuo cha Mipango Dodoma, saa 12.00 asubuhi. Mgeni rasmi katika Bonanza hili atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya bonanza hilo, jioni kutakuwa na tafrija itakayoanza Saa 12.30 jioni na kuendelea. Kauli mbiu ya Bonanza hili ni "Umoja Wetu, Ni Nguvu Yetu." *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine mnakumbushwa kwamba nyaraka zote kwa ajili ya mjadala wa Kamati ya Mipango ambayo itaanza kujadiliwa siku ya Jumatatu, tarehe 2 Februari, 2026 tayari zimeshawekwa kwenye vishikwambi vyenu. Nyaraka hizo ni kama zifuatazao:-

(i) Mpango wa Elekezi wa Maendeleo ya Muda Mrefu 2026/2027 - 2050/2051

(ii) Mpango wa Eneo wa Nne wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2026 - 2031; na

(iii) Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Waheshimiwa Wabunge, wote mnasisitizwa kuanza kupitia nyaraka hizo muhimu ili kutoa ushauri na maoni yatakayosaidia utekelezaji mzuri wa Mipango inayowasilishwa na Serikali ndani ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo yalikuwa matangazo kwa siku yetu ya leo. Baada ya hapa nimwite Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA- KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

**Hotuba ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa ufunguzi Rasmi wa Bunge la Kumi na Tatu, Tarehe 14 Novemba, 2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tuna wachangiaji wengi sana siku ya leo. Kwa hiyo, muda wetu utakuwa dakika nane na katika dakika nane kengele ya pili ikilia au ikipigwa, unaanza kuhitimisha usiongeze tena sentensi nyingine baada ya kengele ya pili ili tuweze kupata wachangiaji wa kutosha.

Waheshimiwa Wabunge, basi nimwite sasa mchangaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, ajiandae.

Mheshimiwa Esther hauko tayari! Uliomba baadaye! Basi tuendelee na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, halafu Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja, ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza kwa kuchaguliwa kwake kwa kura nyingi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwepo wakati Mheshimiwa Rais anahutubia Bunge kwa ajili ya kulifunga. Nilimsikiliza sana kwa makini na nilimwangalia wakati anazungumza, alionesha ana hisia kali sana. Sasa na sisi ambao tulikuwa tunahutubiwa kwa

niaba ya Watanzania wote, na waliokuwepo nje waliona hilo jambo. Sasa kitu gani tunatakiwa tufanye na sisi kama Wabunge? Kitu gani? Tunatakiwa tushauri na tufanye kazi yetu ya kibunge kuisimamisa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii iligusa mambo mengi sana, lakini Mheshimiwa Rais alijielekeza sana katika Dira ya Taifa katika hotuba yake, lakini la pili, alijielekeza katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Tatu, yalikuwa ni maelekezo kwa wasaidizi wake ambao ni watendaji wa Serikali na akiwemo Msaidizi Mkuu wa Shughuli za Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hili ushauri wangu nilikuwa ninaomba sana hayo maelekezo ya Mheshimiwa Rais waanze kuyafanyia kazi katika bajeti hii, tuone sasa mwelekeo na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, je, yanafuatwa? Kama bajeti itakuja tena kinyume cha hotuba yake, tutaona sasa wasaidizi wake wameshindwa kumsaidia Mheshimiwa Rais ipasavyo katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitegemei kama watakuwa wameshindwa, na sisi kama Wabunge tutawasaidia kuwashauri, na itakaposhindikana, basi aliyewapa dhamana ndio atajua sasa wapi mahali pa kuwapeleka, kwa sababu moja ya waliyopewa ni hiyo kumsaidia Mheshimiwa Rais katika maono yake aliyoyapanga katika uendeshaji wa Serikali kwa hii miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ambazo Mheshimiwa Rais anakuja kuzifanya ni pamoja na kuwaondolea matatizo wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pamoja na kuwaondoa matatizo ya kiuchumi na ya kijamii, ni kuwapa na wenyewe wapate tabasamu kama alivyosema kwamba atawaacha wako katika tabasamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi sekta alizozigusia amezungumzia katika hotuba yake sekta binafsi, uwezeshwaji wa sekta binafsi, uwezeshwaji wa wananchi kiuchumi na alitoa ahadi katika kampeni kwamba ndani ya siku 100 kuna chochote

kitatoka kwa ajili ya kuwasaidia wananchi. Sasa siku 100 zinakwisha na hatujaona hata cheche zinakwenda kule katika Halmashauri zetu. Sasa hapa ndiyo inaonesha wasaidizi wake wako namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nakwenda kulizungumza ni sekta ya uzalishaji kilimo, madini na masuala ya mifugo na uvuvi. Pia kuna sekta ya ujenzi ambayo ni sekta wezeshi. Bila barabara zetu kuimarishwa, hali itakuwa bado ni ngumu. Tutawezeshaje sasa wananchi ambao ni sekta binafsi, wakandarasi wako kule, kama madeni ya Serikali hayalipwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mategemeo yetu sisi kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba pesa za Mfuko wa Barabara zisiende katika Mfuko Mkuu, hili jambo litakuwa ni jema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ninaungana kabisa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu yeye ndiye alikuwa Waziri wa Fedha, anajua huko wenzetu wa *TARURA* wana miradi mikubwa ambayo haijakamilika, *TANROAD* wana miradi mikubwa ambayo haijakamilika, sasa mtawawezeshaje wananchi kiuchumi kama barabara hazijafunguka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni yaliyoko kule kwa wakandarasi, kuna wakandarasi wana hali mbaya sasa hivi, wamekopa katika mabenki na kila mahali. Sasa kama hatuwezi, na wao kuwasaidia katika jambo hili, kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Rais, kwamba uwezeshaji wa sekta binafsi na kukuza sekta binafsi, hili ni jambo la msingi sana. Tunategemea sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili atusaidie sana hao wakandarasi walioko kule waweze kulipwa fedha zao na miradi ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tunataka kulizungumza kwa ukubwa wake ambalo tunatoa ushauri wa kiungwana, kwamba sisi kama Wabunge hapa ndani, tunakuja kuisaidia Serikali kama jicho, lakini tunaishauri Serikali, na kufanya kazi za kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri zaidi miradi mikubwa ya nchi inayokuja kufunguliwa, kwa mfano, kama juzi tumekwenda kufungua meli, Mheshimiwa Waziri amekuja pale kumwakilisha Mheshimiwa Rais, wananchi wamekuja pale kwa tabasamu kubwa kuona meli inafunguliwa, lakini waliondoka pale hakuna hata maji. Yalikuwepo maji ya kunywa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitegemea siku hiyo mradi mkubwa wa shilingi bilioni 120 tungeweza kupata nyati kama 20 wakachomwa, unaona bwana! Watu wakapata wali na nini, sisi ndiyo tulivyo kule Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, miradi kama hii ikiwa inafunguliwa, watu wakitoka pale wanaenda sasa wanasimulia ile miradi, lakini wasitoke pale wamekaa toka asubuhi wanamsubiri Mheshimiwa Waziri Mkuu, anakuja anazungumza halafu anaondoka wanasahau, kwa sababu wameondoka na njaa, na mradi umefunguliwa wa shilingi bilioni 120.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifungua daraja kule Sengerema, tulipiga ng'ombe 30, watu wametoka pale wamekula, yaani mpaka leo linazungumzwa daraja na wanazungumzia hali iliyokuwepo pale. Sasa miradi yetu hii ya Serikali ikiwa inafunguliwa kinyonge, wakati imejengwa kwa pesa nyingi. Kwa nini msiweke hata asilimia moja ya sherehe, kwamba tunakwenda kufungua *ring road* ya Dodoma siku hiyo kuna sherehe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo angalia Ndugu yetu Mheshimiwa Makonda, amekwenda tu kwa ajili ya kuwa na *Land Rover* kuu kuu, mbovu za miaka 50 iliyopita, siku hiyo watu walichoma nyama, karibu ng'ombe 100 walichinjwa Arusha, kuangalia *Land Rover* mbovu tu. Sasa je, hili ni daraja tunafunga meli ya shilingi bilioni 120, watu wanatoka pale wana njaa. Haiwezekani. Kwa hiyo, tunataka tumsaidie Mheshimiwa Rais pamoja na kuyasema haya na sherehe ziwepo kwenye hii miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, tunachozungumzia hapa zaidi, sasa ninaweka mkazo wangu ni

kwamba tunategemea bajeti hii, safari hii itakuwa ni bajeti ya wananchi, tuone miradi ya kilimo, ya umwagiliaji, mifugo pamoja na ujenzi wa vizimba katika Ziwa Victoria. Kule sasa hivi Wachina ndiyo wamechukua eneo kubwa. Kwa hiyo, hotuba ya Mheshimiwa Rais uwezeshwaji wa wananchi bado haijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Taarifa inatolewa wakati mtu anachangia siyo akiwa amemaliza.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mchangaji wa pili. Nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa nami niwe miongoni mwa wachangaji wa hotuba ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweza leo kuwepo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee pia nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwa kishindo na wananchi wa Bagamoyo, tarehe 29 walimchangua kwa kishindo, walinichagua mimi kuwa Mbunge wao na Madiwani wa Chama cha Mapinduzi. Ninawashukuru sana wananchi wa Bagamoyo kwa imani yao kwangu na kwa mara ya kwanza kuweka historia Jimbo lile kuongozwa na mwana mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposimama kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ninamshukuru Mungu kwa sababu, sehemu kubwa ya hotuba ile, hasa kwenye miradi ya kimkakati iligusa Jimbo letu la Bagamoyo ili kuwakilisha Taifa

hili. Ninapojadili leo hotuba hii ndani ya siku 100 za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa madarakani, ninawiwa kusema kwamba hata miradi ya kimkakati kazi imeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajielekeza kwenye sekta ya viwanda na uwekezaji. Nia ya Serikali ya kuanzisha kongani nyingine ya viwanda kwenye Halmashauri yetu ya Mji wa Bagamoyo, jambo ambalo lilichukua takribani miaka 15, eneo lilikuwa limepimwa na wananchi wamesubiri sana kwa mara ya kwanza tarehe 31 Disemba, 2025 tulimpokea Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Prof. Kitila Mkumbo akija na wawekezaji sita na kuwakabidhi hati ili ndani ya mwaka ya mmoja wajenge viwanda. Wanabagamoyo tunashukuru hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba haitoshi, katika kipindi cha siku 100 tumepokea Mawaziri watatu, akiwemo Waziri Mkuu mwenyewe Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Ninawapongeza kwa kazi nzuri tangu mmeteuliwa, Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba haitoshi, ndani ya siku 100 tumeona ushuhuda wa kuanza kwa mradi wa ujenzi wa Bandari mpya ya Bagamoyo, baada ya Mamlaka ya Bandari Tanzania kusainiana *MoU* na kampuni ya ujenzi wa Bandari ya Bagomoyo kwa kuanza ujenzi wa gati tatu. Miradi hii mikubwa imepelekea wananchi wa Bagamoyo kupitia ziara niliyoifanya Kata karibu zote, kuwashukuru na kuzikiliza kero zao, kunipa maoni yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa tunachoiomba Serikali, kwa kuwa tunajua wanaongoza kwa kauli mbiu ya Kazi na Utu, utu wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan tumeuona, mara nyingi ombi letu ni malipo ya fidia kwenye maeneo ambayo yalichukuliwa kwa ajili miradi hii. Tumesubiri muda mrefu, lakini tumeenza kuona mwangaza hasa baada ya Serikali kuamua kufungua Ofisi katika Kata ya Zinga, Kiseza kwa ajili ya kusikiliza wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa maeneo ya Kondo, maeneo ya Mlingotini, Pande Zinga, Kiromo kwa sasa kwa kuwa tumeshaona dalili na mwelekeo wa miradi hii kuanza na maelezo ya Serikali hatua za awali, tunaamini watalipwa fidia na kupewa makazi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kwa kuwa miradi hii itahitaji sekta ya uwezeshaji ya nishati, na kwa kuwa tumeona ndani ya siku 100 kishindo cha uongozi wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kusaini mikataba ya kusambaza umeme vitongoji 9,009, mradi mkubwa wa aina yake utakaogharimu shilingi trilioni 1.200, Bagomoyo tunashukuru kupata vitongoji 21 kati ya vitongoji 330 vya Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii pia na mpango wa ujenzi wa *substation* Kata ya Zinga na njia ya kusafirisha umeme kutoka Chalinze mpaka Bagamoyo, pamoja na miradi wezeshi ya barabara ya Makofia - Mlandizi na kipande cha *SGR* kutoka Kwala mpaka eneo la viwanda, tunayo imani ndani miaka hii mitano Bagamoyo inaenda kuwa mji mwingine kabisa, na baada ya kupata hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vingine ambavyo ningependa kuchangia kutoka na hotuba hii ya Mheshimiwa Rais ni mafanikio ya sekta ya madini. Tunatambua ndani ya miaka mitano iliyopita ya muhula wake wa kwanza, aliweka historia ya kuhakikisha kwa mara ya kwanza tangu uhuru, Benki Kuu inanunua dhahabu. Uamuzi huu ulikuwa haujawahi kufanyika na mpaka sasa tunaposimama hapa, zaidi ya tani 1.7 zimenunuliwa na Benki Kuu na kuifanya nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi kumi kwenye Ukanda wa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kama Serikali inafanya maamuzi ya kuuza akiba yake kwa ajili miradi hii ya kimkakati, ninapenda kuiunga mkono na kuiomba Serikali isisikilize maneno ya watu ambao hawaitakii mema. kimfaacho mtu chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mama Samia anatoa maono haya ya Benki Kuu inunue dhahabu, hata hawakutoa

maoni, ni Bunge la Kumi na Mbili kupitia Kamati ya Nishati na Madini, kupitia Kamati ya Bajeti ambapo Mheshimiwa Rais alisikiliza na Wizara ya Madini ikaanza kufanya hiyo kazi. Inaposema leo inataka kuuza sehemu ili kugharamia miradi yake ya kimkakati kupunguza utegemezi wa mikopo ya nje, ni jambo la kuliunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanaharakati uchwara ni wa kuwapuuza na kuwaomba Watanzania wasipate taharuki yoyote kwa sababu huo ni uamuzi wa kimkakati, na ni sehemu ya hotuba yake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye ukurasa wa 14, na ninaomba niinukuu aliposema: "tutaimarisha masoko ya mtaji kwa kuhamasisha uwekezaji wa ndani na kutumia rasilimali zetu, kama madini kudhamini mikopo ya uwekezaji."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja hii na kumtakia kila la heri Mheshimiwa Rais. Katika hotuba hii, mengi yanatekelezeka katika muhula huu wa pili na kwamba tuna imani maendeleo makubwa yatapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango. Nimwite sasa Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja, atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, ajiandae.

**MHE. TWAHA S. MWAKIOJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninakushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Pili, nitumie nafasi hii adhimu na adimu kumshukuru muumba wetu kwa namna ambavyo ametupa neema hii ya uhai na afya ambayo hatuilipii hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amesimamia kwa uadilifu na weledi kwa kuzingatia Katiba, Kanuni na

miongozo yote ya chama chetu kuanzia Wilaya, Mkoa hadi vikao vya Taifa vya Kamati Kuu na Halmashauri Kuu, na hii leo mimi nikateuliwa na kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Chama chetu Chama Cha Mapinduzi. Ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika hotuba hii, niwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Mkinga kwa namna ambavyo walishiriki kikamilifu, kwa utulivu na amani, hatimaye kumchangua Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kura za kishindo za 99%. Hawakuishia hapo, walinichagua mimi Ndugu yao kwa kura za kishindo hivyo hivyo, za 97%. Kubwa zaidi waliweka historia kwa mara ya kwanza katika Jimbo la Mkinga kuchagua Madiwani wote wa Chama chetu Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Ninawashukuru sana Ndugu zangu wa Mkinga, dunia imeona, nchi imeona, Mkoa wa Tanga umeona namna walivyofanya kazi kubwa. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie pia nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wetu wa Mkoa wa Chama Cha Mapinduzi. Kwa kweli MCC wetu kwa weledi wake na ujasiri wake ameifanya Tanga kwa upande wa CCM haishikiki. Ninamshukuru sana Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye hotuba yetu kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ukiichambua hotuba yake, unaikuta ina pande mbili. Ina upande wa kwanza ambao unaonesha ulezi, huruma na upendo kwa Watanzania. Ukiitazama kwa upande wa pili, unauona weledi wake wa kutoa dira ya kiuchumi, wa kutoa dira ya maendeleo ya kijamii, kwa maana ya *social economic development*. Kwa kweli Dkt. Samia Suluhu Hassan ametutendea haki Watanzania, ameitendea haki nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watesi wanaosema kwamba tumekuwa na maendeleo ya vitu hatukuwa na maendeleo ya watu, hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na utendaji kazi wake wa miaka minne umedhihirisha dunia na nchi

ya Tanzania kwamba analenga kuendeleza watu na analenga kuiendeleza nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla, ninaomba niwataarifu kwa kujadili hotuba hii, kwa kuangalia maeneo makuu matatu. Tukiangalia, katika kipimo cha umaskini; tukipima kipimo cha kizamani tutahesabu tu idadi ya maskini; lakini tukiangalia kipimo cha kisasa cha *HDI*, tukiangalia kipimo kingine cha *multi-dimensional poverty* lazima tuangalie masuala za maji, elimu, na afya. Katika maeneo haya yote matatu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameupiga mwingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza eneo la kwanza la maji, wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani mwaka 2021 alikuta miradi zaidi ya 177 imekwama. Aidha, pesa imeliwa au mradi umejengwa, lakini hautoi maji. Akamwita na kumteua kijana wake, ndugu yetu Mheshimiwa Jumaa Aweso. Akampa maelekezo mahsusi kwa kutumia maneno yake, kwamba "ukinizingua, tutazinguana."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalishuhudia Bunge lako Tukufu kwamba ndugu yetu hakuzingua. Aliikwamua miradi 164, alihakikisha wakati anaingia madarakani ni vijiji 4,300 vinapata maji. Leo tunavyoongea hapa, ni vijiji 9,700 vinapata maji. Alikuta hali ya maji vijijini ni 70%, ninaposimama hapa, hali ya upatikanaji wa maji vijijini ni 85%. Alikuta maji mjini ni 85%, ninaposimama hapa upatikanaji wa maji mijini ni 92%. Hali ya Mkinga ni kubwa kuliko aliyotufanyia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametuletea mradi mkubwa wa zaidi ya shilingi bilioni 35, haujawahi kutokea. Mradi huu ukikamilika; na punde unakamilika, tutatoka 60% ya upatikanaji wa maji katika Jimbo la Mkinga na kufika 85%. Ni mradi unaokwenda kuwanufaisha zaidi ya 50% ya wananchi wa Mkinga. Ni mradi utakaonufaisha vijiji 37 na kata zaidi ya 10. Ni mradi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu akipenda keshokutwa, tarehe mosi, mradi huu wa maji utafunguliwa. Nami Mungu akinijalia, nitaacha kila kitu nikanywe maji haya tuliyopewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha.

**MHE. TWAHA S. MWAKIOJA** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, wakati wenzetu wakitukana, wenzetu wakibeza, sisi tutawajibu kwa hoja na kwa takwimu. Ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilishamwita Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, atafuatiwa na Mheshimiwa Lutevele Nathan Dickson, Mheshimiwa Yunus Mohamed ajiandae.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, hatimaye niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Mchinga kwa kunichagua na kwa kumchagua kwa kishindo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, nimpongeze tena Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteua Baraza lake la Mawaziri likiongozwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Kwa kweli wanakwenda na kasi ile ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anaihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ambaye ndiye Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha Bunge la Kumi na Tatu. Hongereni sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wale wa zamani na wale wapya, ambao

Mwenyezi Mungu amewajaalia na kurejea tena kwenye Bunge letu Tukufu kuendeleza kazi hii ambayo wananchi wetu wametupa sisi kama wawakilishi wao kueleza matatizo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, vilevile ninaomba nimpongeze Katibu wetu wa Bunge, Ndugu Baraka kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nijikite kuelezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhusu Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kufungua rasmi Bunge la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma tarehe 14 Novemba, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini ninachotaka kukisema? Kwanza niwapongeze Wabunge wote, kila aliyesimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu hakuna mtu ambaye hajampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametembea nchi nzima. Amefika mpaka kule kitongojini. Kufika kitongojini haina maana kwamba yeye mwenyewe afike, isipokuwa ana wawakilishi wake ambao ni Wabunge, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na kadhalika. Kwa hiyo, kule amefika na kutoa mabilioni ya fedha, na ndiyo maana nchi imefikia hapa tulipo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa uchumi umeongezeka kutoka 3.9 mwaka 2021 hadi kufikia 5.6 mwaka 2025. Haya ni mafanikio makubwa. Wakati huo huo, pato la Taifa limeongezeka kutoka shilingi trilioni 156.4 mwaka 2021 hadi kufikia shilingi trilioni 205.84 mwaka 2024. Huu ni uthibitisho wa sera nzuri za kiuchumi za Taifa letu la Tanzania. Nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala zima la miundombinu, hapa tunazungumzia suala la usafiri, ikiwa na

maana barabara, reli, bandari. Serikali imefanya kazi kubwa na ya kihistoria ambayo mpaka hivi sasa mtandao wa barabara umeongezeka, mtandao wa barabara za lami umeongezeka, barabara za changarawe umeongezeka, mwendokasi nao umeongezeka. Huu mwendokasi umerahisisha sana kazi za Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mtu akitaka kutoka hapa sasa hivi anafika Dar es Salaam na usiku anaweza akarejea. Hongera sana mama, tunakupenda kwa kazi yako kubwa na nzuri ambayo unaifanya. Ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege, ndege zimeongezeka, ujenzi unaendelea, kila kitu kiko kwenye *track*. Madaraja makubwa yapatayo kumi yakiongozwa na daraja la JPM nalo limekamilika, yaani, kigongo – Busisi ambalo lina urefu wa kilometa tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala zima la bandari, maboresho makubwa yamefanyika ikiwemo gati namba moja mpaka lile gati namba saba, kuongeza kwa kina kwa mita 14.5. Halikadhalika na kule Mtwara pamoja na Tanga, ujenzi wa meli MV Mwanza umekamilika, thamani yake ni shilingi bilioni 109.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uwekezaji sekta binafsi, yaani *DP World*, muda wa meli kusubiri umepungua kutoka siku 46 mpaka siku saba, haya ni mafanikio makubwa sana katika suala zima la usafiri. Halikadhalika, hata makasha kutoka 159,807 hadi kufikia makasha 215,286 yameongezeka. Hili ni jambo kubwa na ni jambo la kujivunia kabisa. Kodi imeongezeka kutoka shilingi milioni 850 mwaka 2023/2024 hadi kufikia shilingi trilioni moja. Nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ni kwa nini watu wanazungumza? Kwa nini watu wanasema? Ni kwa nini maneno ni mengi? Ukiona mti wenye matunda unapopolewa, ujue kuna matunda matamu. Ndiyo maana Mama Samia mara huku wanasema hivi, kwa kazi kubwa na nzuri ambazo amezifanya katika Taifa hili. Mama Samia anafahamika hapa kwa kazi kubwa na nzuri. Anafahamika Afrika na duniani, na ndiyo maana hata

dunia inamtambua kwa kumpa *award* mbalimbali kwa ajili ya kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe,…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe uchaguzi mkuu tumeufanya wenyewe kwa mara ya kwanza. Hatukupeleka bakuli kuombaomba. Sasa hii wale yanawaudhi. Nini tufanye? Tuendelee kulinda amani yetu, tuendelee kuitunza amani yetu, amani ndiyo kila kitu kwa maendeleo yoyote ya Taifa lolote duniani. Tumsemee Mama Samia kwa mazuri yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, muda umekuwa mdogo, nilikuwa na mengi ya kusema. Ninaunga mkono hoja, ninamtakia Mama Samia afya njema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete kwa mchango wako mzuri. Ninamwita Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, atafuatiwa na Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed, Mheshimiwa Suleiman Premji Arif ajiandae.

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaomba nitoe shukrani za dhati kwa kupata nafasi ya kuchangia. Kwa kuwa ndiyo mara ya kwanza kusimama kuchangia kwenye Bunge hili Tukufu, ninaomba niwashukuru sana kwa heshima na taadhima wananchi wenzangu, masela wenzangu wa Mafinga Mjini ambao wamewezesha mimi kuingia kwenye jimbo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu ambao kwa dhati ya moyo tunampongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hotuba nzuri yenye

mwelekeo wa kujenga Tanzania yetu katika kipindi cha miaka mitano aliyoitoa tarehe 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shukrani hizo, wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akipita kuomba ridhaa ya Watanzania, sisi kwenye Jimbo letu la Mafinga Mjini tulisema mengi ambayo yamefanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema mengi mno, na tulimshukuru sana na kumpongeza, na tukamwahidi kumpa kura za kishindo. Hilo tumelifanya, Wanamafinga wamelifanya kwa kumchagua kwa kura nyingi, na pia kwa kunichagua mimi Mbunge wao ambaye ndiye Katibu Mwenezi wa Chama mpaka sasa. Hapa ndani Bungeni ninawawakilisha waenezi wote wa Chama cha Mapinduzi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nijielekeze kwenye kuchangia hoja. Katika maeneo mengi ambayo Mheshimiwa Rais ameelekeza kwenye hotuba yake, lipo eneo muhimu ambalo ninaomba nichangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye eneo letu la Mji wa Mafinga, vijana wengi na wananchi wengi ni wafanyabiashara. Wengi humu ndani mnajenga, lakini mbao zote zinazojenga nchi hii zinatoka Mafinga na Njombe ambako wewe unatoka, lakini kidogo sana na Kilolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamejiajiri kwenye eneo hilo. Kwa nafasi hii ninaomba nichukuwe nafasi kuipongeza Serikali kupitia mamlaka ya mapato, hivi juzi wametatua kero kubwa sana ambayo ilikuwa inawakwaza sana wakulima kwa sababu ilikuwa inatakiwa lazima mkulima awe na mashine ya *EFD* kwa ajili ya kutoa risiti ndipo auze mzigo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuja na mpango rafiki kwa wananchi, kwamba watatozwa asilimia mbili tu ya mauzo wanayoyauza kwenye nchi hii. Hii asilimia mbili haimhitaji mtu kuwa na *EFD*

*Machine*. Ninafikiri hii ndiyo mipango mizuri ambayo tunatakiwa tuipeleke kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima mwenye shamba ambalo amepanda miti miaka 20 au 15 iliyopita, leo hii ukimwambia awe na *EFD* mashine kwa ajili ya kuuza mauzo ya mara moja kilikuwa ni kitu kinachowaumiza sana wananchi. *TRA* wamekuja na mpango mzuri ambao ninaupongeza, na tunaendelea kuhamasisha wananchi wengi sasa watumie fursa hii kufanya biashara zao za kuuza mazao ya misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaomba nitoe ushauri, kwa sababu wenzangu wengi wameshapongeza, na tumeeleza mazuri yaliyofanywa kwenye maeneo kadhaa. Ninaomba nitoe ushauri kwenye mikopo ya 10%, kwa maana ya 4:4:2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengi ambayo tumefanya ziara na tumezungumza na vijana katika jimbo langu, eneo kubwa ambalo linazungumzwa ni kuhusiana na masharti yaliyowekwa kwenye mkopo wa 10%. Moja kati ya kipengele kilichomo kwenye mkopo ule ni kwamba, kwanza mkopeshwaji lazima awe na kitu kisichohamishika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu kijana tunayemjadili leo, ni yule aliyetoka chuo, amemaliza masomo, bado hajawa na kitu, hajajenga nyumba au hajawa na dhamana, kwa maana ya kitu. Kwa hiyo, ninaomba mamlaka husika ziangalie. Kama sheria zilipitishwa Bungeni humu, tuangalie namna bora ili fedha hizi ziweze kuwasaida hawa watu na ziwafikie walengwa, tuangalie namna bora ya kuweka masharti rafiki ili hawa waweze kupata huo mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu Tanzania sasa hivi tumeendelea. Taarifa za kila mtu zipo kwenye kitambulisho chake cha *NIDA* na mamlaka za maeneo wanapotoka. Basi tuangalie namna ambavyo vijana wanaweza kuzipata fedha hizi kwa kutumia uangalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nimezungumza kuwa ninatoka kwenye eneo la viwanda, ninaomba ku-*declare interest*. Jana hapa amezungumza mchimbaji mwenzangu mdogo wa madini, mimi ni mfanyabiashara wa mazao ya misitu mdogo kabisa ambaye nimekuzwa na *TFS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Jimbo la Mafinga Mjini vipo viwanda, pia vipo Njombe na maeneo mengine. Sisi biashara kubwa sasa hivi wilayani kwetu na jimboni kwetu ni kuzalisha, kuongeza thamani mazao ya misitu, kuzalisha *vinea* ambazo zinakwenda kutengeneza *plywood.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali; sifahamu kama sheria hii ilipistishwa hapa Bungeni na bila shaka sheria hii ilipita hapa; Serikali kwenye kipindi kilichopita iliongeza *tax* kwenye *export* ya *veneer materials* ambazo zinazalishwa; kwenye *export* imeongeza shilingi 150 kwa kilo moja. Kitu ambacho ukipiga hesabu kwa *cubic meter* zilizopo kwenye kontena unapata shilingi milioni nne, mtu anatakiwa alipe *tax* ya *export* wakati faida ya zao lile lililomo mle ndani hata kama ikifika India au China haifiki shilingi milioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, imefanya wawekezaji wengi waliokuwa wamewekeza kwenye wilaya hizi nilizozitaja wameondoka kwenda nchi za jirani kwa sababu *export* tena haiwezekani, lakini katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais naomba nimnukuu kwenye ukurasa wa 24 alisema hivi:

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** "Tunapoelekea safari ya muhula wa pili wa miaka mitano ya Awamu ya Sita, tunajipanga kuweka kongani za viwanda katika wilaya ili kuongeza thamani ya mazao, kilimo na uvuvi, mifugo na madini tutakayozalisha na kuwawezesha kuzalisha bidhaa zitakazohitajika kwenye maeneo yetu. Tutahamasisha ujenzi wa viwanda vitakavyozalisha viwanda vingine kwa malighafi na vipuli; na viwanda vitakavyozalisha bidhaa zinazohitajika kwenye masoko ya kikanda."

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dickson muda wako umeisha nilikuwa nakuacha umalize *quotation*. Naomba tu uunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Wizara inayohusika ilitizame jambo hili, kwa sababu Wanamafinga waliowekeza kwenye eneo hili kwa kupeleka magogo kwenye viwanda, sasa nao wamekosa kazi, na maelfu ya vijana wamekosa kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Arif Suleiman Premji ajiandae.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona na kunipa nafasi hii ili nami niweze kuweka mchango wangu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo aliitoa Novemba 14 hapa Bungeni. Jina langu ni Kijakazi Yunus Mohamed. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema ambaye ameweza kutukutanisha hapa siku ya leo, nami kuweza kupata kibali cha kuzungumza mbele ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi kwa kuniona kwamba, natosha na ninafaa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Lindi kwa heshima kubwa waliyonipa, kwa kunichagua kwa kura zilizotosha kunifanya kuwa Mbunge wao niwawakilishe hapa Bungeni. Nawashukuru sana na niseme tu kwamba imani ambayo wamenikopesha, nami nitawalipa kwa kadri walivyoniamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na wachangiaji wenzangu ambao kwa wiki nzima hii tumekuwa tukijadili hotuba hii ya Mheshimiwa Rais, na niseme kwamba imekuwa hotuba ambayo imeonyesha kwamba yeye ni mama mstahimilivu, mama msamehevu. Pia hotuba hii imejaa utu, imejaa uwajibikaji, imejaa upendo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yameelezwa mengi kwenye hotuba hii, na kama wengine walivyoeleza, leo naomba nijikite kuzungumza kuhusiana na sekta ya maji. Kwa nini maji? Kwa sababu ukizungumza maji, kama tunavyojua, unazungumza afya; pia ukizungumza maji, unamzungumza mama, unamzungumza mwanamke, unazungumza ndoa nyingi ambazo zimevunjika kwa ajili ya wakinamama kwenda kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama ukurasa wa 17 kwenye huduma za kijamii, Mheshimiwa Rais anaeleza namna ambavyo alikuta hali ya upatikanaji wa maji na hali ilivyo sasa, na ninaomba nimnukuu, anaeleza: "Kwa upande wa huduma za kijamii, maendeleo makubwa yamepatikana kwenye sekta ya maji ambapo hali ya upatikanaji wa maji ilipanda kutoka 84% hadi 91.6% mijini na kutoka 70.1% hadi 85% vijijini." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hili na naomba nieleze, katika mkoa wetu wa Lindi, wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani mwaka 2021 hali ya upatikanaji wa maji ilikuwa ni 58% tu, lakini leo tunapozungumza hali ya upatikanaji wa maji imefika 75%. Siyo hilo tu, leo ipo miradi 18 ambayo inaendelea kutekelezwa, miradi ambayo ina thamani ya shilingi bilioni 150, na nitazungumza miradi miwili mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kwanza ni Mradi wa Ruangwa, Nachingwea na Lindi, wenye thamani ya shilingi bilioni 119. Mradi huu utakapokamilika utaweza kuhudumia vijiji 56 vya Wilaya ya Ruangwa, Wilaya ya Nachingwea na Wilaya ya Lindi. Vile vile hali ya upatikanaji wa maji itaweza kufika 85% vijijini. Nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kudhihirisha kwamba kazi inaendelea kwenye mradi huu, tarehe 21 Disemba, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba tulikuwanaye Ruangwa akituwekea jiwe la msingi la utekelezaji wa mradi huu, na tayari mradi ule umefikia 69%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia upo mradi wa Mavuji wenye thamani ya shilingi bilioni 44 ambao ukikamilika utakwenda kusaidia upatikanaji wa maji katika eneo la Kilwa Kivinje, Kilwa Masoko na Vijiji vya Nangurukuru, Singino, Chakama na Mavuji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu mpaka sasa mkandarasi yupo *site* anaendelea na kazi na umefika 90% na itakapofika mwezi Machi mwaka huu 2026, basi mradi huu utakamilika na Wanalindi, Wanakilwa, na Wananangurukuru, wataendelea kunufaika na maji. Mkandarasi ameanza majaribio ya kusukuma maji kwenye mradi huu. Nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama kwenye ukurasa huu huu wa 17, Mheshimiwa Rais anaeleza kwamba atakamilisha ujenzi wa gridi ya Taifa ya maji ambayo itategemea maji kutoka Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Kazi hii siyo kwamba itaanza, kazi hii imeanza na sisi ni mashahidi kwamba leo watu wa Tabora wanakunywa maji kutoka Ziwa Victoria, na tunafahamu kwamba mpango ni maji haya kufika hapa Dodoma, yakipitia Singida kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda hautoshi, nilikuwa na nondo nyingi sana, nina imani kwamba nitapata muda wakati mwingine. Kwa sasa nieleze tu ya kwamba naunga mkono hoja na niwatake Wabunge wenzangu pamoja na wananchi wa Tanzania tumuombee sana Mheshimiwa Rais, na Mheshimiwa Awesso ambaye anamsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza maono yake kwa kiwango kikubwa sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed kwa mchango wako.

Nilimwita Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati anafungua Bunge letu la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuweza kunisaidia kufika hapa leo kwenye Bunge la Kumi na Tatu, ikiwa ni wakati wangu wa awamu ya nne, Mbunge *senior* kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninakishukuru chama changu cha Mapinduzi kwa kuniteua na kunipeleka nipeperushe bendera kwenye Jimbo la Tarime Mjini chini ya Jemedari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru viongozi wote wa chama ngazi ya mkoa na wilaya kwa jinsi tulivyoshirikiana kuhakikisha kwamba tunainadi Ilani ya Chama cha Mapinduzi na hatimaye tukashinda ngazi ya Urais, Ubunge na Madiwani wote katika Halmashauri ya Mji wa Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niwashukuru wananchi wangu wa Mji wa Tarime na niwaambie kabisa kwamba imani waliyonipa nitaendelea kuwatumikia kwa kushirikiana nao kuhakikisha kwamba tunapeleka maendeleo yenye tija katika mji wetu wa Tarime. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo na shukrani hizo, niseme sasa napenda kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona kabisa kwamba ni Rais mwenye utashi wa kisiasa wa kuweza kufanya maendeleo ya Taifa letu. Ni Rais ambaye yuko *people development centred.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia maeneo mengi, ndiyo maana hata ilipelekea akaweza kupata tuzo mbalimbali kwa sababu amegusa sekta ya afya, elimu, barabara, utalii, nishati, maji na kwingine ambapo hayo yote ni maendeleo ya watu. Ameweza kupata tuzo zaidi ya saba kwa kipindi cha miaka minne. Kwa sababu ya changamoto ya muda, nitaweza kutaja tatu tu ambazo nitazifafanua muda ukiniruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameweza kupata *The Presidential Global Water Change Makers Award* na ukiangalia Mheshimiwa Rais, kwa kweli amewekeza sana. Kule kwetu Tarime ametuletea mradi wa maji Ziwa Victoria ambao ni takribani shilingi bilioni 134. Ule mradi ukikamilika, utawanufaisha watu wa Rorya, Tarime mitaa yote 81, utawanufaisha watu wa Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Rais aliweza kupata *The Gate Goll Keepers Award* kwa sababu alionyesha ni kiongozi mwenye dhamira ya dhati ya kupunguza vifo vya mama na mtoto, lakini pia kuboresha huduma ya afya, na ukiangalia ameboresha kwa Tanzania, Hospitali za Rufaa, Hospitali za Mikoa, Wilaya lakini hata kujenga vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameweza kupata *award* katika zile saba, *award* ya *Africa View Road Builders.* Kwa kuona kwamba ana utashi wa kuendeleza miundombinu ya barabara, reli, anga lakini hata pia kuboresha bandari zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda kuelezea kwa uchache kabisa jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais wakati anaingia anapokea kijiti kutoka kwa Hayati Dkt. Magufuli kwa ile kaulimbiu yake ya kazi iendelee, aliendeleza *function project* zote, lakini zaidi aliweza kuwekeza na hapa nitarejea kwenye hotuba yake *page*

ya 30 mpaka 33 jinsi ambavyo ameona atawekeza kwenye sekta ya usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye uwekezaji wa anga, Mheshimiwa Rais siku ile akatuletea, kwanza ametoa shilingi bilioni 35 kwenye ukarabati wa uwanja wa Musoma, kwenye *runway, tax way* na *up road*. Pia ameweza kutupa Mradi wa Mugumu ambao tumeupigania tangu Bunge la Kumi. Leo tunapata uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Mugumu ambao utagharimu zaidi ya shilingi bilioni 300, lakini Uwanja wa Msalato, Mwanza na kwingine. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Shirika la Ndege, Mheshimiwa Rais kwa kipindi cha miaka minne aliongeza ndege saba zikawa ndege 16, lakini naona tija ambayo ilileta, nitaenda kusema kwa muda kidogo maana yake umenigongea kengele. Kwenye mapato yaliweza kuongezeka kutoka shilingi bilioni 175 hadi shilingi bilioni 595.7 ikiongezeka kwa kipindi cha miaka minne shilingi bilioni 420 takribani 240%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iliongeza abiria kutoka 537,000 hadi 1,178,000, ongezeko la 640,000 abiria ambapo ni zaidi ya 119%. Mizigo kutoka tani 1,290 hadi 6,919 ikaongezeka tani 5,629 kwa maana zaidi ya 426%. Pia fedha za kigeni ziliongezeka kutoka dola…

**MWENYEKITI:** Malizia malizia.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika mbili tu. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** …dola milioni 43 hadi dola milioni 157 sawasawa na 264%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bandari sasa hivi anategemea kuwekeza kutoka gati 12 mpaka gati 22, na pia atafanya *extension* ya Bagamoyo ambayo itajenga gati 20.

Tunaenda kuwa miongoni mwa bandari, kuwa kwenye *Sub Saharan Africa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tulikuwa tunashindwa kuwa washindani, na hii yote itasababisha kuongeza mapato *on average* shilingi trilioni 10 kwa mwaka na kuchangia mapato ya *TRA* zaidi ya 40%…

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine nitayachangia kwa maandishi, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nilimwita Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, na Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa wajiandae.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na Mwenyezi Mungu akujalie kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nitoe pongezi kwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa, pia Makamu wa Rais, Waziri Mkuu wetu, Mawaziri, Manaibu na Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa na walioteuliwa. Hongereni sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nichukue nafasi hii nitoe shukrani zangu za dhati kwa Chama Cha Mapinduzi. Mwenyekiti wangu wa CCM Taifa, viongozi wangu wa Taifa wa mkoa, wilaya, kata, shina na bila kuwasahau mabalozi waliotusaidia sana sisi viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninashukuru wananchi wa Mtwara Vijijini kunipatia nafasi ya kuja kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu la Kumi na Tatu. Ahsanteni sana kwa hilo. Pia niwashukuru ndugu zangu na familia yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninaomba niwashukuru Watumishi wa Bunge hili, maana yake nilikuwa napata tabu,

walikuwa wananielekeza; pita huku, pita huku. Kwa hiyo, ninawashukuru sana na ninaomba Katibu wa Bunge wapelekee salamu hizo kutoka kwa Mheshimiwa Arif Suleiman Premji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *development* ni *progress.* Wakati nchi hii inapata uhuru walikuwepo wananchi milioni tano, leo hii tunapozungumzia tupo wananchi milioni 70, lakini ukiangali *square meter* za mraba za Tanzania ziko vilevile. Hiyo ndiyo *growth,* na wengi wameongelea kuhusiana na *growth.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Mheshimiwa Mbunge aliyesimama akasema kwenye jimbo lake hakujafanyika kitu, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa hilo. Hakuna Rais kwenye nchi hii ambaye hajafanya *developments* tangu tupate uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri, lakini naomba ninukuu sehemu ya mwisho kabisa, maana yake siku zote kama ukitaka kujua mtu anachomaanisha kwenye hotuba, ni *closing statement* yake anasema *hivi:* "Namwomba Mungu kuwa mwisho wa utumishi wa Awamu ya Sita usipimwe tu kwa vitu, bali pia kwa tabasamu la utu litakaloachwa kwenye nyuso za Watanzania." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anamwomba Mungu, anamtanguliza Mola wake, maana yake anapenda haki. Pia amesema neno "utumishi" kwenye hiyo *statement,* na sio mtawala. Yeye ni mtumishi wa Watanzania. Pia kasema, "tabasamu la utu." Inaonyesha dhahiri kabisa ana nia njema na ya dhati kwa sisi Watanzania anaotuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitie neno hapo, "tabasamu la utu" ndiyo ngome ya mwanamke mwenye busara na hekima. Mengi yamefanywa hata kwenye Jimbo la Mtwara Vijijini. Hapa tunavyozungumza, shilingi bilioni 434 kuna bandari inajengwa Kisiwa Mgao, na sio sehemu nyingine yoyote Tanzania, ndiyo itakuwa ni bandari ya kwanza Tanzania ambayo itakuwa ni *Dirty Port* kupokea mizigo michafu na kutoa nje, pia ya makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vingi vimefanywa, kila Mbunge anayesimama anamwaga takwimu, atamwaga bilioni atasema ni hizi. Kwa hiyo, hilo nimpongeze sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mtwara Vijijini lina kata 21 na wananchi, pia wamenituma, siyo kwamba hakuna changamoto, zipo. Kama nilivyosema awali, *development* ni *progress.* Yapo mambo ambayo yanapaswa kuboreshwa, bado tuna uhitaji wa maji katika baadhi ya kata. Tunaomba hilo tabasamu la utu litufikie sisi Mtwara Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, bado tuna changamoto za barabara, tuna kilomita 614 na ndani ya kilomita 614 kilomita nane tu ndiyo tuna barabara ya lami. Tunaomba tabasamu la utu litufikie sisi Mtwara Vijijini.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Bwana Premji, muda wako umeisha, malizia.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Nimesikia kengele ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, kwenye sekta ya elimu ninaomba uniwie radhi ninaliongelea hilo...

**MWENYEKITI:** Siyo kwamba uendelee.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *close*.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa ninafunga. Ninaunga mkono hoja, Mwenyezi Mungu ambariki Mheshimiwa Rais, awabariki viongozi wetu, awabariki Watanzania wote ili tuweze kupata maendeleo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, atafuatiwa na

Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, Mheshimiwa Mary Daniel Surati ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kusimama kwa mara nyingine ndani ya Bunge hili ili kutoa mchango wangu juu ya hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda huko, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wapigakura wangu wa Wilaya ya Rorya kwa kunichangua kwa mara ya pili kwa kura nyingi. Pamoja na mshikemshike uliokuwepo kuanzia ndani ya chama mpaka kura ya nje, lakini bado waliamini ninatosha na sasa nimesimama kwa ajili ya kuwasemea. Niwaahidi nitafanya hivyo kwa moyo na kwa nguvu zote mchana na usiku kama ilivyo dhamira yao ya kunituma ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuwashukuru sana kwa kura nyingi walizompatia Mheshimiwa Dkt. Samia wakati tunakwenda kwenye mchakato wa uchaguzi hasa kwa kutambua kazi kubwa, nzuri iliyofanywa kwenye wilaya hii. Huwa tumekuwa tukisema, toka uhuru, kazi kubwa, nzuri iliyofanywa imefanywa Awamu hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nikuhakikishie wananchi hawawezi kumsahau kwa mazuri yaliyofanyika kwenye Wilaya yetu ya Rorya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna nzuri na bora alivyoanza kufanya kazi, kutekeleza maono na dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia. Pia amekuwa akizunguka maeneo mbalimbali kutengeneza uhai wa Serikali na kujibu yale ambayo yanapaswa kujibiwa kwa mujibu wa utaratibu na namna ambavyo ameelekezwa na mtangulizi, kwa maana ya kwamba ameelekezwa na aliyemteua kwenye nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, sisi Wabunge na wananchi kwa ujumla wake yapo mambo kadhaa ambayo tumekuwa tukisimama tunayasema, na tunayaomba

ambayo ndiyo mwelekeo wa kura ili kutuinua kisiasa turudi ndani ya Bunge, na pia kijamii tuweze kuwasaidia wananchi wetu kwenye maeneo tunayotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiomba maeneo mengi hapa; juu ya namna ya uimara wa miundombinu ya barabara, juu ya namna ya upatikanaji wa huduma za umeme, juu ya namna ya upatikanaji wa huduma za maji, afya, elimu kwenye maeneo mengine na mengine huwezi kuyamaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge hili, Wabunge waliopita na Wabunge wapya waliokuja, wote tutasimama mashahidi. Katika Awamu hii iliyopita na Awamu inayoendelea kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia, maeneo haya yote niliyoyasema Mheshimiwa Dkt. Samia ametekeleza kwa kiwango cha hali ya juu. Ndiyo maana unaona leo hii Wabunge tumesimama, Wabunge tumechaguliwa na kurudi ndani ya Bunge kwenye maeneo mbalimbali bila kikwazo chochote kwa sababu wananchi wanatambua kazi kubwa nzuri aliyoifanya Dkt. Samia kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda mbali zaidi kwa tathmini ya mwenendo wa uchumi wa dunia ambayo imetolewa na Benki Kuu ya Tanzania, ni mambo yapi ambayo yameashiria ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia ameyafanya na yamepelekea sisi kupata kura nyingi; na siyo kura peke yake, yamepelekea yeye kuaminiwa na wananchi na kumchagua kwa kura nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ni namna alivyosimamia uimara wa uchumi wa ndani ya nchi. Mheshimiwa Mama Salma Kikwete amezungumza hapa, sina sababu ya kurudia. Amesimamia namna ya uchumi wa ndani ya nchi kuendelea kuwa imara kwenye maeneo mbalimbali, kuendelea kutoa fedha kwenye maeneo mbalimbali. Nenda uone alivyotoa fedha nyingi kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ametoa fedha nyingi kwenye sekta wezeshi, sekta za uzalishaji. Hii yote amefanya

kwa mapenzi makubwa aliyonayo ndani ya nchi hii. Ndiyo maana leo tunasimama tunajipiga vifua mbele tunasema Mheshimiwa Dkt. Samia amefanya kazi nzuri, anahitaji maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda uone namna ambavyo Mheshimiwa Rais ameendelea kuimarisha na kusimamia mfumuko wa bei kwenye maeneo mbalimbali. Mpaka sasa tunavyozungumza katika maeneo mbalimbal,i bei imeendelea kuwa imara, kwa sababu anajua na namna alivyofanya ni kuendelea kuwahudumia wananchi kwa namna ambavyo imekuwa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya nishati kwa maana ya umeme, leo watu wanazungumzia Bwawa la Mwalimu Nyerere. Juzi tu, Mheshimiwa Dkt. Samia ametoa shilingi bilioni 1.2 kusaini mkataba wa vitongoji zaidi ya 9,000 *plus,* ambavyo vinakwenda kutuhudumia sisi wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu, kama mnakumbuka, wakati tunaingia Bunge la Awamu iliyopita, katika vitongoji 64 *plus* nchi hii tulikuwa tuna zaidi ya robo tatu ya vitongoji. Hivyo havikuwa na huduma ya umeme. Mama amepiga kwa awamu iliyopita, na sasa amekwenda amesaini mkataba wiki iliyopita, zaidi ya vitongoji 9,000 vinakwenda kunufaika na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kumshukuru sana kwa sababu nimechungulia kabrasha, nimeona Wilaya yangu ya Rorya ina vitongoji zaidi ya 70, ukiongeza na vile 80 ambavyo *TANESCO* wanavitekeleza, nina vitongoji zaidi ya 100. Ninaamini ndani ya miaka mitatu ya utekelezaji wa awamu hii changamoto ya umeme kwenye eneo langu inakwenda kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia ameitoa vizuri sana, na lengo na dhamira yake: Moja, apate ushauri wa Bunge. Pili, wasaidizi wake waweze kuyasimamia yale anayoyasema ndani ya Bunge. Sisi kama

Wabunge hatutakoma, tutaendelea kushauri yale mazuri ambayo tunaamini ndiyo mwelekeo wa Mheshimiwa Dkt. Samia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake amezungumzia namna atakavyokwenda kuimarisha kilimo biashara kwenye maeneo mbalimbali. Dhamira yake ni kwamba, Waziri wa Kilimo atalichukua ili aone namna ya kufanya. Vilevile, kwenye hotuba yake Mheshimiwa Rais ameongezea namna ambavyo anakwenda kuongeza fedha kwenye sekta wezeshi na uzalishaji, kwa mfano upande wa *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira yake na sisi kama Bunge, tunamwomba Waziri husika alichukue hili aone namna ya kwenda. Wabunge wengi humu ndani sasa wanazungumzia uchakavu wa barabara katika maeneo ya vijijini tunakotoka, kwamba barabara hazipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Mheshimiwa Mheshimiwa Dkt. Samia mpaka kwenye hotuba yake kuamua kuongeza fedha, dhamira yake ni nzuri kwa wananchi wale wanyonge. Tunatamani wasaidizi wake na sisi Bunge tumsaidie ili fedha ziweze kuongezeka kwenye eneo hilo ili wananchi waweze kupata huduma nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili hili Mheshimiwa Rais ameongea namna anavyokwenda kuongeza fedha za upatikanaji wa miradi ya maji kwenye maeneo mbalimbali, na tutalisema sana wiki ijayo wakati tunachangia Mwongozo wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Mheshimiwa Rais ameonesha namna anavyokwenda kutoa fedha kuwasaidia wananchi wanyonge na kumtua mama ndoo kichwani. Dhamira yetu na mwelekeo wetu, tunatamani wasaidizi wake Mheshimiwa Waziri walichukue hili waone namna ya kulifanya ili liweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameelezea namna ambavyo anakwenda kuimarisha sekta ya madini.

Anaenda kutoa vitalu kwa wachimbaji wadogo. Mfano mimi ninayezungumza hapa, tayari nimepata tetesi za machimbo eneo langu la Nyanjage, Kijiji cha Nyanjage, Kata ya Kisumwa na wananchi wameanza kuchimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia na Mheshimiwa Waziri ni ili angalau wachimbaji wadogo ambao wamejitokeza maeneo yale waweze kupewa vibali waanze kuchimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli yapo mengi ambayo Daktari ameyasema, na kwa muda wa dakika tano ninaamini ukipewa huwezi kuyasema yote ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia ameyafanya. Itoshe kusema kwamba, mama ameupiga mwingi, tumwombee Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu. Sisi kama Bunge, tupo imara, tutashauri pale inapobidi, tutaelekeza pale panapotakiwa ili mambo yaendelee kuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, Mheshimiwa Mary Daniel Surati atafuatia, Mheshimiwa Yohana Steven Msita, na Mheshimiwa *Eng.* Ramadhani Hamza Singano wajiandae.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fadhila na neema yake aliyoweza kunijalia, hatimaye na mimi nimeweza kurudi kuwa Mbunge baada ya kuwa nimepotea kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita, lakini kwa neema yake ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninawashukuru wanawake wote wa Mkoa wa Lindi kwa kuniona na kunirejesha tena Bungeni. Ninawaambia uongozi ni utumishi. Niliwaomba kuwatumikia, nitawatumikia kwa nguvu zangu zote, kwa utashi

wangu wote, na kwa bidii na maarifa yangu yote kwa kadiri ambavyo Mwenyezi Mungu amenijaalia kipawa hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kuunga mkono hotuba ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ukisoma hii hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ninampongeza sana, ninaungana na wenzangu wote kumpongeza kwa dhati. Unauona ule utayari wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wa kufanya kazi kwa kasi ya kuwaletea maendeleo Watanzania na hasa kutimiza yale matarajio yao ya kuwainua kiuchumi uchumi wa mtu mmoja, mmoja na hususan kikundi cha vijana pamoja na kikundi cha wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninatamani ile *spirit* ya Rais wetu ya kuwa na kasi na kuwa na utayari iweze kuambukizwa kwa walengwa ambao ni vijana na wanawake. Wawe na utayari wa kuchangamkia fursa zilizopo za uwekezaji, fursa za kupewa mitaji, fursa za kuanzisha viwanda vyo uzalishaji, fursa za kwenda mashambani kwenda kulima mazao ya kibiashara na mazao ya chakula, lakini fursa ya kufanya shughuli za uvuvi na shughuli za kilimo, fursa ya kufanya shughuli za utalii, fursa ya kuuza na kufanya biashara ndani na nje ya Tanzania, lakini fursa ya kuwa ma-*CEO* wa kampuni zao wenyewe watakazozianzisha ili wao pia waweze kuzalisha ajira kwa Watanzania wengine. Ndugu zangu fursa hizi zinahitaji watu ambao tunao, zinahitaji ardhi ambayo tunayo na zinahitaji mipango madhubuti ambayo tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuisemea machache na hususan nitalenga zaidi katika Mkoa wangu wa Lindi ambako ndiko waliponichagua. Tayari ndani ya siku 100 tangu uchaguzi umefanyika, Rais wetu ametenga kiasi cha shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kukuza mitaji ya vijana na wanawake. Ninawaomba vijana na wanawake twende na utayari wa Mama Samia kwenda kupata mikopo hii na kutumia fursa hii ili tuweze kukuza mitaji yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejenga Bandari ya Uvuvi katika Wilaya ya Kilwa Mkoani Lindi. Ni bandari kubwa sana ya kimkakati, bandari ambayo imegharimu kiasi cha shilingi bilioni 279, na bandari hii mpaka sasa iko katika 90% na, ina maana hivi karibuni itakwisha. Bandari ina uwezo wa kubeba meli 13 kwa wakati na mpaka sasa Rais Samia ameshatuletea meli tano za uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, kutakuwa na fursa mbalimbali pale za kuanzisha viwanda vya kutengeneza nyavu za kuvua samaki, kutakuwa na viwanda vya kuchakata samaki, lakini pia kutakuwa na viwanda vya kuhifadhi samaki *(cold rooms)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kutahitajika kuanzisha *fish farming* kwa maana ya kuanzisha mabwawa madogo madogo ya kuzalisha samaki, kutahitajika chakula cha Samaki, kutakuwa na fursa ya kupokea wageni wengi watakaohitaji mahali pa kulala, huduma za hospitali, huduma za shule hizo zote ni fursa ambazo ninawaomba vijana na akina mama twende na utayari wa mama Samia ili tuweze kuzichangamkia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaingia mkataba wa Bomba la Gesi na Mafuta kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri ametuelezea kwa ufupi na yenyewe inahitaji utayari wa Mama Samia. Ninaomba vijana na wanawake twende tukaichangamkie *spirit* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya madini upo mpango wa kuwaandaa wachimbaji wadogo wadogo waweze kuwa na maeneo yao rasmi ya kuchimba na kurasimishwa na kuwekewa miundombinu iliyokuwa imara, inayofaa sana kwa ajili ya kutumika kwenye shughuli hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwenye madini nako kuna fursa mbalimbali, kwenye masuala ya *transportation, logistics* na usafiri kwa maana ya usafirishaji. Kwenye masuala ya huduma mbalimbali za chakula, kwenye masuala ya huduma za hospitali,

kwenye masuala ya huduma ya mafundi watakaokuwa wanatengeneza zile *mechanics*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba na katika Mkoa wetu wa Lindi ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab, ninaona unakwenda *speed,* muda umekwisha, hebu malizia.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yatawezekana kama tutakuwa na utayari, kama Serikali itatusaidia kutuwezesha kuwa na zile shule za *VETA* ambazo zitawa-*train* vijana wetu wakawa na *skills* ili waweze kutumika katika...

**MWENYEKITI:** Malizia hoja yako, kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia na miundombinu ya barabara tunaomba izingatiwe katika Mkoa wetu wa Lindi kama fursa kwa ajili ya kuwekeza na kupokea utayari wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambao ninaamini utaambukizwa kwa vijana na wanawake. Pia, kwenye sekta ya kilimo, ninawaomba vijana wawe na utayari kwa sababu Serikali itawatengea maeneo vijana na kuwasaidia...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, Kiti kikisema malizia maana yake usianze upya, hatutamaliza.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *thank you*. Ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya mwisho. Kwa unyenyekevu mkubwa sana, ninaendelea kumpongeza Rais kwa utayari wake na kasi yake ya kutuletea maendeleo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tutajifunza pole pole. Nilishamwita Mheshimiwa Mary Daniel Surati, Mheshimiwa Yohana

Stephen Msita, atafuatia Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano na Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo, wajiandae.

**MHE. MARY D. SURATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Serengeti kwa kuniamini mimi kama binti na kijana kwa mara ya kwanza kuwa Mbunge wa Jimbo la Serengeti. Yanaweza yakaonekana ni mambo ya kawaida, lakini kwa mtu yeyote anayeufahamu Mkoa wa Mara na kwa mtu anayezijua mila na desturi za Mkoa wetu wa Mara, mimi kusimama hapa siyo jambo dogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongezee, hii yote imetokana na imani kubwa na ari na utayari ambao Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, matendo ambayo amekuwa anayafanya, udhibiti wake, uongozi wake na kwa jinsi ambavyo amekuwa ni kiongozi madhubuti amefanya hata sisi wanawake, mabinti na vijana wa jinsia ya kike tuendelee kuaminika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru tena Wananchi wa Jimbo la Serengeti kwa kura nyingi na za kishindo walizozitoa kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambazo zimechangia mpaka leo hii yeye amekuwa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeonesha wazi dira, dhima na jinsi ambavyo yeye kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni wapi anataka nchi ielekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa kama kijana, baada ya kuisoma hotuba yote, hekima yangu inanituma, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amewabeba vijana moyoni mwake na ndio ambao amewaweka katika moyo wake kwa nafasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku 100 ambazo Mheshimiwa Rais amekwenda kuanza kutekeleza majukumu yake ni kwa upekee mkubwa sana ameweza kutupatia vijana Wizara ya Vijana. Jambo hili linaweza likaonekana ni jambo la kawaida na pengine mtu anaweza akafikiria ni jambo limefanyia tu kulala, pakawa; nikuhakikishie, ni jambo ambalo vijana walio katika asasi mbalimbali za kiraia, vijana ambao wanafanya *lobbying and advocacy* watakwambia wamehangaika kiasi gani kuhakikisha vijana tunapata Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuja, amelifanya *in just a single snap,* kitu ambacho kimepelekea sasa vijana kupata chombo chao ambacho kinaweza kuwaongoza, kuwasikiliza na kutatua changamoto zote ambazo wanazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niendelee kugusia miradi ya kimkakati ambayo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameigusia kwa Mkoa wetu wa Mara hasa Jimbo la Serengeti. Sisi Serengeti tumenufaika kikubwa sana kwa kupata Uwanja wa Ndege wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja huu unaweza ukaonekana pia pengine ni moja kati ya viwanja vingine ambavyo vinaendelea kujengwa nchini. Ila nikuhakikishie uwanja huu ni wa kipekee, kwa sababu Hifadhi ya Serengeti sasa hivi ni mara ya nne mfululizo imeiletea nchi yetu tuzo ya heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, tunaamini Hifadhi ya Serengeti itakuwa moja kati ya hifadhi kubwa ambapo yale malengo ya Mheshimiwa Rais ya kufikia watalii 8,000, Serengeti tutakwenda kuhakikisha jambo hilo linafanikiwa pakubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mambo hayo ambayo nimeweza kuyazungumzia, niseme kwamba, hawa ambao baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamewataja kama watesi; ila ninakumbuka, Mheshimiwa Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alituongoza tuwaite ndugu zetu wa vyama rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe zinapokuja ajenda za Kitaifa tuzijadili Kitaifa na tusiweke ushabiki. Nikimaanisha nini? Leo hapa asubuhi wakati tunaendelea kuongea, baada ya swali kuulizwa kuhusiana na uanzishwaji wa Baraza la Vijana, swali la muhimu na la msingi, ilitokea taarifa ya kwamba, mmoja kati ya Waheshimiwa Wabunge akagusia kuwa, lile jukwaa ambalo lipo kwa ajili ya kutatua changamoto za vijana kwamba linafanyika kama ki-UVCCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kuwaomba vijana wote nchini Tanzania waendelee kuwa na imani kubwa na Wizara ya Vijana kwa sababu, Mheshimiwa Rais ametuamini sana. Sambamba na hilo ninawahakikishia sasa hivi hakuna jambo linafanyika kwa siri, kazi zote ambazo Mheshimiwa Waziri wa Vijana amekuwa anazifanya tangu aanze zinapatikana *instagram*. Nenda kaangalie *instagram account* ya Wizara ya Vijana, kaangalie *page* halisi pia ya Mheshimiwa Waziri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona tokea ameanza kufanya majukumu yake, Waziri husika, amefanya kazi alizomtuma Mheshimiwa Rais, kuunganisha vijana na kuhakikisha wanapata chombo cha kuwaunganisha pamoja. Kwa kuyasema hayo, ninasema ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ninamwita sasa Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano ajiandae, akifuatiwa na Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo.

**MHE. YOHANA S. MSITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata fursa hii adhimu kabisa ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo aliitoa hapa Bungeni tarehe 14 Novemba, 2025. Kwa kuanza ninachukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu na ndani ya Bunge la Kumi na Tatu ni miongoni mwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ninayetoka Jimbo la Itigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Itigi kwa kura nyingi ambazo zimenifanya leo niwepo ndani ya Bunge lako Tukufu. Tatu, ninamshukuru sana

Mheshimiwa Rais, ambaye ni Mwenyekiti wa Chama chetu Chama Cha Mapinduzi, chama dume kabisa, pamoja na viongozi wote wa Chama Cha Mapinduzi katika michakato yote na kupendekeza jina langu. Ninasema ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaanza kwa kutoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameanza kazi ndani ya muda huu mfupi tangu ulipofanyika Uchaguzi, Oktoba 29. Pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye pia, naye ameanza kwa kasi kubwa; amesema hapa kwenye hotuba yake kwamba, anakuja na rato na fyekeo na kweli, tumeona kwenye ziara yake tayari amekwishaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaanza kujielekeza kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Yapo mambo mengi ambayo yamezungumzwa na Wabunge Wenzangu na ninataka nikwambie ninakubaliana na michango yao yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nijikite kwenye mambo kama matatu. Moja ni kwenye hotuba tumeiona dhamira halisi ya Mheshimiwa Rais kutaka kutupeleka mahali ambapo ni pazuri. Ndiyo maana ukiisoma hotuba yake, kule mwishoni anamalizia kwamba, hakika mara baada ya kumaliza kipindi chake atatuacha Watanzania tukiwa na tabasamu. Hili tabasamu siyo la maneno ni kwa sababu ya mambo na mikakati ambayo ameizungumza kwenye kitabu chake hiki cha hotuba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala la kwanza ni kuhusiana na mambo ya utumishi na utawala bora. Yamezungumzwa mambo ya uwajibikaji na uwazi, ninataka niseme kwamba, sisi kama Taifa tukisimama katika kuwajibika na mambo yetu yakawa katika hali ya uwazi, Nchi yetu ya Tanzania itapiga hatua sana. Sisi Watanzania tuna imani kubwa sana na Mheshimiwa Rais kwa hatua ambazo ameendelea kuchukua, ninataka niseme ndani ya miaka hii mitano hakika tutafika kule ambako tunaitarajia kuiona Nchi yetu ya Tanzania inakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa masuala ya usimamizi wa fedha na rasilimali. Sisi Jimbo la Itigi tumekuwa

wanufaika sana, ndani ya miaka minne iliyopita iko miradi ambayo imetekelezwa kwa kiwango kikubwa sana. Hivi tunavyozungumza hospitali yenye hadhi ya wilaya ndani ya jimbo langu, yenye thamani ya shilingi bilioni 1.75, imejengwa; ni kwa sababu ya usimamizi wa rasilimali na mali za umma. Ipo barabara ya kilomita 10 ndani ya Jimbo langu la Itigi imejengwa, lakini pia, yako mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia muda wowote ujenzi wa stesheni ya treni ya mwendokasi, ambayo stesheni kubwa itajengwa pale Itigi. Kwa hiyo, mambo haya ya fedha yakisimamiwa vizuri, ninaamini ndani ya Bunge lako hili la Kumi na Tatu, masuala ya usimamizi wa fedha na rasilimali za nchi lazima tuyasimamie kikamilifu, ili kuona nchi yetu inapata manufaa ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mambo mengi sana ya namna ya kudhibiti rushwa. Tunayo Taasisi yetu nzuri kabisa ya Kupambana na Kuzuia Rushwa, hii taasisi inakwenda kufanya makubwa sana ndani ya miaka mitano. Bunge hili tuko tayari kuisaidia hii taasisi, ili wale mafisadi na wala rushwa ndani ya nchi hii, kama ambavyo amechangia mchangiaji mmoja hapa, ndugu yangu Mheshimiwa Kangi Lugola. Bunge hili tuisaidie taasisi hii na Serikali yetu, ili kuhakikisha wale wala rushwa wote na mafisadi wanaoitafuna nchi hii wasiwe na nafasi katika Awamu hii ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda kwenye kipengele cha michezo. Imezungumzwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais kwamba, michezo ni ajira, michezo inaleta furaha, michezo pia, inajenga afya. Tunayo maandalizi ya kupokea *AFCON* 2027 na moja ya jambo ambalo limezungumzwa ni kuanzisha hizo *Sports Academies* kwenye nchi yetu. Sasa ninasema iko haja sasa ya kujenga vituo halisi, nimesikia baadhi ya majibu hapa kwamba, kuna shule zimetengwa, nadhani iko haja ya kujenga shule maalum za michezo angalau kwenye kila kanda ambako tutachuja watoto wadogo na kuwajenga, ili leo na keshokutwa tuwe na wachezaji muhimu sana kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumzia pia, suala la utamaduni ambalo kwa kweli, kama nchi sioni tunalipa kipaumbele sana, sisi kama Taifa la Tanzania tunao utamaduni wetu. Ukiangalia katika masuala ya kiutamaduni jambo pekee ambalo linazungumzwa sana ni Lugha yetu ya Kiswahili, lakini yako mambo mengi ya utamaduni wa Mtanzania bado tumeyaacha hatujayapa kipaumbele. Tunapozungumza utamaduni yapo mambo mengi, mpaka kula ni utamaduni, kusalimiana ni utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo tamaduni zetu kama Watanzania, lakini mambo mengi hatuyapi kipaumbele. Moja ya jambo ambalo tungetamani kuliona kwenye suala la kiutamaduni ni kuhusiana na Tanzania kuwa na vazi letu rasmi. Tumeona kwenye michezo, hata kule *AFCON* yalikuwepo mataifa yanashuka pale wanakuja wamevaa mavazi wanajulikana hawa ni Wanigeria, hawa ni wa wapi, lakini Watanzania ni lini tutakuwa na vazi rasmi la Watanzania, ili ukishuka mahali wanajua Mtanzania ameingia hapa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. YOHANA S. MSITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano, muda ukiruhusu tutaendelea na Timida Mpoki.

Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninakushukuru kwa kuniona. Pili, ninakupongeza kwa nafasi hiyo uliyoichukua hapo. Ninatumia fursa hii pia, kuwapongeza viongozi wetu wengine, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni jembe kwelikweli na tunaamini atatuvusha, nikiziangalia Wizara ninapata matumaini makubwa sana. Ndugu zangu isingekuwa Awamu ya Tano na hii ya Sita hata mimi mtoto ninayetokea kwenye familia ya wawinda ndezi nisingeweza kutokea hapa.

Kwa sababu, ni viongozi wenye maono, wanaogusa nyoyo za watu, basi na mimi nikapata *courage* nikaona kwamba, ninaweza nikafika siku moja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kupata nafasi hii. Pia, ninawashukuru wananchi wenzangu wa Bumbuli kwa kuniamini kwa kura nyingi sana za kishindo, kura 98.4% na Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia, wakamvisha taji kwa kura 98.7%. Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia, kule Bumbuli sisi ametugusa sana kwa sababu, miaka ile ya 2021/2022 hadi 2024/2025, takribani shilingi bilioni 23 zimekuja, kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo. Sasa kwa nini tusimshukuru Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia, tupewe donda tuuguze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baada tu ya hotuba yake hii inayogusa mioyo ya Watanzania, mioyo ya makundi yote na rika zote. Wakati ninatoka hapa nikawa ninafikiria kwamba, hii hotuba inatekelezeka, lakini kabla sijafika kule nikaambiwa shilingi bilioni nne zimeingia. Sasa una nini wewe mpaka usimshukuru Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia na kumpongeza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda moja kwa moja, baada ya pongezi hizi kwa Mheshimiwa Rais, kwenye hotuba yake. Sitagusa mambo mengi kwa sababu, imenigusa sana hotuba hii, hata ukurasa mmoja siwezi kuumaliza, lakini nikipata fursa ya kuandika basi nitaandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya elimu Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hotuba yake inasisitiza Sera ya Elimu; tena elimu ujuzi ndani ya miaka mitano hii. Hili jambo ni kubwa na hakutugusa tu Watanzania, lakini amezigusa na nchi jirani tena mpaka nchi za kimataifa za mbali kwa sababu, hata jirani anaweza akakuonea wivu ukiwa na mipango mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ameligusa kundi la vijana, lakini mkazo ameuweka katika masomo ya hisabati na sayansi. Mimi kwa kuwa ni mwanasayansi yalinigusa siku ileile na nikajua kwa sababu, ndiyo mwakilishi kule Bumbuli, basi nitamsaidia kuwagusa Wanabumbuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akaongeza kwamba, lengo ni kupata wanasayansi wabobezi na hili ndilo tunalolihitaji. Tanzania ya leo, dunia ya leo, bila wabobezi katika sekta mbalimbali ni shida ndiyo maana nina matumaini makubwa sana na sekta zile za miundombinu. Mimi sina wasiwasi, ninajua zitatekeleza, hata kule *TAMISEMI* ninamwona Profesa Shemdoe na sauti yake ya mamlaka na wale wasaidizi wake, ananipa matumaini makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndiyo uone Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia, alivyo kiongozi mwenye maono hata wasaidizi wake hakosei. Angalia kule Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso na msaidizi wake Mheshimiwa Kundo; waangalie Waziri wa Vijana; ndugu yangu Mheshimiwa Makonda. Nilikuwa ninatamani, nikiwa huko nje, siku moja nifanye naye kazi, kumbe Mungu kuna historia anaiandika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya ni maono ya Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia. Hata shule za sekondari za vipaji amezigusa, hivi vitu ni muhimu sana kwa sababu, upo msemo unaosema wajibu wa kwanza usipotekelezwa vizuri, basi hata ule wajibu mkubwa hauwezi ukafana. Ndugu zangu maeneo aliyoyagusa Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia, ni mengi sana, lakini lingine alilowagusa Wanabumbuli ni mambo ya *VETA* kwa sababu, kulingana na jiografia Bumbuli haijakaa vizuri. Ipo ile ya wilaya, lakini bado kwa jiografia haiwezi ikakidhi haja, ninaomba tena hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine alilotugusa Wanabumbuli ni alivyogusa mazao ya chai, parachichi na kahawa. Hapa ametumaliza kabisa, Jimbo la Bumbuli, kata 14 zinalima chai, lakini kwa bahati mbaya viwanda vinasumbua. Ndugu zangu kwenye sekta ya viwanda ninaamini Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia, hajakosea kuwapanga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba wavifikirie viwanda vya chai. Ninakushukuru sana,

ninampongeza Mheshimiwa Rais, lakini ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante. Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo.

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru kwa fursa hii ya kihistoria nami kuweza kuchangia katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Ninaomba nianze kwa kuwashukuru vijana wenzangu wa Kitanzania katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani kwa imani kubwa waliyonipa kuona ninatosha kuweza kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. Ninakishukuru chama changu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani hii kubwa na ninaahidi imani nitailinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais, kwa ushindi wa kishindo. Pia, ninawapongeza wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kutuletea jembe la kazi ambalo sasa limepewa dhamana kubwa ya kuweza kumsaidia Mheshimiwa Rais kutafsiri maono yake katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais, hotuba ambayo binafsi ninaona siyo ya kawaida, ni ya kizazi na mkataba mpya kati ya Taifa na vijana wake. Hotuba ambayo Mheshimiwa Rais amelenga kuwajenga vijana wa Kitanzania ambao wanaweza kushauri, wanaweza kupendekeza, wanaweza kujadili, lakini pia, wanaweza kurekebisha. Ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hotuba kubwa, ambayo imetutambua vijana wa Kitanzania kama nguvu kazi ya kujenga Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais, ametutoa vijana kutoka kwenye neno vumilieni ametuweka kwenye neno shirikini. Ametutoa kutoka kukaa pembeni tukisubiri mipango na mikakati ya Serikali na kutuweka katikati ya sera na

mipango ya Serikali. Hii inaonesha dhamira kubwa ya Mheshimiwa Rais akimaanisha vijana ndiyo walinzi, wajenzi na warithi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutekeleza hayo ameanza utekelezaji kwa kuanzisha Wizara rasmi ya Vijana. Wizara ambayo inafanya kazi kubwa ya kutafsiri maono ya Mheshimiwa Rais chini ya kaka yangu Mheshimiwa Joel Nanauka, ninampongeza sana. Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imejibu maswali ya vijana wengi wa Kitanzania, maswali kama nitapata wapi nafasi na nitafanya nini nikitoka shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais, ameelezea kwa upana suala zima la elimu, suala zima la ujuzi na kutuunganisha vijana na miradi ya kimkakati. Katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais, ameelezea dhamira kubwa ya kuendelea kushirikiana na sekta binafsi ili kuendelea kufungua dirisha la kuwawezesha vijana, ili wawe wawekezaji; yaani *youth investment windows.* Dhamira hii ya Mheshimiwa Rais itatekelezeka endapo vijana hawa wa Kitanzania wataweza kushirikishwa, wataweza kuandaliwa na pia, wataweza kuwa wanufaika wa maendeleo yanayoendelea katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaomba nishauri katika suala zima la kuwekeza na kupanua uwekezaji. Tunavyopanua uwekezaji ina maana tuna-*expand production,* tuki-*expand production* tunapunguza tatizo kubwa la ajira. Hapa Tanzania tuna vijana wenye tatizo la ajira wa aina mbili; yaani wale waliomaliza la saba na *form four,* lakini pia, wale ambao wamemaliza vyuo vikuu. Ninaomba tunavyoandaa mifumo mizuri ya hawa wawekezaji katika Taifa letu, basi tuhakikishe tunaandaa mfumo mzuri ambao utahakikisha hawa wawekezaji wanaajiri vijana wetu kutokana na *skills* walizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hotuba yake amejikita katika kuelezea namna ambavyo anataka kutatua changamoto ya ajira. Hivyo, kwa vijana wenzetu ambao wako vijijini tumeona namna nzuri

ambavyo Mheshimiwa Rais amewavuta kutoka pembezoni na kuwaweka katikati ya msingi wa uchumi wa Taifa letu kupitia miundombinu, kupitia maji, kupitia kuimarishwa kwa Benki za Maendeleo, lakini pia, kupitia kilimo cha kisasa na umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tumemwona Mheshimiwa Rais katika hotuba yake akielezea kwa upana suala zima la uvuvi na uchumi wa bluu. Hapa, ametuhakikishia kwamba, baada ya kumalizika kwa Bandari ya Uvuvi ya Kilwa ajira, takriban 30,000, zinaenda kutengenezwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie kwa kusema, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetupa vijana sikio kubwa kwa kutuambia, vijana Serikali imewasikia, Serikali imewazingatia, lakini pia, Serikali ya Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan ipo tayari kutembea nasi kwa safari ya miaka mitano ijayo. Kwa niaba ya vijana wenzangu tunamwomba Mheshimiwa Rais aendelee kujenga miundombinu kwa sababu, kujenga miundombinu ni kujenga ndoto za kijana wa Kitanzania; ni ajira wakati wa ujenzi, ni ajira panapomalizika kwa ujenzi, lakini pia ni fursa kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya vijana wa Mkoa wa Mbeya na vijana wote wenzangu wa Tanzania Bara na Visiwani tunaunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa, kwa dhati ya moyo wangu, lakini pia, kwa matumaini makubwa mazito. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tumemaliza majina. Muda wetu umeisha na majina bado mengi; tutakaporudi mchana tutaanza na Mheshimiwa Agnesta Lambert, atafuatiwa na Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Ussi

Yahya, atafuatiwa na Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka. Wengine tutawataja kadri muda unavyokwenda.

Nina tangazo moja. Wageni waliopo mchana huu ndani ya ukumbi wetu, wote mnawaona. Hawa ni wageni 215 wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Waziri wa Madini. Hawa ni wanafunzi na Walimu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Bunge kutoka Kikombo, Mkoani Dodoma. Tunaomba watoto wetu msimame na muwapungie mikono maana hii shule imejengwa na hawa Wabunge. Ahsanteni sana na karibuni sana kwenye Bunge letu kwa ajili ya kujifunza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, ninasitisha Kikao cha Bunge, mpaka Saa Kumi na Moja Jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Hapa Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Hati za kuwasilisha Mezani.

**SPIKA:** Hati za kuwasilisha Mezani, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kanuni.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**MHE. DANIEL B. SILLO – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KANUNI ZA BUNGE:**

Maelezo kuhusu Azimio la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kanuni kuhusu Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni ya 165 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA KAMATI

### Azimio la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kanuni za Bunge kuhusu Marekebisho ya Kanuni za Bunge

**MHE. DANIEL B. SILLO –MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KANUNI ZA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali yote kwa ujumla na kwa ushirikiano wanaolipatia Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni ya 179(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Kanuni za Bunge kuhusu Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni 165.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeundwa chini ya Kanuni 140 ya Kanuni. Mojawapo ya jukumu la Kamati ni kujadili na kupendekeza maboresho ya Kanuni za Kudumu za Bunge kama ilivyoanishwa katika Kifungu 3(3)(a) katika Nyongeza ya Nane.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Januari, 2026 Kamati ilibaini changamoto ya matumizi ya Kanuni 165 kuhusu utambulisho wa wageni wanaofika Bungeni. Kanuni ya 165 inamtaka Mheshimiwa Spika kutambulisha wageni mashughuli wa Kitaifa na Kimataifa na mgeni mwingine yoyote ambaye ametoa mchango kwa Kitaifa unaohitaji kuenziwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na masharti hayo wageni wengine wanaofika Bungeni kwa kualikwa na Wabunge au kufanya ziara za mafunzo hawapati fursa ya kutambulishwa. Kamati ilijadili na kuona kwamba upo umuhimu wa Kanuni ya 165 kuboreshwa ili kuwezesha wageni wengine wanaofika Bungeni kutambulishwa.

Mheshimiwa Spika, Bunge kama chombo cha uwakilishi wa wananchi hupokea wageni wengi wanaofuatilia Shughuli za Bunge kwa kulitembelea ili kuona namna linavyofanya kazi na kufuatilia kazi nzuri zinazofanywa na Wabunge wao pamoja na kufanya miadi na wawakilishi wao.

Mheshimiwa Spika, hivyo kutambulisha wageni ni jambo linalolifanya Bunge liwe karibu na wananchi na kuwafanya wafurahie Bunge lao. Aidha, kwa upande mwingine wageni hujifunza mambo mbalimbali yanayohusu Bunge, shughuli za Bunge na utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hizo Kamati inapendekeza Kanuni ya 165 iboreshwe kwa kuandika upya Kanuni ndogo ya (2) na kuongeza Kanuni ndogo ya (3) ili kuweka masharti yanayoruhusu wageni wengine kutambulishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hiyo, ninaomba sasa kuwasilisha mapendekezo ya Maboresho ya Kanuni ya 165(2) na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na endapo Bunge hili litaridhia na kupitishwa kwa njia ya Azimio zitatumika, ambapo marekebisho hayo yatasomeka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 165(1) Spika anaweza kuwatambulisha wageni mahsusi wa Kitaifa na Kimataifa waliopo katika Ukumbi wa Bunge. Kanuni Ndogo ya (2) Spika anaweza kuwatambulisha wageni wengine ambao:

(a) Wametembelea Bunge kwa mwaliko wa Wabunge;

(b) Wametembelea Bunge kwa ajili ya ziara za mafunzo; na

(c) Wametoa mchango wa Kitaifa unaohitaji kuenziwa.

Mheshimiwa Spika, Kanuni Ndogo ya (3) Spika atawatambulisha wageni kwa utaratibu atakaoona unafaa katika Kikao cha Bunge kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, Kamati inapendekeza Bunge lijadili na kuridhia na kupitisha mapendekezo ya Kamati kwa njia ya Azimio kwa mujibu wa Kanuni 179(1) na (2).

Mheshimiwa Spika, hitimisho; ninawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kanuni za Bunge kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kujadili na kuandaa mapendekezo ya marekebisho haya. Ninaomba majina ya Wajumbe yaingie katika *Hansard* za Bunge. Vilevile ninaishukuru Sekretarieti chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu Baraka I. Leonard kwa utaalam na uratibu wa shughuli za Kamati hadi kufanikisha na kumamilisha kazi hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha mapendekezo ya Kamati ili Bunge lijadili na baadaye kupitishwa kwa njia ya Azimio mabadiliko ya Kanuni ya 165 yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

**MHE. DANIEL B. SILLO – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KANUNI ZA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Baada ya hoja kuungwa mkono, ninaomba niwasilishe Azimio la Bunge kuhusu mpendekezo ya kufanya marekebisho au mabadiliko katika Kanuni za Bunge, hii imetolewa chini ya Kanuni ya 179(1) na (2) na Kifungu cha 3(3)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

KWA KUWA katika Bunge hili imejitokeza changamoto ya matumizi ya Kanuni ya 165 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, kuhusu utambulisho wa wageni wanaotembelea Bunge letu;

NA KWA KUWA ni utamaduni uliozoeleka katika Bunge letu na Mabunge ya Jumuiya za Madola kufanya maboresho au mabadiliko katika Kanuni zinazotumika kwa njia ya kurahisisha utekelezaji wa Shughuli za Bunge;

NA KWA KUWA Kanuni zetu zinaruhusu kufanyika maboresho ya Kanuni ili kuondosha changamoto iliyopo ya kuwatambulisha wageni wanaotembelea Bunge kwa mwaliko wa Bunge au Waheshimiwa Wabunge na wageni wanaofika kwa ziara ya mafunzo;

NA KWA KUWA Kamati ya Kudumu ya Kanuni za Bunge ilifanya uchambuzi wa changamo hiyo ya matumizi ya Kanuni ya 165, kuhusu utambulisho wa wageni na kupendekeza Bungeni kufanyika kwa mabadiliko ya Kanuni hiyo;

NA KWA KUWA Kanuni ya 140, 179(1) na (2) na Kifungu cha 3 (3)(a) cha Nyongeza ya Kanuni ya Nane ya Kanuni, kwa pamoja vinatoa mamlaka kwa Kamati ya Kanuni kujadili na kutoa mapendekezo juu ya kufanya marekebisho au mabadiliko katika Kanuni na kuwasilisha Bungeni mabadiliko ya Kanuni za Bunge kwa njia ya Azimio;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba mapendekezo ya marekebisho au mabadiliko ya Kanuni za Kudumu za Bunge kama ilivyowasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 179 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 yanapitishwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante, hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutachangia kwa dakika mbili mbili kuhusu Azimio hili kama kawaida ya Kanuni zetu. Ninaanza

na Mheshimiwa Timotheo Mnzava, hajafika? Mheshimiwa Paresso, jiandae Mheshimiwa *Advocate* Olelekaita.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya maboresho ya Kanuni ya 165.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida binadamu yeyote anapenda kutambuliwa bila kujali hali yake na kwa kuwa hili ni Bunge la wananchi na sisi ni wawakilishi wa wananchi. Katika kutelekeza majukumu yetu msingi wetu mkubwa ni wananchi wale tunaowawakilisha, wakati fulani wananchi hawa wanapenda kufika na kuona mazingira na maeneo ambayo wawakilishi wao tunafanya kazi ama kujifunza au kushuhudia wenyewe kwa macho yao, kwamba mwakilishi wao anafanya nini, basi ni busara na hekima na ni muhimu sana wananchi wanapofika waweze kutambuliwa na wakaona haya mazingira kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii muhimu, wageni wote wanapofika ndani ya Bunge waweze kutambuliwa. Ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa *Advocate* Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Kwa kuwa ninazungumza kwa mara ya kwanza, ninamshukuru Mwenyezi Mungu na wananchi wa Kiteto kwa kunipa heshima ya kurudi tena Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kama Mjumbe wa Kamati ya Kanuni za Bunge ninakupongeza wewe na Kamati kwa kuona haja ya kuleta mabadiliko ya Kanuni ili kuruhusu Watanzania ambao ndiyo wametuleta hapa kuwapa heshima ya kutambulishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni tulizonazo sasa Mheshimiwa Spika alikuwa anaweza tu kutambulisha wale wageni wa Kitaifa na mashuhuri, lakini sasa kwa mabadiliko haya wananchi wetu ambao wanapenda sana kutembelea Bunge hili

kama sehemu nzuri ya historia ya Taifa letu, wana haki ya kutambulishwa na wakapata na wao kumbukumbu hiyo kwamba wamefika mbele ya Bunge hili na kwamba wamewafuata wale waliowachagua kuja hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo maamuzi haya na mjadala kwenye Kamati yetu ni maamuzi sahihi sana na imefuata taratibu zote kama alivyosoma Mheshimiwa Naibu Spika kwamba mabadiliko ya Kanuni hizi zinaongozwa na Kanuni ya 179 kama ilivyosemwa kwamba ilijadiliwa na sasa ipo mbele ya Bunge kama Azimio.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya sasa makundi yote ya Kitaifa, Kimataifa, mashuhuri wale wanaotembelea Bunge na kwa ajili ya mafunzo watapata fursa hii muhimu sana ya kutambulishwa mbele ya Bunge hili. Kwa hivyo, ninawashawishi Wabunge kwamba mabadiliko haya yapite haraka sana tena kwa nguvu kama risasi hivi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya hata Wabunge walishaanza kunong'ona kwamba inawezekanaje kumtoa mwananchi kutoka Mbeya ama kutoka Kagera au Makete kilomita 1000 ama 500 anakuja hapa halafu aondoke kimya kimya tu hajatambulishwa! Kwa hiyo, maamuzi haya ni maamuzi mazuri sana yenye tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hili ni jumba la wananchi na wananchi wanaruhusiwa kuja saa yoyote.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Ado Shaibu.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuunga mkono hoja. Kwa hiyo la kwanza ninatamka kwamba ninaunga mkono hoja hii. Msingi wa kuunga hoja hii ni Katiba hii, ambayo ndiyo inayotuongoza.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 63(2) inasema, sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndiyo chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, hii maana yake ni kwamba tunatekeleza wajibu wetu kwa niaba ya wananchi, wenye Bunge hili ni wananchi, kwa hiyo wananchi wanapofika na kutembelea Bunge wanatembelea chombo chao kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, ukipata hata *privilege* ya utambulisho ni kama unawatia ugeni ndani ya nyumba yao wanayoimiliki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninatamka kwamba ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Kimsingi kama walivyotangulia wachangiaji wenzangu chombo hiki ni chombo cha wananchi, ni haki yao ya kutambulishwa.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwamba wananchi na wageni mbalimbali wanaoingia kwenye jengo hili wapate fursa ya kupata utambulisho. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mtoa hoja.

**MHE. DANIEL B. SILLO – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KANUNI ZA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninakushukuru tena kwa kunipa nafasi niweze kuhitimisha hoja ambayo ipo mbele yetu ya Azimio la Bunge la kuwatambulisha wageni au wananchi wanaofika katika Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, wamechangia Wabunge wanne, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Olelekaita Kisau, Mheshimiwa Ado Shaibu pamoja na Mheshimiwa Asia Halamga.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote hawa waliopata nafasi ya kuchangia wameunga mkono hoja hii ambayo ipo mbele yetu wakitambua kwamba chombo hiki cha Bunge ni Chombo cha Wananchi na tuliopo humu ndani wote ni Wawakilishi wa Wananchi na tupo kwa niaba yao. Nimefurahi sana kwamba Waheshimiwa Wabunge wanalitambua jambo hili ni jambo lao ni jambo la wananchi wao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge likubali Azimio la Bunge kwamba wageni wote na wananchi wanaoingia katika Bunge hili watambulishwe.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji wanaoafiki Azimio la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kanuni za Bunge kuhusu Marekebisho ya Kanuni za Bunge, kwamba wageni wote na wananchi wanaoingia katika Bunge hili watambulishwe.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru kwa kukubali kupitisha marekebisho ya Kanuni ya 165 ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025. Kwa marekebisho haya sasa, wageni wanaotembelea Bunge letu watatambulishwa na hivyo kuliweka Bunge letu karibu na kuwafanya wananchi wafurahie Bunge lao. Aidha, hatutachapisha vitabu vipya vya Kanuni badala yake marekebisho haya ya Kanuni yatasomwa sambamba na Kanuni za Kudumu za Bunge 2025. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

**Hotuba ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa Ufunguzi Rasmi wa Bunge la Kumi na Tatu, Tarehe 14 Novemba, 2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala. Walishatangazwa wachangiaji wa jioni tunaanza na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, wajiandae Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja na Mheshimiwa Maryam Ussi Yahya.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami kama walivyofanya Waheshimiwa Wabunge wengine, niweze kuchangia machache katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Awali ya yote ninaomba kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia uzima na afya na siku ya leo nipo ndani ya Bunge hili Tukufu nikiwa ni Mbunge wa Jimbo la Segerea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namba mbili, ninaomba kwa moyo wa unyenyekevu na moyo wa shukrani, niwashukuru sana wananchi na wapiga kura wa Jimbo la Segerea walioniamini wakanichagua kwa kura nyingi kura zilizoniwezesha siku ya leo niko hapa nami ninaitwa ni Mbunge wa Jimbo la Segerea. Ahadi yangu kwa Wanasegerea, bila kujali itikadi za chama, dini, wala rangi, wala kabila, ahadi yangu kwao ni kwamba, ile imani waliyonipa, kwamba nije kuwa sauti ya wao, nitakwenda kuwa sauti yao, lakini zaidi sana changamoto zao zote nitakwenda kuziwasilisha ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hoja ni moja, ni kuhusiana na Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwanza kabisa nikiri kabisa kwa moyo wangu wa dhati, kwamba Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekidhi matakwa yote ya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati ninasema imekidhi matakwa yote ya wananchi wa Tanzania ninaomba niseme kwamba wakati Mheshimiwa Rais anatuhutubia ndani ya Bunge hili, alionesha utu mkubwa sana kwa kutupongeza sisi Wabunge tuliopenya katika majimbo yetu na tukawa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa utu huo alioutumia, ninaomba nitumie utu huo huo kumpongeza kwa moyo wa dhati kwa jinsi ambavyo ameshinda kiti hiki cha Urais na leo ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo kwa Mheshimiwa Rais, ninaomba sasa kwa moyo wa upole na unyenyekevu nitoe pole nyingi kwa wananchi wa Jimbo la Segerea kutokana na yale yote yaliyotokea tarehe 29 Oktoba, 2025.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu kuwa ndani ya Jimbo la Segerea wapo waliokumbwa na kadhia iliyoonekana na kutokea katika maeneo mengine. Nitumie nafasi hii kuwapa pole nyingi sana, lakini kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Segerea kwa jinsi ambavyo wamekuwa watulivu, kwa jinsi ambavyo baada ya tarehe 29 wote kwa pamoja, pamoja na maumivu tulikubaliana kwamba tunakwenda kutulia tunakwenda kutanguliza amani yetu kwanza na mambo mengine baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo la tarehe 29, ninaomba nichukue nafasi hii tena kumpongeza Mkuu wetu wa Wilaya (*DC)* Edward Mpogolo pamoja na Mkurugenzi wetu Elihuruma; kwa sababu hawa wawili wametusaidia kama Wilaya ya Ilala kuwa ni wamoja, kusimama pamoja katika kipindi hiki. Niseme ndani ya Bunge hili Tukufu, kama wapo wakurugenzi na wakuu wa wilaya wanaomsaidia Mheshimiwa Rais kutimiza majukumu yake huko chini basi. mkuu wangu wa wilaya yuko kwenye tano bora na mkurugenzi wangu yupo kwenye tano bora.

Nitumie nafasi hii kuwaomba waendelee hivi hivi kutuunganisha kama Watanzania na kutusaidia tuweze kupata maendeleo kwa kuwa maendeleo hayana chama, wala kabila, wala hayana rangi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais yapo niliyojifunza mengi, lakini kwa sababu ya muda ninaomba niseme kwamba, Hotuba ya Mheshimiwa Rais imejaa uwajibikaji, hotuba yake imejaa utawala bora, imejaa nia njema na ya wazi ya kuwaletea Watanzania maendeleo. Kwa sababu hiyo nitakwenda moja kwa moja kujikita katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais kwenye ukurasa wa tisa, pale alipoongelea suala la kwenda kuwainua vijana, wanawake na wenye ulemavu kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze kwanza Mheshimiwa Rais kwa kuliona hili; lakini nikiri kwamba hata kabla ya hotuba yake tulikwisha kuona jinsi ambavyo mikopo hii ya 10%, chini ya uongozi wake alisema mikopo hii itakuwa mikopo isiyokuwa na riba kabisa.

Mheshimiwa Spika, tunakumbuka mikopo hii ya 10% imekuwepo miaka nenda rudi chini ya watangulizi wa Mheshimiwa Rais waliotangulia, mikopo hii ilikuwa inaitwa mikopo yenye riba nafuu. Hata hivyo, mikopo chini ya Mheshimiwa Rais ni mikopo isiyokuwa na riba kabisa.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mwigulu kwa jinsi ambavyo ameikonga mioyo ya Watanzania, hususani Wanailala na zaidi sana Wanajimbo la Segerea kwa majibu mazuri aliyoyatoa jana wakati ninamwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Inawezekana hayupo mitandaoni, lakini ninaomba nimwambie, kwamba wananchi wamepokea majibu yake kana kwamba tumezaliwa upya leo. Nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu ashikirie pale pale katika yale aliyoyaongea ili yale aliyoyasema yaonekane kwa vitendo, kwamba hakika Serikali iliyoko madarakani ina nia njema ya kumkomboa kijana wa Kitanzania, ina nia njema ya kumkomboa mwanamke na wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Mheshimiwa Rais pamoja na nia njema kabisa ya Serikali ninaomba niseme, kwamba hatuwezi kwenda kuyapata haya aliyoyasema ikiwa walioko chini yake hawatakwenda kuwajibika. Tumesikiliza mwelekeo wake tulikotoka, tulipo na anapotaka kutupeleka, lakini haitasaidia jambo lolote...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** *Ooh my God!* Ninaomba dakika moja niwa ... *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante. Mheshimiwa Nyamizi Saimon Mhonga, jiandae Mheshimiwa Mariam Ussi Yahaya.

**MHE. NYAMIZI S. MHOJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba jina langu la mwisho lisomeke Mhoja na siyo Muhoga. Ahsante.

**SPIKA:** Kwa hiyo kaa chini, siyo wewe. Au ndiye wewe sasa? Haya endelea.

**MHE. NYAMIZI S. MHOJA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, awali ya yote nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kibali chake na neema yake kwa kuniwezesha kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi chini ya kiongozi wetu, Mwenyekiti wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na uongozi wote wa CCM, hasa kabisa CCM Mkoa wa Tabora pamoja na Idara zake zote, pamoja na wapiga kura wangu, ninasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wenye ulemavu tuna mambo mengi ya kuzungumza juu ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ili niweze kueleweka vizuri ninaomba nitoe tafsiri kidogo ya ulemavu ni nini? Ulemavu maana yake ni mtu mwenye upungufu wa muda mrefu kimwili, kiakili, hisia au afya ya

akili ambayo anapokutana na vikwazo mbalimbali, vikwazo hivyo mfano vikwazo vya kimazingira, vikwazo vya miundombinu, mitazamo hasi ya jamii na mifumo ya huduma katika jamii ambayo humzuia kushiriki kikamilifu na usawa katika jamii yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hapa; hata wale watu wa *formula;* tunaona kabisa kwamba kama hakuna vikwazo basi hakuna ulemavu. Ulemavu upo kwa sababu kuna vikwazo. Hiyo ni *simple formula* tu. *No* vikwazo *no* ulemavu. Kwa tafsiri hiyo nipende kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo mengi mazuri aliyoyafanya angalau kuondoa vile vikwazo kwa sisi watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niyataje kati ya mengi ambayo ameyafanya Dkt. Samia Suluhu Hassan katika uongozi wake. Cha kwanza kabisa ni kwa mara ya kwanza sisi watu wenye ulemavu kutambulika kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa upekee wetu. Tumetajwa kabisa, kwamba ni watu wenye ulemavu, kuendeleza michezo kwa watu wenye ulemavu, imetaja kabisa kwa upekee wetu. Kwa hiyo, hiyo ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipeleke pia pongezi zangu kwa Tume Huru ya Uchaguzi ya Mwaka huu 2025. Wote ni mashahidi, siku ile ya kuzindua kampeni pale Kawe Dar es Salaam Mheshimiwa Rais alizindua kitabu mahususi kwa ajili ya watu wasioona; na hiyo ni mara ya kwanza kabisa. Haijaishia hapo tu, Tume yenyewe ilitushirikisha watu wenye ulemavu kuanzia ngazi ya kwenye mchakato mpaka mwisho. Ili nieleweke vizuri, wametushirikisha na sisi tukashiriki vizuri katika nini? Kwenye vituo vyote vya kupiga kura kwa mara ya kwanza, sisi wenye ulemavu tumejitokeza kwenda kupiga kura kwa sababu tu vile vituo ni rafiki kwa sisi watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, rafiki kivipi? Kile kituturu cha kupigia kura, kile kiboksi cha kukaa kilikuwa rafiki. Ukienda kutokana na aina ya ulemavu wewe mwenye ulemavu, mfano mwenye *wheel chair* kinatengenezwa kinawekwa kwa namna

kwamba ana uwezo wa kukaa mwenyewe kupiga kura kwa siri. Si hivyo tu, siku chache kabla ya uchaguzi Tume yenyewe ilitoa elimu kwa watu wasioona Tanzania nzima, zaidi ya 800, jinsi ya kutumia kifaa kwa ajili ya kupigia kura kwa wasioona, kinaitwa *tactile ballot folder* ambacho ni mpapaso, kinamwezesha mwenye ulemavu anapiga kura bila kuwa na msaidizi. Wote tunafahamu kuwa suala la kupiga kura ni siri na faragha. Tulikuwa tunapoteza kura zetu kwa sababu nitamwaminije yule msaidizi? Kama tutatofautiana maisha yataenda atanipigia kule anakotaka yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru pia Serikali hii hii imetushirikisha katika Dira ya Taifa ya Maendeleo. Pia katika hotuba yake ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nyamizi ahsante kwa mchango mzuri, muda wako umepita. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. NYAMIZI S. MHOJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Ussi Yahaya, ajiandae Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka.

Waheshimiwa Wabunge kuna orodha hapa ya kuchangia ya wajumbe wa kuchangia kama 20. Hatutaweza kuwachukua wote kutokana na muda. Tuna Mawaziri saba na kuna ku-*wind up* hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, niwaombe hawa waliobakia wote watachangia kwenye mpango kuanzia siku ya Jumatatu; na mpango unaendana sawa sawa na Hotuba ya Mheshimiwa Rais sababu ndio mwongozo ambao amekwishautoa na mpango utahusiana na hii ratiba, kwa hiyo, tutakuwa na wajumbe watano au sita baadaye tutaikaribisha Serikali.

Mheshimiwa Mariam Ussi, wajiandae Mheshimiwa Kassimu Amari na Mheshimiwa Yannick Ndoinyo.

**MHE. MARIAM USSI YAHYA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, nami niungane na Wabunge wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijaalia mimi kuwepo hapa siku ya leo. Pia nimshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ushindi wake wa kishindo wa kutuwezesha na sisi wa Viti Maalum kuweza kuingia katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika muktadha huo huo, niwapongeze Wabunge wote wa CCM na wasiokuwa wa CCM kwa kuweza kuingia katika Bunge hili. Nikupongeze nawe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi yamesemwa. Ninaomba kwanza kuchukua nafasi hii kukushukuru pia kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan aliyoitoa tarehe 14 Novemba 2025.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi yamesemwa, kwa hiyo nisingependa niyarudie. Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejaa maono makubwa sana ya kuipeleka nchi yetu mbele katika miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nijikite katika eneo moja tu, na nitakuwa-*very brief*. Ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuanzisha Wizara ya Vijana. Ningeomba pia kiufupi kabisa kuwaomba watendaji wote, hasa Waziri wa Vijana na Naibu wake pamoja na Serikali kuhakikisha kwamba wanayafikia maono ya Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuwasimamia vijana. Mheshimiwa Rais ameonesha nia yake madhubuti na tunu yake ya kuwasaidia vijana wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kubwa kabisa ninaloliomba hasa katika Wizara ya Vijana ni kuhakikisha kwamba Baraza la Vijana la Tanzania linafanya kazi. Baraza hili lilipitishwa tangu 2013 katika

Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika nchi zote, ukiondoa nchi ambazo zimeingia hivi karibuni, mabaraza haya yanafanya kazi. Kwa hiyo, kutokuwa na Baraza la Vijana katika nchi yetu kunawapunguzia fursa kubwa sana vijana wetu wa Tanzania ambao wanapata haki sawa kwenye baraza hili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Baraza hili lingewawezesha wao kupata ajira, kufanya *joint venture* na nchi jirani na kuweza kujiinua kiuchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuweza kuzitumikia na kuzipata, kama wenzao wao wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, fursa zote ambazo vijana wanazipata katika Jumuiya. Kwa hiyo ningemwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe sasa, miaka 11 imekwishakuwa mingi sana kwa hawa vijana kutokuweza ku-*enjoy* hizi *benefits za* Jumuiya katika Baraza la Vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamwomba sana pia kuhakikisha kuwa katika sera zake anatunga sera madhubuti ambazo ataunganisha vijana na Wizara zingine za kisekta kama Kilimo, Uwekezaji, Biashara na Madini. Vijana wasiachwe tu kupewa mashamba wakalime, vijana wanaweza kuwa katika madini na wanaweza kuwa katika uwekezaji. Tuwekeze kwa vijana, ambao ndani ya miaka mitano tutajivunia kwamba kuna vijana milionea; na Mheshimiwa Rais Samia ndilo hilo analolitaka.
Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka, jiandae Mheshimiwa Yannick Ndoinyo.

**MHE. KASSIMU A. MBARAKA:** Shukrani sana Mheshimiwa Spika. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia kufika katika Bunge hili Tukufu baada ya mbilinge mbilinge za muda mrefu sana na uchaguzi huu. Ndoto hii kutimia toka mwaka 2010 na hatimaye 2025 imetimia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo ninamshukuru sana Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

pamoja na Kamati yake yote ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kwa kunipitisha na kuwa Mgombea Ubunge Jimbo la Tanga Mjini na hatimaye kuwawakilisha watu wa Tanga ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Rais ni pana sana imeeleza maeneo mengi sana; lakini kwa muhtasari kuna maeneo muhimu sana yanayogusa jamii ambayo ninapenda nijikite hapo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais ameeleza kwa muhtasari kuwa lazima sheria za nchi hii sasa zifike mahali ziandikwe katika Lugha ya Kiswahili. Kwa heshima kubwa ninapenda kusema kwamba ninaishukuru Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kupitia Baraza la Kiswahili Taifa (BAKITA); jambo hilo tayari limeanza kufanyika na kazi inaendelea; sheria nyingi kuandikwa katika Lugha ya Kiswahili badala ya kuwepo katika Lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, hii tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba Watanzania wengi ambao ni waswahili wanajua Kiswahili, wataweza kuzisoma sheria hizi vizuri na wataweza kufanya shughuli zao za kiuchumi na kimaendeleo bila changamoto yoyote na kubabaishwa kokote kule; kwa sababu watakuwa wanafanya kazi katika misingi ya kisheria na sheria wanazozijua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ninapenda sana kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hususani kwenye upande wa mitaala ya elimu. Mitaala hii imeleta mageuzi na mabadiliko makubwa sana. Hapo zamani katika suala zima la elimu na kujifunza tumekuwa kwa kiwango kikubwa sana mfumo wetu wa elimu uko katika upande wa *cognitive domain*. Hapa nimezungumzia istilahi ya kiualimu. Yaani nikizungumzia *cognitive* ninazungumzia maarifa zaidi na nadharia zaidi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa upana jambo la elimu linakuwa na nukta kubwa za msingi tatu kwenye kupata maarifa. *Cognitive domain*, *psychomotor domain* and *affective domain*.

Hivi vyote ni muhimu. *Cognitive* inahusika na maarifa. *Psychomotor* inahusika na *skills* au ujuzi na *effective domain* inahusika vile vile na suala zima la maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tunaona ujio wa mitaala mipya imeingiza kwa kiwango kikubwa sana *Psychomotor domain skills,* ujuzi na ndiyo ulimwengu wa leo unahitaji watu wenye ujuzi. Haya ni mageuzi na ni mabadiliko makubwa sana. Kongole kwa Wizara ya Elimu kwa kumsikiliza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuhakikisha mitaala hii imekaa katika mfumo huu wa kiutendaji. Leo hii kijana akimaliza kidato cha nne aliyesoma mkondo wa amali anapata cheti cha *NACTVET* pamoja na cheti cha *NECTA*. Tayari ana ujuzi na anaweza kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo niseme kwamba Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameifanyia mambo mengi sana Tanzania yetu. Upande wa Tanga kumefanyika uwekezaji ndani ya Bandari ya Tanga takriban bilioni 429.1 zimewekezwa. Bandari hii imekuwa leo ni tegemeo ya lango kuu la uchumi Afrika Mashariki na *SADC*. Tunaona meli zinaingia kwa wingi, zinashusha mizigo, zinapakia mizigo. Kwa shughuli hizi za kiuchumi na Bandari ya Tanga imefufuka. Jambo hili ni kubwa limefanyika na kuandika historia mpya ya Tanga wakati wa Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiasi hicho cha pesa kilichoekezwa kimeleta tija nyingi sana ndani ya Jiji letu la Tanga. kimeongeza idadi ya ajira za watumishi hadi kufikia ajira takribani 457 za watumishi na vibarua au wafanyakazi wa kutwa ajira takribani 17,871 kutoka ajira 6650 za wafanyakazi wa kutwa. Haya ni mabadiliko na ni mageuzi makubwa sana kwenye upande wa Bandari ya Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, ukisikiliza hotuba yake Mheshimiwa Rais anaeleza pia kuhusiana na azma ya kufufua viwanda. Hapa ninapoeleza Tanga tulikuwa na kiwanda cha chuma kimekufa, kimepoteza mwelekeo ndani ya siku 100 za Rais Samia kiwanda kimefufuka kimeanza kuzalisha nondo za milimita 16 na milimita

12. Tulikuwa na kiwanda maarufu cha sabuni aina ya *FOMA*. Leo hii kimefufuka na sabuni zinazalishwa Tanga na viwanda Tanga vimeanza kurejea. Haya ni mazuri ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya uchukuzi, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ndani ya Jimbo la Tanga Mjini amewekeza bilioni 78 kuhakikisha uwanja wa ndege wa Tanga unajengwa wa kisasa mzuri ili ndege mbalimbali ziweze kutua. Ukiacha haya vilevile tayari mchakato wa kuifufua *meter gauge railway* umeanza miaka 20 iliyopita reli hii ilikuwa imekufa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuja kuifufua reli ya Tanga ya *meter gauge railway* inabeba mizigo leo kutoka bandarini na kuelekea sehemu mbalimbali za Kilimanjaro na Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiacha hayo anaenda kujenga reli ya kisasa *SGR* ndani ya Jimbo la Tanga, kutoka Tanga - Kilimanjaro - Arusha - Singida mpaka Musoma kilomita 1128. Haya ni mambo makubwa na ni maono makubwa ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mambo hayo makubwa aliyofanya lazima tuyaelezee kwa wivu mkubwa, tuyalinde kwa wivu mkubwa na kumsifu popote pale tutakapokuwepo kwa kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Rais ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo hotuba imejaa maono mapana sana ya nchi hii na kuonyesha dira wapi nchi yetu inaelekea ndani ya 2030 inayokuja. Hivi ninavyowaambia Barabara ya Tanga - Segera itaenda kupanuliwa takribani kilomita 72 kutoka Tanga Mjini, haya ni mambo makubwa haya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa.

**MHE. KASSIMU A. MBARAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Yannick, ajiandae Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi. Nitumie muda huu kuchangia kwa unyenyekevu na kwa upendo mkubwa hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwanza niwashukuru sana Wanangorongoro walionichagua kuwa Mbunge wao, lakini pia waliomchagua Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kura nyingi sana zilizomfanya yeye kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninawashukuru Chama Cha Mapinduzi. Kwa kweli niwapongeze sana viongozi wote waliochaguliwa kuongoza Bunge hili na Serikali pamoja na Wabunge, hongera sana kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Wabunge wengi na wote wamezungumza wamesema mambo mengi mazuri miradi mingi iliyofanywa ya kimkakati ndani ya nchi yetu ya Tanzania na katika majimbo yetu mbalimbali. Sifa ni nyingi na kwa kweli Mama Samia anastahili hizo sifa kwa sababu ni Rais mchapakazi na msikivu sana. Ninashukuru sana kwa sababu wametuonyesha sisi Wabunge wapya nini kinafanyika huku kwetu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatokea Wilaya ya Ngorongoro na michango yangu itaenda sehemu kuu tatu. Kwanza kama mnavyojua mimi ninatoka wilaya ambayo uhifadhi na utalii na ufugaji ni vyanzo vikuu vya uchumi na mapato ya wananchi. Kwa muda mrefu sana hicho ndicho tunachomshukuru sana Mama Samia.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na minong'ono ya sintofahamu kubwa sana kati ya wahifadhi na wananchi kuhusu maeneo ya hifadhi. Kwa kweli tunamshukuru Mama Samia ameingilia kati ameleta utulivu ambao mambo yameanza kutulia kabisa na tunamshukuru na matumaini yetu makubwa sana kwamba mambo yanaenda kuwa mazuri. Wananchi wana imani na upendo na wanamsubiria kwa hamu kwa mambo mengine mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wilaya yetu ya Ngorongoro ni kanda ya uzalishaji, ni kanda ya ufugaji, ni kanda ya utalii. Lengo la Serikali ya Mama Samia ni kuongeza watalii wafike milioni nane ndani ya miaka hii mitano. Tukitengeneza miundombinu kikamilifu kwa mfano barabara nyingi za lami kama nilivyosema itaongeza idadi ya watalii hata hiyo milioni nane ikawa ni idadi ndogo sana kwa sababu kila mahali kutafikika.

Mheshimiwa Spika, kule kwetu Loliondo na Ngorongoro kwa ujumla watalii wanapata ugumu kufika maeneo nyeti kwa sababu ya ugumu wa barabara na ninatumaini kwamba sisi sasa tunaenda kujengewa barabara. Kwa hiyo, hotuba hii na kwa ahadi yake Mama Samia kwa sababu bahati nzuri nilishiriki naye kwenye kampeni na ameahidi kwamba kwa kweli atatutengenezea barabara hizo na kazi imeshaanza kuonekana na ile barabara inayotoka Roduwale na Geti la Ngorongoro kwenda Serengeti na yenyewe imeshaanza kutengenezwa. Kwa hiyo, kwa kweli kuna vitu vingi sana tunapenda kumshukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunachoomba sekta ya ufugaji ni sekta ya uzalishaji, tunataka kuona sekta hiyo ikiongeza pato la wananchi na pato la Taifa. Kwa hotuba hii na kwa *commitment* yake hii sekta inaenda kuboreshwa pamoja na kwamba maeneo ya ufugaji malisho yataongezeka na hiyo sekta yenyewe itaenda kuboreshwa zaidi iwe ya uzalishaji kuongeza pato la Taifa, lakini kuongeza pato la wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunampongeza sana Mama Samia kwa sababu amewateua viongozi wanaomsaidia kazi ambao pia ni wasikivu sana. Hapa ninayo orodha karibu ya Mawaziri sita ambao wako tayari kutembelea Wilaya ya Ngorongoro na kuona shughuli za wananchi, kuona changamoto na kusaidia namna ya kutatua. Kwa kweli binafsi nimefarijika sana na wananchi wa Ngorongoro wanawasubiri kwa hamu ili wote kwa pamoja tumsaidie Mama Samia ili azma yake anayoitaka basi tuifikie na ile Tanzania tunayoihitaji wote tuifikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mawaziri siyo wasaidizi peke yake wa Rais, pia kuna viongozi wengi, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na Watendaji wa Vijiji na Kata wote ni wasaidizi wa mama Samia na inatakiwa wote wachangamke wote waende kwa hiyo *speed* ili sasa changamoto ambazo tunaziona na azma ambazo tunataka ku-*achieve,* basi wote tuweze kufikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja na ninaomba Watanzania na Wanangorongoro wenzangu tuunge hii hoja mkono kwa sababu hii ndiyo njia itakayotufikisha Tanzania na Kanaan tunayoitaka. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mgore Miraji, ajiandae Mheshimiwa Baraka Ambindwile Ulimboka

**MHE. MGORE M. KIGERA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa siku ya tarehe 14 Novemba, 2025 wakati akihutubia Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa chama changu pendwa Chama Cha Mapinduzi chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi kwa kuweza kuniamini na kuniona ninatosha na kuniteua kuwakilisha na kupeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi katika Jimbo la Musoma Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haikuwa rahisi sana kama unavyojua huko tunakotoka sisi Mkoa wa Mara ni Kanda Maalum na Jimbo la Musoma Mjini tangu uhuru ndiyo kwa mara ya kwanza wameweza kumchagua Mbunge mwenye jinsia ya kike ambaye ni mimi nimesimama hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu uhuru tumeandika historia kwa kumchagua Rais mwanamke, mwanamama mahiri, hodari na

shupavu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa ushindi wa kishindo wa 97%. Wengi wanashangaa kwa nini 97%? Aliyoyafanya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Tanzania hii, kwa Mkoa wa Mara na kwa Jimbo langu la Musoma Mjini alistahili kupata hata 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda niwashukuru wananchi wa Jimbo la Musoma Mjini kwa kuonyesha kuwa wanawake tunaweza na Musoma inaenda kubadilika chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan wa muhula huu wa pili nami mwakilishi wao Mgore Miraji Kigera.

Mheshimiwa Spika, ninatoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais kwa ushindi wa kishindo yeye na makamu wa Rais Dkt. Emmanuel Nchimbi. Ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchagua Baraza la Mawaziri ambalo ni baraza lenye weledi mkubwa likiongozwa na Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba. Mawaziri hawa wameonesha ni namna gani wanaenda kukimbizana na kasi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kufuatia hotuba yake ya tarehe 14 Novemba, 2025.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nijikite katika utekelezaji wa majukumu makubwa ambayo amepanga kuyafanya kwa Watanzania hasa wa Jimbo la Musoma Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika uwekezaji ameelekeza ataenda kuhakikisha kongani za viwanda zinaongezeka Tanzania hii kama ilivyo Kwala, Buzwagi pamoja na Bagamoyo. Katika suala hili niombe Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji Naibu Waziri alifika Musoma na akafika katika Kiwanda cha *MUTEX* na pale tayari mwekezaji ameshapatikana na yuko katika makubaliano na Serikali ili aweze kuja kuwekeza na wananchi wa Jimbo la Musoma Mjini waweze kupata fursa za ajira na uchumi uweze kufunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami kama Mbunge wa jimbo hilo ninamwomba Naibu Waziri wa Uwekezaji kwa kushirikiana na Waziri Mkuu mwekezaji huyu aweze kupewa eneo la ekari 11.73 ambapo ndipo kuna kiwanda tu na nafasi inayobaki ya ekari 13

waweze kuweka viwanda vidogovidogo na fursa za ajira ziweze kuongezeka kwa wananchi wa Jimbo la Musoma Mjini.

Mheshimiwa Spika, kwani kwa kutoa eneo lote kwa mwekezaji mmoja itakuwa ni changamoto kama ilivyokuwa hapo nyuma. Kwani kiwanda hiki toka mwaka 1994 kilivyoweza kupewa mwekezaji wawekezaji wawili aina tofauti wameshindwa kufanya vizuri na hivyo kufanya wananchi wa Musoma Mjini wasiweze kupata fursa ya ajira pamoja na uchumi katika jimbo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais niongelee pia suala la uwekezaji katika sekta nzima ya uchukuzi. Katika sekta ya uchukuzi nimpongeze Mheshimiwa Rais ameweza kuleta fedha bilioni 35 ya kuweza kujenga Uwanja wa Ndege wa Musoma na leo Naibu Waziri wa Uchukuzi amethibitisha mbele ya Bunge lako Tukufu mwezi Machi wanaenda kufanya *first flight* katika ku-*test* uwanja huo. Hivyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais na ninamshukuru kwa kutujalia watu wa Musoma kuweza kupata uwanja wa ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya uchukuzi Mheshimiwa Rais anaenda kujenga Reli ya kutoka Tanga - Arusha mpaka Musoma ya kilomita 1108. Reli hii inaenda kufungua fursa ya uchumi na ajira katika Jimbo la Musoma Mjini. Wananchi wa Musoma Mjini wameteseka kwa muda mrefu, lakini kwa kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na haya mambo anaenda kuyafanya kwa kupitia hotuba yake, tabasamu la kweli linaenda kupatikana katika Jimbo la Musoma Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika sekta hii ya uchukuzi niendelee kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi awasisitize *TRC* kuna hoteli ya Musoma na juzi Naibu Waziri wa Mipango na Uchukuzi na Uwekezaji alikuwa pale, alishuhudia Musoma Hotel na mwekezaji ameshapatikana na wanatarajia kufunga mkataba ifikapo Juni ili aweze kuwekeza kwenye hoteli hiyo na iwe hoteli ya nyota tano. Ninaomba Waziri wa Uchukuzi uweze kutusaidia kupitia *TRC* na hoteli hii iweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye sekta ya uvuvi. Mheshimiwa Rais amegusa wavuvi wa kufuga samaki kwa kutumia vizimba. Sisi Musoma tunategemea ziwa na sasa hivi samaki wengi wamepotea ziwani tunategemea vizimba ili tuweze kupata samaki na vijana wetu waweze kupata fursa ya ajira. Katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ameongelea kusaidia upatikanaji wa chakula cha samaki kwani ndiyo imekuwa changamoto katika Jimbo la Musoma Mjini kwa wafugaji wa samaki kupitia vizimba. Nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi aweze kulisimamia hili ili wananchi wa Musoma Mjini waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niguse katika sekta binafsi ambapo ni mikopo, hii mikopo ya halmashauri ya 10% ninaomba kunukuu hotuba ya Mheshimiwa Rais katika ukurasa wa 16: *"Fedha hizi ni mikopo na siyo msaada, ni mbegu na siyo mavuno na ni mtaji na siyo ruzuku."*

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aweze kutusaidia katika hili, halmashauri nyingi wamekuwa fedha hizi hawafanyi kama ambavyo ni matarajio ya Mheshimiwa Rais na katika Jimbo langu, Halmashauri ya Manispaa ya Musoma watu walikopeshwa fedha milioni 543 na mpaka sasa fedha hizo hazijarejeshwa na inasemekana waliokopeshwa hawajulikani.

Mheshimiwa Spika, sasa kama waliokopeshwa hawajulikani fedha hizo zilitokaje? Nimwombe Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI akishirikiana na Mkurugenzi wa Manispaa ya Musoma waweke jicho kwenye fedha hizi ziweze kurudishwa na waweze kukopeshwa akinamama na vijana na watu wenye mahitaji maalum. Fedha hizi milioni 543 zitaenda kwa vikundi vya watu 10, 10 takribani vikundi 110. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, kausha damu inatesa wanawake wa Musoma Mjini. Tuombe watu wakopeshe watu ambao wana vigezo na zisiwe fedha za kutoka kwa kupendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuanza kutoa tabasamu kwa wananchi wa Musoma Mjini kwani katika ujenzi wa Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ambayo iliweza kusimama kwa takribani miaka 30 amekuja kuikamilisha na hospitali hiyo inatoa huduma zilizo bora. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mgore.

**MHE. MGORE M. KIGERA:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 14 Novemba, 2025. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Baraka Ulimboka wajiandae Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunenge na Amour Seif Abdalla.

**MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa uzima na uwezo wa kufika siku ya leo katika jambo ambalo kama Watanzania tunatakiwa kujisikia sifa na nguvu kubwa ni juu ya hotuba hii ambayo aliitoa Mheshimiwa Rais mbele ya Bunge lako Tukufu. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri aliyoitoa, lakini pia kwa ushindi mkubwa alioupata katika uchaguzi uliofanyika mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ninasimama kwa mara ya kwanza pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kyela ambao kwa heshima kubwa wamenipa kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu kwa maana ya kunipa ushindi wa kishindo. Pia nimshukuru Mwenyekiti wangu wa Chama Cha Mapinduzi, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo alinipitisha kwenye Kamati Kuu na kwenye halmashauri kuu kuwa mimi nikawe mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kyela. Ninashukuru sana sana mimi ni mtoto wa mkulima sikustahili, lakini yeye amenistahilisha kwa kunipa nafasi hii na kuteuliwa kuwa mgombea wa Chama Cha Mapinduzi kupitia Jimbo la Kyela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wanakyela tunakubali na tunakubaliana na hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Rais siku ya kulizindua Bunge hili Tukufu. Katika mambo mbalimbali ambayo aliyasema, mimi ninayasoma na kuona kuwa yameonyesha maono mbalimbali ambayo Mheshimiwa Rais anaenda kuyafanya katika miaka mitano inayokuja.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii pia ameonyesha nia njema ambayo ameifanya katika miaka minne iliyopita na sisi wananchi wa Kyela tunakiri katika miaka minne iliyopita ametuboreshea mambo mbalimbali yakiwemo mambo ya afya. Mfano ndani ya Jimbo la Kyela ametuwezesha kupata zaidi ya shilingi bilioni 4.5 kwa ajili ya ujenzi wa kituo wa hospitali ya wilaya pale kwa ajili ya jengo la mama na mtoto, sisi Mheshimiwa Rais tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ametoa fedha mbalimbali kwa ajili ya vituo vya afya kama Kituo cha Afya cha Matema, Ngisi na maeneo mbalimbali ndani ya Jimbo la Kyela. Hivyo tunaona katika kurasa mbalimbali za hotuba yake alionyesha mipango aliyokuwa nayo ndani ya miaka minne iliyopita, lakini ndani ya miaka mitano inayokuja.

Mheshimiwa Spika, sisi wananchi wa Kyela kwa niaba yao ninasema tunashukuru sana, ndani ya kitabu hiki amezungumza pia kuwa anaenda kuanzisha na kuongeza upatikanaji wa umeme vijijini. Niishukuru Serikali kupitia mpango huo ambao tumesaini juzi wa zaidi ya vitongoji 9,000 ambapo kwangu nimepata vitongoji 31. Ninashukuru sana. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kama alivyosema kwenye hotuba yake na Wananchi wa Kyela tunamshukuru. Hivyo, nimebakiwa na vijiji 52. Ninashukuru kwa vijiji 31 nilivyovipata.

Mheshimiwa Spika, katika kilimo pia tunamshukuru Mheshimiwa Rais. Ukurasa wa 20 amesema anaenda kuongeza uwezekano wa umwagiliaji katika maeneo mbalimbali na pia kilimo biashara ili wananchi waweze kulima. Ninashukuru pia ndani ya Jimbo letu la Kyela tuna mradi mkubwa ambao

tumepewa zaidi ya shilingi bilioni 20.5 ambazo zimeenda kutolewa katika Skimu ya Umwagiliaji ya Makwale.

Mheshimiwa Spika, kupitia hiyo skimu ya umwagiliaji itaenda kuongeza tija kwa wananchi wa Ndobo, wananchi wa Kata ya Makwale na wananchi wa Kata ya Lusungo kwa kuwa tunaenda kuongeza tija katika kilimo ili wananchi wale waweze kulima kwa wakati wote na hasa zao la mpunga.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo yote hayo, nimshukuru Mheshimiwa Rais katika hotuba yake anasema na katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imeandikwa kuwa: "Tunaenda kuongeza na kuweka Gridi ya Maji ya Taifa." Niombe; jambo hili kwetu kule ni changamoto kubwa sana. Ninashukuru sana kwa miradi ya ambayo iko ndani ya Jimbo la Kyela ikiwemo Mradi wa *Ngana Group,* Mbambo na Lema, yote hiyo ni miradi ambayo inaenda kutekelezwa ndani ya Jimbo la Kyela, lakini pia, kuna Mradi wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni moja tu, na Waziri wa Maji yupo hapa, yule mkandarasi ninaomba ahamasishwe kama kuna chochote anadai niombe sana aweze kulipwa ili wananchi wa Kyela Mjini waweze kupata tabasamu lile ambayo iko ukurasa wa mwisho wa hotuba ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake pia amezungumza kuongeza fedha za *TARURA*. Kyela; maombi haya niyaombe kwa umuhimu wa pekee sana. Sisi kule bondeni ndiyo wilaya ya mwisho kuelekea sehemu ya Ziwa Nyasa. Niombe mambo haya mawili tuweze kupewa kipaumbele. Kwanza, kuongezewa bajeti ya *TARURA* kwa sababu muda mwingi miundombinu yetu inaharibiwa kwa sababu ya hali ya hewa na kule kwa sababu tuko mwishoni muda mwingi tunapata mafuriko.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, hata juzi nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika kule Kyela na tuliongea kwa muda mrefu sana. Tuliomba na nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu aliniuliza mafuriko unasema kila siku, lakini tufanyeje ili kuboresha

hayo mafuriko yasiwakute Wanakyela. Tuliongea mambo mengi na ninaomba leo niwasilishe kama maombi ya Wanakyela. Tujengewe mabwawa yale mabwawa tunaamini yatasaidia mambo mawili. kwanza, yatasababisha tusipate mafuriko ndani ya bonde letu la Kyela na ndani ya Wilaya ya Kyela.

Mheshimiwa Spika, mabwawa yale yatatumika kwenye umwagiliaji ili tuwe na uhakika wa umwagiliaji, kwa sababu mito tunayo na mito ipo muda wote ndani ya Jimbo langu la Kyela. Niombe ili nisipigiwe kengele ya pili niunge mkono hoja. Ninaipongeza sana Serikali na ninampongeza sana Dkt. Samia kwa hotuba nzuri yenye maono ya miaka mitano ijayo ambayo tunaamini kuwa tunaenda kuifanikisha Nchi ya Tanzania kwenda katika hatua ya maendeleo makubwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni jioni hii.

Wapo Wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika: kuna wageni wawili ya Mheshimiwa Naibu Spika kutoka Mkoani Arusha, Ndugu Litiko Januari Mwang'onda, kada wa CCM Mkoa wa Arusha, na Mhandisi Ismail Mgana, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya *Rapid Oversee Elevator*. Karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa, mchangiaji wetu sasa ni Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunenge, jiandae Waziri wa fedha na Waziri wa TAMISEMI. Mheshimiwa Mwalunenge, hayupo? Mheshimiwa Amour Seif Abdalla.

**MHE. AMOUR SEIF ABDALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Siyo Omar Seif Abdallah ni Amour Seif Abdallah, Mbunge wa Jimbo la Wete. Ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ikiwa leo hii ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu hili. Kwanza kabisa, ninampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ushindi mkubwa alioupata. Vilevile, ninampongeza Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushindi mkubwa ambao ameupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, niipongeze hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa maono, lakini kwa uzalendo mkubwa ambao umejaa katika katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Ninaomba nichangie katika sehemu mbili: sehemu ya sekta ya anga na sehemu ya uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, sote tunajua kwamba hakuna ncho yoyote inayoweza ikaendelea bila kuhakikisha kwamba inasimamia sekta ya anga na uchukuzi vizuri, lakini tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa sababu ameiboresha sekta ya anga kwa kuhakikisha kwamba ametuletea ndege ya mizigo. Ile ndege ya mizigo imesababisha ongezeko la kampuni za *logistic* zile *air cargo* zimeongezeka. Kwa hiyo, niipongeze Serikali na nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutuletea hii ndege ya B767 ya uchukuzi. Niombe, katika hotuba yake amesema kwamba ataongeza ndege nane tena katika kipindi cha 2025 - 2030. Ninaishauri Serikali katika zile ndege nane ndege nne ziongezwe ziwe ni za *air cargo* kwa sababu itaongeza kipato cha wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Rais kwa mambo ambayo ameyafanya, ninampongeza kwa kuimarisha Viwanja vya Ndege kama vya Arusha na Dodoma kesho kutwa kinakamilika lakini vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kushirikiana na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa kutujengea hata sisi Kiwanja cha Pemba kinakuwa ni cha kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba kwa sekta ya uchukuzi pia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya vitu vikubwa sana, ameboresha mifumo ya uendeshaji ya bandari zetu. Hii imepelekea katika hotuba yake amesema imeweza kuokoa zaidi ya shilingi bilioni 258. Hii yote ni kwa sababu ya kazi kubwa ya Mheshimiwa Rais ambayo anaifanya katika sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, ameboresha vilevile Bandari ya Mwanza, Bandari ya Tanga kama Mbunge aliyepita hapa alisema sasa hivi Tanga wanashusha magari pale. Vilevile, juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu katika sekta ya uchukuzi alizindua meli ya kisasa yenye

ghorofa tatu. Hii yote ni kwa sababu ya maono na uzalendo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuboresha mifumo ya bandari zetu hususan Dar es Salaam. Sasa hivi mizigo imejaa pale, mabasi na malori yanapishana kusomba mizigo ijapokuwa foleni imeongezeka, lakini ninachompendea Mheshimiwa Rais bwana, anapofanya maendeleo changamoto ya foleni pale ile njia ya Kilwa pamoja na ile ya Uhasibu inaongezeka, lakini ameshasema kwamba anajenga reli ile ya *SGR* pamoja na bandari kana kwamba malori hayataingia tena mjini kwa ajili ya kusitisha ile foleni pale.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mheshimiwa Rais Samia anapoleta maendeleo na zinapokuja changamoto anakuwa tayari ana utatuzi wa lile tatizo. Kwa hiyo, tumpongeze Mheshimiwa Rais ile foleni pale itamalizika, kwa sababu malori hayatoingia tena mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tumeona uboreshaji wa bandari ya uvuvi wa kisasa. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais katika sekta ya uchukuzi na anga ameboresha sana, lakini niiombe Serikali wakati tunafanya kampeni ya uchaguzi Mheshimiwa Rais pia alivyokuja Pemba aliahidi kwamba itajengwa Bandari ya Wete na ile Bandari ya Wete ni bandari ya pili kwa ukusanyaji wa mapato Zanzibar, *TRA* na *ZRA*.

Mheshimiwa Spika, sasa niiombe Serikali iharakishe ujenzi ujenzi wa Bandari ya Wete, kwa sababu Bandari ya Wete ni bandari ambayo inachukua *channels* nne: *channel* ya Dar es Salaam, *channel* ya Unguja, lakini vilevile tunategemea *channel* ya Mombasa pamoja na Tanga. Kwa hiyo, itakapotengenezwa ile Bandari kuwa ya kisasa mapato ya *TRA* yataongezeka lakini na uchumi wa mtu mmoja mmoja pale Wete utaongezeka. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ihimize ujenzi huu kwa ajili ya manufaa ya wananchi wa Kaskazini Pemba, lakini kwa manufaa ya Serikali pia.

Mheshimiwa Spika, katika mambo haya mema na mazuri ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyafanya,

niseme kwa hotuba hii na kwa sehemu hizi ninaomba niunge mkono hoja hotuba hii. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, jiandae Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na jiandae Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kwa jina la Mwenyezi Mungu Rahman na Rahim na ninaomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwemo katika Bunge lako hili Tukufu. Ninasimama kwa mara ya kwanza, kwa hiyo, ninaomba nitumie fursa hii vilevile kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwanza kwa kuniteua kuwa Mbunge, pili, kwa kuniteua kuwa miongoni mwa wasaidizi wake kwa dhamana ya Uwaziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba vilevile,nichukue fursa hii kukishukuru sana Chama changu cha CCM pamoja na Wabunge wa CCM kwa kuniteua kuwawakilisha katika Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM (*NEC)*. Ninakushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi lakini ninataka nitumie fursa hii kuwashukuru Naibu Mawaziri wangu wawili: Mheshimiwa Mshamu Ali Munde na Mheshimiwa Laurent Deogratius Luswetula kwa msaada mkubwa ambao wamekuwa wakinipa tokea tumekabidhiwa majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka nitumie fursa hii pia kutoa pongezi kwanza kwa Mheshimiwa Rais kwa ushindi wake wa kuwa tena Rais wa Jamhuri ya Muungano katika kipindi cha pili, yeye pamoja na mgombea mwenza wake Dkt. Emmanuel Nchimbi. Vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushindi wake; Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu kutuongoza timu ya Mawaziri, Waheshimiwa Mawaziri wote, wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote kwa imani waliyoipata kwa wananchi na kupitia vyama vya siasa ambavyo wanaviwakilisha humu ndani ya baraza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya kipindi kilichopita ya utekelezaji wa kazi za Serikali katika kipindi hiki kilichopita yameelezwa kwa kiasi katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, lakini yametolewa ushuhuda mkubwa na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili katika majimbo yao. Kila Mbunge aliyesimama ameeleza kwa kina kile ambacho kimefanyika katika jimbo lake na huu ni ushuhuda mzuri kwa Waheshimiwa Wabunge kwa yale ambayo yamefanyika kwa ajili ya kutekeleza na kutatua changamoto mbalimbali za wananchi.

Mheshimiwa Spika, sikusudii kwenda sana katika kipindi kilichopita lakini ninaomba mchango wangu ujikite katika eneo la muhimu, eneo la tunakokwenda ambalo hili nalo limeelezwa kwa uzuri sana na Mheshimiwa Rais katika kitabu hiki hasahasa kuanzia ukurasa wa 14 mpaka 34. Takribani kurasa 21 za hotuba hii zilijikita katika mwelekeo wa Taifa letu katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, kazi ya ujenzi wa Taifa ni kazi nzito, ni kazi ambayo inahitaji ustahamilivu mkubwa, kazi ambayo inachukua muda mrefu na inayohitaji wakati mwingine kutoka jasho na wakati mwingine kuingia vumbi kidogo. Ni kazi ya lazima na lazima ifanywe na wa kuitekeleza ni sisi wananchi na kwa hapa Bungeni ni sisi ndio tunawawakilisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, tumepiga hatua kubwa katika miaka 60: tokea mwaka 61 uhuru na mwaka 64 Muungano, lakini bado tuna kazi kubwa iliyopo mbele yetu ya kuendeleza maendeleo ambayo yameanzwa katika kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Spika, Taifa letu lina takribani Watanzania milioni 71 sasa hivi kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2022 na kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2050, tunatarajia tutafikia Watanzania milioni 118 ifikapo mwaka huo 2050. Taifa hili linaundwa na Watanzania walio wengi ambao ni vijana na sehemu kubwa ni watoto. Sasa ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Rais ilijielekeza sana kwenye utekelezaji wa dira ambapo kuna mambo matatu makubwa aliyazungumza na yametajwa katika dira: ujenzi wa uchumi imara, jumuishi na shindani; uwezo wa

watu na maendeleo ya jamii; na uhifadhi wa mazingira, ustahamilivu wa mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, katika suala la ujenzi wa uchumi hotuba imejikita zaidi katika suala la ujenzi wa sekta binafsi, ukuaji mkubwa wa uchumi na mageuzi makubwa ya kiuchumi kwamba ukuaji unategemewa sasa kupindukia 7% katika kipindi chote hiki cha kuelekea mwaka 2030. Sekta mbalimbali zimeelezwa, ukuaji mkubwa sekta ya kilimo kutoka asilimia nne ya sasa ifikie 10%. Viwanda kutoka asilimia 4.8 mpaka asilimia tisa, madini mchango wake ufikie 10% kutoka 6.8% ya sasa na utalii tuweze kufikisha watalii milioni nane kutoka milioni tano waliopo sasa.

Mheshimiwa Spika, mambo haya yote yanahitaji rasilimali kubwa ya kuweza kutekelezwa na ukiangalia azma hasa iliyopo ni kutumia rasilimali zetu za ndani iwe za kilimo, mifugo na mazao ya majini (baharini na kwenye maziwa) kuleta maendeleo makubwa ya viwanda katika miaka mitano inayokuja.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais vilevile amezungumzia sekta wezeshi, ukiziangalia zote ni sekta za miundombinu nako ameeleza miradi mikubwa ya kimkakati ambayo itaendelea kutekelezwa na mingine mipya ambayo inakusudiwa kutekelezwa katika kipindi hiki ikiwemo ya kukamilisha maeneo yaliyobakia ya vipande vya ushoroba wa Reli ya *SGR* kuhuishwa Reli ya *TAZARA,* miundombinu mingine kama ya bandari, viwanja vya ndege, maji safi na salama na makazi.

Mheshimiwa Spika, sasa katika hili kunahitajika rasilimali nyingi za ndani. Tunakusudia kuelekea kwenye Taifa linalojitegemea na maana yake ni kwamba tunahitaji kukusanya zaidi mapato ya ndani yale ambayo yanakusanywa ya kodi na *TRA* na maduhuli mbalimbali ya Serikali. Huku Wizara yetu ya Fedha itakwenda kujitahidi kukusanya zaidi kwa tabasamu kama ambavyo imeelezwa bila kuitweza sekta binafsi. Tutakusanya mapato kuhakikisha tunapata mapato ya kuendesha Serikali na kutekeleza miradi yetu lakini mapato ambayo yatasaidia ukuaji wa sekta binafsi badala ya kuikandamiza na kuiua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakusudia vilevile kutumia njia nyingine mbadala za mapato, hasahasa ushirikiano wa sekta binafsi na sekta ya umma *(PPP)* ambayo pamoja na kwamba tumekuwa na sheria, lakini bado haijaweza kufanya kazi vizuri. Kama ambavyo inatarajiwa kwenye dira yetu 70% ya mapato yetu yatokane na sekta binafsi na hili litahitaji ushirikiano mkubwa wa sekta binafsi na sekta ya umma na ushirikiano miongoni mwa watendaji wa Serikali, lakini bado ni jambo ambalo linawezekana.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuahidi kwamba katika kipindi kinachokuja tutashirikiana sote na Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kwamba azma ya maendeleo yetu inatimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, ninaomba niunge mkono hoja. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante. Mheshimiwa Shemdoe - Waziri wa TAMISEMI; jiandae Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni mara yangu ya tatu leo kusimama mbele ya Bunge hili, lakini niendelee tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ametupa fursa hii kuwa pamoja hapa. Niwapongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan; Mheshimiwa Dkt. Nchimbi; na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Viongozi wetu hawa ambao ni viongozi wakuu wanatuongoza na wanatuongoza vema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze nawe pia pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote watatu ambao mnatuongoza vema katika Bunge hili la Kumi na Tatu. Nipende kumshukuru tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniteua kuwa Waziri katika Ofisi wa Waziri Mkuu ninayeshughulikia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba ya Mheshimiwa Rais wamepongeza hotuba hii nzuri sana ambayo imeeleza mambo mengi ambayo yamefanyika kwenye kipindi chake cha kwanza toka 2021 hadi 2025. Mambo muhimu

yaliyopongezwa ama yaliyozungumzwa ni kwenye elimu, afya ya msingi, miundombinu 10%, umaliziaji wa miradi viporo, upatikanaji wa watumishi na nidhamu ya watumishi ambapo ni mambo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamepongeza, lakini vilevile wameendelea kuyaomba ili tuweze kuyasimamia.

Mheshimiwa Spika, sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tunapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa fedha nyingi ambazo amehakikisha zinatolewa na kupeleka tabasamu kwa wananchi kwenye kipindi chake cha kwanza ambacho ameongoza Serikali na nchi yetu. Tutaendelea kuhakikisha kwamba, tunamwomba Mheshimiwa Rais aridhie fedha nyingi zaidi, ili ziweze kwenda kwenye maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameendelea kuyaomba; maeneo haya tumeyasikia asubuhi, barabara, maeneo ya shule na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yote haya kwenye kipindi kijacho tutahakikisha kwamba, tunaomba fedha hizi. Bajeti inakuja hapa, tutawaomba Waheshimiwa Wabunge waweze kuipitisha na tuombe sasa kutekeleza na kuleta tabasamu kwa wananchi wa Tanzania hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya TAMISEMI imeendelea na itaendelea kusogeza huduma za msingi karibu na wananchi kwa kuimarisha miundombinu na kuboresha ubora wa huduma za afya, elimu, barabara za vijijini na mijini, pamoja na huduma nyingine za kijamii, ili kila Mtanzania popote alipo aweze kunufaika na maendeleo ya Taifa hili. Kwenye siku 100 za Mheshimiwa Rais, kwenye muhula wake wa pili, sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumepokea watumishi 12,000; 7,000 wa sekta ya elimu na 5,000 wa sekta ya afya. Watumishi hawa wamekuwa *posted* kwenye halmashauri zetu na tunaendelea kusimamia ugawaji wake, ili waende kwenye maeneo ambayo yana upungufu na yanahitaji huduma hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa huduma za afya kwenye ngazi ya msingi. Tuna jumla ya vituo 7,673 zikiwemo zahanati 6,445 vituo vya afya 1,034 na hospitali 194 za halmashauri ambazo zinatoa huduma. Tunaahidi kwamba, kwa

kipindi hiki cha miaka mitano tutahakikisha kwamba, huduma mujarabu inaendelea kutolewa na inapatikana kwa wananchi na Watanzania wote, ili tuweze kuleta tabasamu kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya elimu. Mheshimiwa Rais ameleta fedha nyingi kwenye maeneo haya kwenye kipindi kilichopita, lakini tunaendelea na sisi kumwomba na tuna hakika kwamba, tutapata fedha ambazo zitatusaidia kuimarisha elimu ya msingi. Wote mnafahamu mwaka 2028 tunaenda kukutanisha madarasa mawili yanayomaliza shule ya msingi kwa hivyo, tutahakikisha kwamba, tunajiandaa vizuri, ili isije ikatokea msongamano wowote katika kipindi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji, kupitia fedha ambazo amezileta Mheshimiwa Rais, tumejitahidi sana kuhakikisha kwamba, tunakuwa na matumizi mazuri ya TEHAMA. Tunahakikisha kwamba, tutaendeleza matumizi haya ya TEHAMA kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha uongozi wa Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumejitahidi sana kuongeza ukusanyaji wa mapato. Mwaka 2021/2022 tulikuwa tunakusanya shilingi bilioni 757, lakini leo hii ninavyokwambia tumefikia kukusanya shilingi trilioni 1.4 kwenye mamlaka zetu za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakuhakikishia kwamba, tutasimamia, hakutakuwa na uvujaji wa fedha za mapato ya ndani, tutasimamia hakutakuwa na ulaji wa fedha mbichi kwenye halmashauri zetu. Kwa namna hii tunategemea kwamba, ndani ya kipindi kifupi tutaweza kukusanya shilingi trilioni mbili ambayo ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba, tujitahidi kukusanya mapato ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikienda kumalizia ninaomba nizungumzie kidogo suala la kuimarisha utawala bora kwenye Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa. Katika kuhakikisha kwamba, azma ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan,

inatekelezwa tumeanza kazi kwa nguvu kubwa; tumetembelea mikoa 19 toka tumeingia ofisini, tumetembelea miradi ya maendeleo na tumetoa maelekezo mbalimbali. Maelekezo haya tunaendelea kuyafuatilia kuhakikisha kwamba, yanafanyiwa kazi, ili kuleta tabasamu kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Kumi na Tatu, tutekeleze majukumu yetu kwa uzalendo, weledi, mshikamano na kushiriki Mabaraza ya Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha suala la uwazi na utawala bora linafanyika vizuri, ninaomba nichukue jukwaa hili kwenye Bunge lako hili Tukufu kuwaelekeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri na Mameya kwamba, tunapoandaa vikao vyetu vya fedha, uchumi na mipango, viandaliwe siku za Jumamosi, kipindi ambacho Wabunge wapo Bungeni ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuhudhuria vikao hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa kutumia jukwaa lako hili ninaomba niwaelekeze wakurugenzi wa halmashauri wa nchi nzima kwamba, wanapopokea fedha za miradi ya maendeleo wahakikishe wanawajulisha Waheshimiwa Wabunge kwa maandishi. Nitajitahidi sana mahali popote pale wenzetu wa Hazina wanapopeleka fedha na mimi nitahakikisha kwamba, ninawajulisha Waheshimiwa Wabunge kwa barua, ili waweze kufuatilia miradi hii ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, anaridhia fedha hizi ziende kwenye majimbo yetu, ziende kwenye halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninachukua fursa hii kusema ninaunga mkono hoja. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Shemdoe. Sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Paul Makonda ajiandae.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa uongozi wako tangu tulipoanza vikao na kujadili hotuba hii muhimu sana ya Mheshimiwa Rais wakati akifungua Bunge letu la Kumi na Tatu. Ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema pia, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniteua mara mbili kuwa Mbunge wa Bunge hili na hatimaye akanikabidhi kazi ya kuongoza Wizara ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa ushindi mkubwa alioupata pamoja na chama chake, Chama Cha Mapinduzi. Ushindi huo msingi wake ni sifa zake yeye mwenyewe, sifa na uimara wa chama kilichopata uongozi na pia, sera ambazo zimetekelezwa na kuleta mafanikio makubwa hapa nchini. Pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Rais, ninampongeza Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar, pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutuongoza vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumza maeneo mawili yanayohusu sekta zangu mbili. Kwanza ni uvuvi; kuhusu uvuvi sera ya jumla ni kuvua kisasa, kuvua kibiashara na kuvua kwa tija. Ili tufikie malengo hayo inabidi tuwe na usimamizi madhubuti wa rasilimali za uvuvi. Katika hili Hotuba ya Mheshimiwa Rais iko bayana kwamba, itabidi twende haraka kuanzisha chombo au mamlaka ya usimamizi na udhibiti wa rasilimali za uvuvi. Hili ni jambo kubwa sana lililoko katika moja ya ahadi kubwa za Mheshimiwa Rais katika Sekta ya Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kubwa ni kuelekea kukamilisha ujenzi wa bandari ya kwanza nchini, Bandari ya Uvuvi Mkoani Lindi huko Wilayani Kilwa. Bandari hii ni ya aina yake, haijawahi kujengwa, kukamilika kwake Mwezi Machi mwaka huu, 2026, kutafungua milango ya nchi yetu kunufaika na uvuvi wa Bahari Kuu. Uvuvi wa Bahari Kuu mlango wake unafunguliwa Tanzania na baada ya kufunguliwa kwa mlango huo halitakuwa tena shamba la bibi la watu kwenda huko Bahari Kuu na kutuibia samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, gharama ya bandari hii ikikamilika itakuwa imetumia shilingi bilioni 280.6 pesa za Watanzania kwa 100%. Kwa kupitia njia hiyo tutakuwa tuna uwezo wa kupata ajira 300 za kudumu; tutaweza kupata ajira za wachakataji wa samaki na wafanyabiashara ndogondogo katika maeneo hayo ya mradi unaokaribia watu 7,800. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa bandari hii unaambatana pia na ununuzi wa meli ya mafunzo kwa mabaharia na wataalam wa uvuvi hapa nchini. Meli hiyo itagharimu shilingi bilioni 15.2. Kwa ufupi, Sekta ya Uvuvi ni sekta ambayo itaweza kufungua milango, siyo tu kupatikana kwa ajira, lakini pia, kupatikana kwa viwanda na kuongeza thamani ya samaki hapa nchini. Ndiyo maana shirika letu la uvuvi linaanza kufufuka na kwa mara ya kwanza limeanza kununua meli, ambayo mwezi ujao tutaipokea hapa nchini, kwa mara ya kwanza nchi yetu kumiliki meli ya uvuvi. Tayari zabuni zimefunguliwa, meli nyingine mbili zitanunuliwa, ili kufikisha meli tano ifikapo 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaenda kwenye eneo la Sekta ya Mifugo kwa ufupi. Jambo la kwanza kubwa ambalo limefanyika ni kufungua soko la nyama nje ya nchi kwa ng'ombe, kondoo pamoja na mbuzi. Mwaka 2019/2020 nyama iliyokuwa inauzwa nje ilikuwa chini ya tani 1,000, lakini kutokana na hatua mbalimbali za Serikali na kuboresha mazingira ya biashara hadi mwaka jana, 2025, nchi imeweza kuuza tani 13,000. Tukijipanga vizuri, kama ambavyo mkakati wetu unaonesha, tunajipanga kuuza nyama nje ya nchi tani 50,000. Hii ni habari njema kwa wafugaji *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa za kuboresha mifugo kwa programu ya chanjo, ambayo ilizinduliwa mwaka jana na Mheshimiwa Rais, pamoja na utambuzi wa mifugo, utafungua zaidi masoko ya nyama nje ya nchi. Sasa hivi tuko katika mazungumzo na Nchi za China na Misri kuwauzia nyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kufanya vizuri katika sekta ya nyama pamoja na maziwa, Serikali imepanga kuunganisha Bodi za Nyama na Maziwa, ili kiwe chombo kimoja imara kuweza

kushughulikia bidhaa zote. Hii itapunguza hata gharama ya uendeshaji ya Serikali, lakini pia, wawekezaji nao watapata huduma chini ya chombo kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado hatufanyi vizuri katika eneo la maziwa, lakini ziko dalili njema kwa sababu, mpaka sasa tunavyo viwanda sita vya kusindika maziwa. Mwelekeo ni kwamba, tukijipanga vizuri kuboresha mbegu pamoja na kutoa huduma za ugani, tutaweza pia kufanya vizuri katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba ninukuu ukurasa wa 10 wa Mheshimiwa Rais, kama njia ya kuhitimisha na nitafafanua kwa nini nanukuu eneo hili kwa urefu kidogo.

Mheshimiwa Rais katika Hotuba yake, Ukurasa wa Kumi, anasema; "Hivyo basi, ni lazima viongozi wa Serikali kwa ngazi zote kuanzia Mawaziri hadi Maafisa Tarafa wawe karibu na wananchi, ili kuweza kufahamu changamoto zao na kuwajibika kwao. Kwa kuwa, ahadi tulizozitoa ni nyingi, matamanio ni mengi, matarajio ni makubwa na muda wa kuyatimiza haya ni mchache, tutaongeza kasi ya utekelezaji wa mipango ya Serikali, ili tuweze kufikia malengo tuliyojiwekea. Nayasema haya mapema kwa watendaji walioko Serikalini na wale nitakaowateua, kwa ajili ya kujitayarisha kisaikolojia na kujipanga vyema kufanikisha malengo hayo. Wananchi wanahitaji mabadiliko chanya kwa maendeleo. Watendaji msipobadilika kuendana na matarajio ya wananchi, tutawabadilikia." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi Bashiru ni nani kwenda kinyume na haya?

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni Waheshimiwa Wabunge tangu tulipoanza ahadi zilizoko kwenye ilani ni nyingi. Ahadi zilizoko hata kwenye dira na matarajio yetu ni makubwa, lakini muda ni mchache. Njia pekee ni kwenda kwa kasi kubwa na kuwajibishana kwa wale ambao hawawezi kumudu kasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana kwa kunisikiliza na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Bashiru. Sasa ninamwita Mheshimiwa Makonda, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Jiandae Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninaungana na Waheshimiwa Wabunge kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutupa uhai na kuturuzuku nafasi mbalimbali ambazo leo wengine tumezikalia kwa kudra na mapenzi yake. Sambamba na hilo niruhusu pia, nimshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mapenzi yake ya dhati ya kuruhusu tuingie kwenye mchakato na kupitia hatua ya kuteuliwa na chama chetu na hatimaye kupata nafasi ya kuwa Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama vile haitoshi, niruhusu pia, nimshukuru Dkt. Samia siyo kwamba, mimi ni bora kati ya wengi bali ni mapenzi ya Mungu na kudra zake kumpa macho ya rohoni kuniona na kunipa nafasi ya kuwa Waziri wa Habari, Michezo, Utamaduni na Sanaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza, niruhusu pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Arusha Mjini, wananchi hawa wamekuwa wakarimu, walinipokea kwa mara ya kwanza miaka 12 iliyopita, wakanipa mke mwema na hatimaye wakanipokea tena wakanipa ushirikiano na kuwa Mkuu wao wa Mkoa na haikutosha wakanipa nafasi ya kuwa Mbunge wao kuwawakilisha kwa miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Arusha wakiongozwa na viongozi wa dini, viongozi wa mila, viongozi wa taasisi mbalimbali, wakiwemo na vijana wenye taaluma mbalimbali ambao kwa namna ya kipekee hakika Arusha inafanya vizuri kwa sababu ya mapenzi na ushirikiano walionipa.

Mheshimiwa Spika, nisipowashukuru wana-CCM na Kamati Kuu kwa sababu mimi na CCM ni damudamu, kwa kunipa nafasi ya kipekee na kurudisha jina langu kupigiwa kura za ndiyo na Waheshimiwa Wabunge na kuwa Mjumbe wa *NEC* wa Chama Cha Mapinduzi kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nina kila sababu ya kuwashukuru sana wana-CCM wakiongozwa na Kamati Kuu pamoja na Wabunge waliopo hapa leo kwa mapenzi makubwa. Ahadi yangu kwenu Waheshimiwa Wabunge, nitaendelea kusimamia, kutetea na kuhakikisha kwamba hakuna haki ya Mbunge hata mmoja itakayopotea ndani ya Kikao cha Halmashauri Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunapochangia hotuba ya Dkt. Samia, Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunaitazama hotuba hii kama maono yanayoleta matumaini ya Taifa letu yakiibeba Tanzania ya leo na kutuonesha miaka mitano ya nchi yetu itakuwaje. Kwa kweli Dkt. Samia anastahili pongezi nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Wizara yetu ya Habari, Michezo na Utamaduni, ninaomba niongelee maeneo mawili tu. Moja, ninaongelea eneo la michezo. Dkt. Samia amewekeza kwenye miundombinu takribani Trilioni 1.267 kuhakikisha kwamba tunabadilisha mazingira na kuwatengenezea vijana mazingira mazuri zaidi ya kufanya michezo yao. Mfano, anakwenda kujenga uwanja wa Arusha ambao unaendelea kujengwa na umeshazidi zaidi ya 70%, takribani bilioni 338 zinatumika pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwanja wa hapa Arusha ambao tayari mkataba umeshasainiwa na mkandarasi ameshalipwa shilingi bilioni 55 wenye gharama takribani ya shilingi bilioni 366. Kama vile haitoshi, Dkt. Samia anajenga viwanja vya mazoezi kwa maana ya mashindano ya *AFCON* kuruhusu mataifa mengine kufanya mazoezi yao ndani ya nchi yetu, vyenye takribani thamani ya bilioni 51. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama vile haitoshi, anafanya ukarabati wa uwanja wetu wa Mkapa takribani bilioni 31, anafanya ukarabati wa uwanja wetu wa Uhuru takribani bilioni 19. Dkt.

Samia amedhamiria kubadilisha na kujenga miundombinu si tu kwa ajili ya kizazi chetu bali kizazi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatumia fursa hii kutoa rai, ninafahamu miradi hii inasimamiwa na iko chini ya Wizara yetu, Wakandarasi wote wanaosimamia na kujenga miradi hii, ninawaomba kwa unyenyekevu mkubwa wafanye kazi yenu kwa mujibu wa mkataba. Viwanja hivi tunavihitaji vikamilike kabla ya mashindano ya *AFCON*, viwanja hivi vitabeba sura ya Taifa letu kuliweka kwenye ramani ya dunia kwa namna ya jinsi ndoto ya Dkt. Samia alivyotaka. Sitakuwa na uwezo wa kumvumilia mtu yeyote yule atakayekuwa mzembe, atakayeshindwa kukamilisha miradi hii kama mikataba inavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu ya kwamba vijana katika nchi yetu wako wengi, kwa muda mrefu wamekuwa na ndoto kubwa si tu kwenye michezo, siyo kwenye filamu, siyo kwenye baiskeli, kwa maana ya riadha, kwa maana ya *Olympic* kila kijana ana ndoto yake, lakini kwenye Wizara yetu tumebaini ya kuwa vijana wengi pia wamekuwa na uwezo mkubwa wa kujipatia fedha kupitia mitandao ya kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mapenzi makubwa ya Dkt. Samia ndani ya siku zake 100 alisema ataweka mpango wa kuwawezesha vijana. Kwetu tayari ameshatoa shilingi bilioni mbili kwa ajili ya *content creators,* ambapo vijana hawa watazitumia kwa malengo mapana ya kujipatia pesa. Ninayo heshima mbele ya Bunge lako Tukufu kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge ya kwamba tayari leo tumetoa tangazo kama Wizara, kijana yeyote kokote aliko kule ndani ya Nchi ya Tanzania, mwenye kipaji chake, aliyekuwa anahangaika kutimiza ndoto yake kwa kutumia simu wakati mwingine hata haina uwezo, fedha za Dkt. Samia ameshazitoa, tunazo. Tunawataka waende kwenye Halmashauri kwa Maafisa Habari, wakajiandikishe, tuweke utaratibu wa kuwawezesha ili vijana hao wawe mabilionea kupitia taaluma yao.

Mheshimiwa Spika, nitatolea mfano mdogo tu, yupo kijana mmoja anaitwa Ndalo, yeye ni mchekeshaji, anatengeneza

*content* zake kupitia simu zake, ameweza kuajiri vijana 20 na yeye kwa mwezi anaingiza siyo chini ya shilingi milioni 17 kwa kazi hii anayofanya ya kutengeneza maudhui. Tumeona tuwashike mkono kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia kuhakikisha kwamba vijana hawa wanapata fursa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu kuwapongeza Taifa *Stars*, timu yetu ya Taifa imetupa heshima kubwa, tangu mashindano haya ya *AFCON* yaanze mwaka 1957 kama sijakosea, Tanzania tuliingia kwenye mashindano mara nne, mwaka 1980, mwaka 2019, 2023, kwa mara ya kwanza 2025, Nchini Morocco Tanzania ilivunja rekodi kwa kuingia katika 16 bora na kufuzu kwenye matamanio ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia fursa hii, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, tunatamani kuwa na mifumo ya kuandaa vijana katika umri mdogo walioko mashuleni wapate fursa ya kutumia nafasi ambayo Mungu amewapa ya vipaji vyao. Ushirikiano wenu Waheshimiwa Wabunge ni muhimu, kwa kuwa Dkt. Samia ameridhia kujenga shule 56 za mfano kwa ajili ya kuanza kuwatengeneza vijana watakaofanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia nafasi hii kuwaomba Wakuu wa Mikoa na nimemsikia vizuri Mheshimiwa Waziri hapa, maelekezo ya Rais na Waziri wetu Mkuu ameyatoa mara kwa mara, ninawaomba Wakuu wa Mikoa, kila Mkoa tuwe na timu ya Mkoa. Tunapokuwa na timu ya Mkoa, tunachechua na kuwatengenezea mazingira mazuri vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tunayo mashirika ya umma, tunayaomba pia mashirika haya yamiliki timu za mpira. Shirika kama la Reli likiwa na timu yake ya mpira litaongeza hamasa pia. Kama haitoshi, ninaomba sana tuhakikishe kwamba watu wanashiriki. Ninaona kengele imegonga, sijui kama ni mara ya pili, lakini ninahisi itakuwa ya mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kumalizia kwa maneno haya, Dkt. Samia, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni binadamu mwenye nyama, hakuna mtu mzima popote pale

duniani, anayependa kila mara kunyooshewa kidole wakati ana masikio. Tumwache Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania afanye kazi aliyoapa. Maneno matakatifu katika Kitabu cha Zaburi 122:6 - 8 "Utakieni Yerusalemu amani; na wafanikiwe wakupendao; amani na ikae ndani ya kuta zako na kufanikiwa ndani ya majumba yako. Kwa ajili ya ndugu zangu na rafiki zangu, niseme sasa, amani ikae nawe".

Mheshimiwa Spika, amani ndiyo msingi wa kila kitu, ninawaomba watu wote hawawezi kufanikiwa kwenye Taifa unalolilaani, hakuna laana inayoweza kubadilika kuwa mafanikio. Tuliombee amani Taifa letu, tulilinde Taifa letu na tuhakikishe ya kwamba tunamlinda Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba tena kusema ahsante kwa kunipa nafasi na ninawakaribisha wananchi wote na Wabunge kuja Arusha kwa sababu ukitaka kula maisha mazuri, njoo Arusha, ukitaka burudani njoo kwenye Wizara ya Michezo na Sanaa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Makonda kwa mchango mzuri, sasa ninamwita Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi, ajiandae Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, ajiandae mtoa hoja Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuungana na wote waliotangulia kusema kabla yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema. Pili, kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniona na kunipendekeza nami leo hii nipo katika jengo lako hili kama Mbunge, lakini pili kama Waziri katika ofisi ambayo umeitambulisha hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kipekee kwa sababu leo ninazungumza mara ya kwanza, ninaomba baada ya kumshukuru sana Rais kwa kuniona nami kuwa sehemu ya wasaidizi wake katika Baraza la Mawaziri, ninataka kupaza sauti pia kuwashukuru sana wananchi

wangu wa Jimbo la Chalinze. Kwa hakika wamekuwa nami siku zote, siyo rahisi sana katika umri wangu kuwa na vipindi vinne ndani ya Bunge lako, lakini leo ninaongea nikiwa na kipindi kizito cha nne na kwa kweli wanaendelea kuniunga mkono, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwanza kwa kutambua mchango mkubwa wa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kutekeleza majukumu yake. Wabunge wengi wamezungumza wakieleza kufurahishwa kwao na jinsi ambavyo tumeendelea kusimamia utumishi wa umma pia nafasi zilizotolewa kwa vijana wetu, vijana wamepata kazi.

Mheshimiwa Spika, ninataka kuungana na maneno mazuri aliyosema Waziri wa TAMISEMI kuwa ile kazi tuliyopewa ya kuajiri watumishi wa umma 12,000 tumeikamilisha. Ninataka kuwashukuru wote, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mwongozo wake, pia kwa kutusukuma mara kwa mara na kuhakikisha kwamba mambo haya yote yanawezekana.

Mheshimiwa Spika, ninataka kuwashukuru wenzangu ofisini maana kazi hii ina maelekezo ya Mheshimiwa Rais, siyo jambo dogo, lakini leo hii ninaposimama mbele yako, ninayo furaha ya kusema kwamba kazi imekamilika na kwamba sasa tunaenda kutekeleza mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo pia, yako maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais aliyatoa, haya ni maelekezo ya nia nzuri ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba vijana wake wa Kitanzania wanaendelea kula neema ya nchi yao. Mheshimiwa Rais alielekeza katika wale vijana watakaokuwa wamepata ajira katika zile nafasi 12,000 basi wale watakaowahi kuingia kazini kabla mwezi Januari haujaisha, waingizwe kwenye *payroll* ya Serikali na wapate mshahara.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa taarifa mbele ya Bunge lako kwamba watumishi 735 wa kwanza waliofanikiwa kuripoti

katika vituo vyao mapema, wote waliingizwa kwenye *payroll* ya Serikali na wamekula mshahara wa mwezi Januari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko jambo ambalo ninataka kulieleza vizuri na ninaomba Bunge lako Tukufu na wananchi wanaotufuatilia kwenye televisheni na vyombo vingine vya habari waniazime masikio yao vizuri. Kumetokea vitu viwili, moja wako watu ambao wamekuwa wanahangaika sana na kufanya mabadiliko ya vituo, malalamiko ni mengi na wengine wanawatumia hata baadhi ya viongozi humu ndani na wengine wanawatumia wazazi wao wanaotufahamu ili tuwabadilishie vituo.

Mheshimiwa Spika, ninataka kusema mbele ya *mic* hii, maelekezo tuliyopewa na ndiyo mtazamo wa Serikali na ndiyo maelekezo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu pia naye ametuelekeza, hakutokuwa na mabadiliko ya vituo vya kazi sehemu yoyote. Kila mtu aende kwenye kituo alichopangiwa kazi. Tanzania ni yetu sote, hakuna mtu mwenye haki ya kukaa mjini, hakuna mtu ambaye hana haki ya kukaa mjini anatakiwa kukaa vijijini. Wote tunatakiwa kwenda kufanya kazi ya kuwatetea Watanzania na kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ninataka kusema katika *mic* hii kwamba maelekezo yaliyotolewa na viongozi nasi pia tunaendelea kuyasimamia, hakutakuwa na mabadiliko ya kituo chochote cha kazi. Kwa hiyo, kama umepangiwa kule Kigoma kwa Wajomba zangu, ninakuomba funga safari, nenda Kigoma ukafanye kazi. Kama wewe umebahatika kupangiwa Dodoma, ninakuomba funga safari njoo Dodoma tufanye kazi. Hakuna upendeleo katika hili na jambo hili liko wazi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Mheshimiwa Rais alituelekeza kufanya mapitio ya mfumo wetu wa mawasiliano Serikalini ambao unawakutanisha viongozi na wananchi wetu, hapa ninakusudia kuzungumzia mfumo wa *e-mrejesho*. Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Utumishi ilifanya kazi yake, tulipitia mfumo huu na kupitia mfumo huu tuliongeza dirisha dogo, dirisha linaloitwa “sema na kiongozi” ambalo linawezesha wale viongozi waliotajwa

katika maelekezo yaliyotolewa, waweze kuzungumza na wananchi moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, hapa ninakusudia kuzungumzia katika ngazi ya Wizara, Mawaziri na Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, ninataka niwaseme hapa kwa majina ili wafahamike vizuri. Katika ngazi ya Sekretarieti za Mikoa, Wakuu wa Mikoa na *RAS,* lakini Wilayani ninazungumzia Wakurugenzi, ninazungumzia Wakuu wa Wilaya na ninazungumzia pia Makatibu Tawala wa Wilaya zetu. Pamoja na wao, pia Wakurugenzi wa zile taasisi ambazo zinatoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, makundi haya ambayo nimeyataja matatu, yote yanatakiwa yaungwe katika mfumo huu wa *e-mrejesho*, dirisha la "sema na kiongozi". Makusudi makubwa ni yale maelekezo aliyotoa Mheshimiwa Rais ya kwamba anataka Serikali yake, viongozi wazungumze na wananchi moja kwa moja, katika kufanya hivyo, Serikali imekwishakamilisha ujenzi wa mfumo huu na sasa tuko katika hatua ya kuwafundisha. Jambo lililo zuri kuliko yote na ndiyo maana nikasema mwanzo niwataje kwa majina na wanisikilize kwamba, mfumo huu umeunganishwa moja kwa moja na *dashboard* ya Rais. Kwa hiyo, kama kuna Waziri, kama kuna Wakuu wa Mikoa, kama kuna watendaji ambao wameunganishwa na mfumo huu, hawatofanya kazi, jambo la *PDF* litawahusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema haya kwa sababu ni maelekezo ambayo tumepewa na Mheshimiwa Rais nasi kupitia Ofisi ya Rais, Utumishi tunachofanya ni kusimamia utaratibu. Pia kama mnavyofahamu, kiranja wetu Mheshimiwa Waziri Mkuu, naye pia ataunganishwa na dirisha hilo ili aweze kusimamia vizuri utumishi wa umma katika Serikali yake. Kwa hiyo, ninaomba tu kusema kwamba kama Wizara inayosimamia utumishi na utawala bora, tulipewa maelekezo mahsusi katika maeneo makubwa mawili na kwa hakika tunayatekeleza kama ambavyo tumeelekezwa.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili la pili, ninaomba tu kuwaomba sana viongozi wenzangu hususan Mawaziri, Naibu Mawaziri pia Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na wengine wote ambao wanahusika na eneo hili, eneo la *e-mrejesho* ni jambo la muhimu. Wananchi wetu wanayo malalamiko yao, upo wakati huwezi kukutana nao mmojammoja, lakini kupitia mfumo huu, upo utaratibu ambao umetengenezwa na watapitishwa wote ili waweze kufanya kazi ambayo Rais aliwaahidi Watanzania nasi kama Wasaidizi wake twende kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, kwa sababu muda wenyewe bado dakika mbili tatu hapa ninaziona, Wizara imefanya kazi kubwa sana, yapo mambo mengi mazuri yamefanyika, ninaomba kutumia nafasi hii ndogo kutoa mrejesho katika baadhi ya mambo mawili ambayo hayakuwemo katika ahadi ya siku 100, lakini ni utaratibu wa Serikali kuendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, moja, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan hivi karibuni ametoa kibali kipya cha ajira ambapo vijana 41,500 watakwenda kuajiriwa katika kada mbalimbali zikiwemo tena kada ya afya, kada ya elimu, kada ya kilimo, kada ya uvuvi, kada ya uhandisi, kada ya zimamoto, Jeshi la Uhamiaj, Jeshi la Polisi na watumishi katika maeneo mengineyo. Ndugu zangu Watanzania Mungu atupe nini, huyu ni Rais Samia Suluhu Hassan, Rais ambaye siku zote watu wanaota katika Tanzania kuwa naye siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana ametoa ajira 12,000, leo anaidhinisha kibali cha ajira 41,500, kwa hakika huyu ni Rais anayewapenda vijana wa Kitanzania. Vijana ambao kwa muda mrefu sana wamekuwa wanalalamika juu ya ajira. Siyo hilo tu, pia kupitia sekta zisizo rasmi, Rais ameelekeza pia tuendelee kuwaangalia kwa kuhakikisha kwamba usimamizi wa miundombinu inayowawezesha vijana inafikishwa mpaka kule chini kwa kuhakikisha kwamba katika bajeti inayokuja, yako mambo ya msingi tunayoenda kuyaangalia mojawapo ni zile kodi ambazo zinaendelea kuwaonea vijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, ninataka kukuhakikishia, Wizara ya Utumishi na Utawala Bora tutaendelea kufanya wajibu wetu, pia ninataka kulihakikishia Bunge lako na Wabunge wako kwamba, tutaendelea kufanya kazi ambayo tumetumwa na Watanzania kupitia maono ya Rais ili tuweze kufanya lile jambo ambalo Rais alilieleza wakati anatuhutubia, anataka nchi siyo ya vitu, lakini nchi ambayo imejaa furaha kwa watu wake.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, pia hivi karibuni, Serikali iliidhinisha shilingi bilioni 4.27 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 78 za watumishi wanaoishi katika mikoa iliyo pembezoni mwa nchi yetu. Ninapozungumzia pembezoni maana yake ninazungumzia ile mikoa ambayo nimetoka kuzungumza dakika mbili zilizopita ambayo vijana wanasema hawawezi kwenda kwa sababu wanaona kwa mazingira yake si mazuri. Visingizio vya watu kutokwenda huko Mheshimiwa Rais anataka kwenda kuvimaliza sasa.

Mheshimiwa Spika, katika *phase* ya kwanza ya utekelezaji wa ujenzi wa nyumba huko wilayani Mheshimiwa Rais alielekeza nyumba 54 zijengwe na sasa nyumba 78 zinaenda kujengwa. Tunatambua kwamba bado mahitaji makubwa; katika bajeti inayokuja tutaleta maombi mbele ya Bunge lako litukubalie kuongeza nyumba ili watumishi wetu waweze kukaa sehemu nzuri, wafanye kazi ya kuhudumia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge sasa ninamwita Mheshimiwa Juma Hamidu Aweso Waziri wa Maji, ajiandae Mheshimiwa Waziri Mkuu, mtoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, moyo usiokuwa na shukrani hukausha mema yote. Nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu na kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kunipendekeza kupitia Chama chetu Chama Cha Mapinduzi kuwa mgombea katika Jimbo la

Pangani na kuniamini kuwa Waziri wa Maji kwa mara nyingine katika Wizara yetu ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kuwa mimi Juma Aweso ambaye nimepewa dhamana katika Wizara hii ya Maji sitokuwa kikwazo kwa Waheshimiwa Wabunge wa Tanzania kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza. Kwa namna ya kipekee niwashukuru wananchi wa Pangani kwa kunichagua kuwa Mbunge. Ninataka niwaambie ndugu zangu wa Pangani, kwamba sina Marekani nyingine, Marekani yangu ni Pangani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nimpongeze na nimshukuru pia Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais. Vilevile kwa namna ya kipekee ninaomba niseme dhati ya moyo, unapopewa dhamana na kiongozi wako mkuu unatakiwa ufanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ameaminiwa kuwa Waziri Mkuu. Ninataka niseme, anafanya kazi. Ameaminiwa kwa muda mfupi sana tunamwona katika kila pande za Tanzania akifuatilia maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi katika Wizara yetu ya Maji ameshakuja mara tano. Amekuja Dar es Salaam ambapo kulikuwa na *crisis* ya maji. Mheshimiwa Rais amemtuma, amemwelekeza kuwa pamoja na sisi. Amekwenda kule Lindi ambako tuna mradi wa zaidi ya bilioni mia moja, kuweka jiwe la msingi.

Mheshimiwa Spika, amekuja pia katika Wizara yetu ya Maji, ameenda Mwanza ambako tumezindua na tumeweka jiwe la msingi kwa ajili ya Jiji la Mwanza waweze kupata maji kwa maana Wanaluchelele, Wanabuhongwa na maeneo ya Kishiri na maeneo mengi ya Jiji la Mwanza waweze kupata huduma ya maji safi. Ninataka niseme, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kielelezo chema na anamsaidia kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wa Kamati kwa namna ya muda mfupi ambavyo

mnatuongoza, sina mashaka kwamba Bunge hili litaleta mageuzi makubwa kwa maono ambayo ameweka Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi kujua unapokwenda kama hujui ulipotoka. Ni lazima Waheshimiwa Wabunge tufanye tathmini, sisi wote ni Watanzania. Ni lazima tujue ni wapi tulipotoka, ni wapi tulipo na ni wapi tunapokwenda. Ninachotaka kusema kama kijana wa Kitanzania Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametutoa mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa *Chief Whip* wetu hapa Mheshimiwa Lukuvi wao ni Wabunge wa muda mrefu. Wizara ya Maji miaka ya nyuma ilikuwa Wizara ya kero na lawama. Fedha nyingi zilikuwa zikiwekezwa, lakini matokeo hakuna. Nitawapa mfano; tuliwahi kwenda gari jembe, zilipelekwa pale zaidi ya milioni 500. Unafika kiongozi unauliza mradi uko wapi, mradi haupo fedha zimeliwa. Viongozi walikuwa wakienda kutagua miradi ya maji unazindua mradi wa maji, mradi unatoa maji kiongozi ukiwepo ukiondoka maji hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyopewa dhamana ya kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Taifa hili alitoa maelekezo mahususi katika Wizara yetu ya Maji. Alisema ya kwamba yeye ni mama na asilimia kubwa ya wanaoteseka juu ya adha ya maji ni akinamama; hivyo hataki kusikia, hataki kuona akinamama wa nchi hii wanateseka juu ya adha ya maji. Akaenda mbali akanisimamisha mimi Waziri wa Maji akaniambia ukinizingua tutazinguana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka niwaambie, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kipindi tu cha miaka minne amefanya mageuzi makubwa ndani ya sekta ya maji. Amefanya *reforms* nyingi sana. Wahandisi amewapandisha, ameanzisha Wakala wa Maji Vijijini *(RUWASA);* huko ndiko kulikokuwa na changamoto. Tulikuwa na ufinyu wa bajeti miaka ya nyuma, tulikuwa tukipata milioni 300, 400 na wakati mwingine hazitoki. Amebadili bajeti ya Wizara ya Maji zaidi ya bilioni 894 alitupatia sisi Wizara ya Maji.

Alitambua kabisa pasipokuwa na fedha hatuwezi kufanya miujiza ili Watanzania wapate huduma ya maji safi. Akaasisi falsafa ya kumtua mwanamama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka niwaambie ndugu zangu, nchi yetu ya Tanzania ina vijiji 12,333 kupitia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na uanzishwaji wa Wakala wa Maji Vijijini kwa muda wa kipindi hiki cha miaka minne tumefika vijiji 10,758 huyu ndio Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muda wake tu wa miaka minne amejenga miradi zaidi ya 6,000 katika vijiji 7,929 pekee amevifanya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tulikuwa na *program* inaitwa *P4R*, tumeshindanishwa na *world bank* zaidi ya nchi 50; Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa Waziri wa Fedha tuliitwa pale Ethiopia, nchi ambayo inaongoza kwa miaka miwili mfululizo ni Nchi ya Tanzania chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tumepata tuzo nyingi kutoka nchi mbalimbali kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi ambao wamefanya kazi kwa muda mrefu. Yapo maazimio ambayo yaliamuliwa na Bunge zaidi ya miaka 60 hayajawahi kutekelezwa. Bwawa la Farkwa miaka ya 70 lilitakiwa litekelezwe Bwawa la Farkwa lakini halijatekelezwa. Bwawa la Kidunda kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji Dar es Salaam na Morogoro yake halijawahi kutekelezwa tangu miaka 60; Dkt. Samia Suluhu Hassan yeye ndiye anatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Bwawa la Farkwa ambalo lilitakiwa kujengwa kwa miaka ya nyuma mabwawa au kazi kubwa au miradi mikubwa ya kimkakati ilikuwa ikijengwa kwa fedha za ufadhili Dkt. Samia Suluhu Hassan anajenga kwa fedha zake za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuja kulikagua lile bwawa; nawe ukimaliza na muda ukikuruhusu tunakuomba ukaone kazi kubwa na nzuri iliyofanywa katika

Bwawa la Kidunda. Bwawa lile linagharimu zaidi ya bilioni 329 mradi upo wa zaidi ya 40%. Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja, hivi karibuni mkandarasi alikuwa anadai zaidi ya bilioni 24. Ninataka nimpe taarifa, kwa maelekezo aliyoyatoa bilioni 24 zote zimekwishatolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka niwaambie tupo katika uelekeo sahihi. Mheshimiwa Rais amehutubia katika Bunge hili, ametupa dira ya uelekeo wa Serikali yake. Ninataka niwaambie, kwamba ameweka malengo makubwa na tunakwenda katika maendeleo makubwa. Ili tuweze kuyafikia malengo makubwa ninataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge na Watanzania tusilale usingizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kuwa na Rais aina ya Dkt. Samia Suluhu Hassan hapatikani kila wakati, kuwa na Rais aina ya Dkt. Samia Suluhu Hassan hatuwezi kumpata kila mahali. Tumempata, hivyo ni lazima tumtumie kwa maslahi ya Watanzania. Maandiko yanasema shika sana ulichonacho asije mtu akatwaa taji lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusimame imara, hatuna nchi nyingine, nchi yetu ni Tanzania; hatuna Rais mwingine, Rais wetu ni Dkt. Samia Suluhu Hassan. Amefanya makubwa. Kazi ambazo amezifanya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan si za kutumia tochi, zinaonekana kwa macho. Leo anatupa maelezo makubwa katika Wizara yetu ya Maji. Anasema nchi yetu ya Tanzania si maskini wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, ukienda Katavi, Rukwa na Kigoma kuna Ziwa Tanganyika; ukienda Mwanza, Geita, Mara hadi Bukoba tuna Ziwa Victoria. Ukienda Ruvuma tuna Ziwa Nyasa; maeneo ya Mtwara tuna Mto Ruvuma; ukienda zako Mkoa wa Pwani tuna Mto Rufiji; ukienda Kigoma tuna Mto Malagarasi; ukienda Kaskazini tuna Mto Pangani. Kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan vyanzo vile vikatumike kutatua matatizo ya maji. Haya ndiyo maelekezo ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, ninataka niwaambie, kwamba ndani ya siku 100 ambazo ametupa maelekezo hayo safari ya kuyatoa maji ya Ziwa Victoria kuja katika Jiji la Dodoma *feasibility study* tumekwishaikamilisha. Maelekezo ambayo ametupa, ya kuhakikisha maji ya kutoka Ziwa Tanganyika yaende katika Mikoa ya Katavi, Rukwa mpaka Kigoma, Mhandisi Mshauri tumeshampata. Wanataka Dkt. Samia Suluhu Hassan afanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka niwaambie, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Rais wa kusema na kutenda. Tunapozungumzia kuhusu *National Grid* haina maana kwamba ndiyo tunataka tufanye, tumekwishaanza. Tunapozungumza Wizara ya Uchukuzi ina *SGR* kutoka zake Dar es Salaam kuja Dodoma, Wizara ya Maji ina *SGR* ya maji kutoka Jiji la Mwanza mpaka kuja katika Mkoa wa Tabora, maji yamekwishafika Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tumepewa kazi nyingine ya kuyatoa maji Ziwa Victoria pale Tabora kuja hapa Dodoma. Kama ameweza kuyatoa maji Ziwa Victoria kufika Tabora atashindwa kufika hapa Dodoma? Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan apewe heshima yake. Piga makofi mengi sana kwa Rais Daktari Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ukienda Simiyu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri pamoja na hoja zako unazungumza vizuri, ninakuongezea dakika mbili. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, leo ukienda katika Mkoa wa Simiyu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anatekeleza *National Grid* ya zaidi ya bilioni 440. Ukienda Mkoa wa Mara amekwishatekeleza Mradi wa pale Mugango - Kiabakari, zaidi ya bilioni 71, mradi umekamilika. Ukienda kwa dada yangu Esther Matiko na Jimbo la Rorya anajenga mradi wa bilioni 130 kwa fedha za ndani. Ukienda Tunduma Mheshimiwa

Rais anajenga mradi wa zaidi ya bilioni 100 kwa fedha za ndani; anayatoa maji Mto Momba anapeleka Tunduma, anapeleka Vwawa. Ukienda pale Mkoa wa Mbeya ana mradi wa zaidi ya bilioni 119 kuyatoa maji ya Mto Kiwira kazi amekwishaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda zako Mbarali pale Rujewa tuna Mradi wa kuyatoa maji Mto Mbarali tunayapeleka Rujewa, yanakwenda Wanging'ombe, yanakwenda mpaka Makambako. Huyo ndiye Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda Kaskazini kuna mradi wa zaidi ya miaka 20 ambao ulishindikana, Mradi wa Same – Mwanga. Mradi ule, fupa lile ambalo lilikuwa gumu yeye ameligeuza *biscuit*. Maji yanatoka Same – Mwanga yanaenda Korogwe. Pale Korogwe sasa hivi ameshaanzisha mradi mkubwa wa zaidi ya bilioni 70; anayatoa maji ya Mto Pangani yanakwenda Korogwe, Muheza, Handeni, Pangani mpaka yafike Chalinze katika Jimbo la Mheshimiwa Ridhiwani. Huyo ndiye Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninataka niwaambie; tusigombanishwe, tusifitinishwe na Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sina mengi sana ninaomba niunge mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Waheshimiwa nilikuwa ninamwona Mheshimiwa Ado anapiga makofi kimoyomoyo. Waheshimiwa sasa ninamwita mtoa hoja. Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu hoja kuhusu kujadili Hotuba ya Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa tarehe 14 Novemba, 2025 wakati wa kulifungua Bunge la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mungu kwamba asilimia kubwa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia na Waheshimiwa Wabunge ambao wapo hapa Bungeni ni

Wabunge ambao walikuwepo wakati Mheshimiwa Rais akihutubia Bunge lako Tukufu. Kwa maana hiyo walipata fursa ya kumsikia moja kwa moja Mheshimiwa Rais akiainisha masuala mbalimbali kuhusu mipango na mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi kingine cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ametoa nyenzo ya kufanyia kazi kwetu sisi sote wasaidizi wake na ametoa dira ya utekelezaji wa dira ya maendeleo ambayo sote tulishuhudia ikizinduliwa. Sote ni mashihidi kwamba wakati akielezea vipaumbele anavyotaka vitekelezwe katika kipindi cha miaka mitano ijayo Mheshimiwa Rais aliweka bayana kuwa mambo yote muhimu yatakayotekelezwa yamebebwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2025, na mipango ya maendeleo ambayo itaendelea kuwasilishwa mwaka kwa mwaka na ile ya miaka mitano mitano.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe Mheshimiwa Rais alisema kwamba atahakikisha anatekeleza masuala baadhi ambayo aliyatoa wakati wa kampeni yatekelezwe ndani ya siku 100 tangu alipochaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, baada ya Hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa tarehe hiyo utekelezaji wa maelekezo yake ulianza mara moja kwenye maeneo mbalimbali, zikiwemo ahadi za siku 100 kama ambavyo Mheshimiwa Spika; umetoka kushuhudia Waheshimiwa Wabunge wakikiri utekelezaji wake na wananchi katika maeneo yetu wameshuhudia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, hii ni kutokana na ukweli kwamba Wizara na taasisi zote za Serikali zilichukua hatua za makusudi kuchambua hotuba hiyo na kuainisha maeneo mbalimbali ya utekelezaji sambamba na kuandaa mipango ya utekelezaji wa muda mfupi, wa muda wa kati na ule wa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais zimetekelezwa kwa mafanikio makubwa sana kupitia sera,

mipango na mikakati ya kitaifa chini ya kauli mbiu ya kazi na utu tunasonga mbele, ikiwemo katika maeneo ambayo baadhi tumetoka kusikia. Kwa mfano, kwa upande wa sekta ya afya Serikali imeanza kutoa bima ya afya kwa wote kwa makundi machache ya wazee, watoto na wajawazito. Vilevile tumeanza kugharamia magonjwa sugu; yaani saratani, figo, moyo, kisukari na mifupa kwa watu wasio na uwezo. Hii ni tafsiri ya utu.

Mheshimiwa Spika, kuondoa pia zuio la kuchukua miili ya marehemu katika vituo vya umma vya afya ambavyo vinatoa huduma zote za afya kote nchini kwa kigezo cha kutokulipa gharama za matibabu ama madeni. Hii nayo ni moja ya ile tafsiri ya utu katika kauli mbiu ambayo inajenga uelekeo wa utekelezaji wa majukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeajiri watumishi wa Sekta ya Afya kama ambavyo tumetoka kuambiwa 5,000 na inaboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Nisisitize kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Sekta ametoka kusema, kila aliyepangiwa kituo na ameshapokea barua ya kupangiwa kituo aripoti kwenye kituo chake. Kama hataki, hapendi kwenda katika eneo alilopangiwa aandike barua ya kukataa ajira aliyopewa ili Watanzania wengine wachukue nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Elimu, Serikali imeendelea kukuza na imeendelea kutekeleza mipango mikakati ya kisayansi ya kujenga umahiri wa kusoma, kuandika na kuhesabu, wenye kauli mbiu ya 'Mtoto Asome, Aandike na Ahesabu Bila Shida'; unaolenga kuongeza ubora wa elimu ya msingi na mbinu bora za kufundishia na kuandaa mpango wa pamoja kati ya mwajiri, vyuo vya ufundi stadi, pamoja na vyuo vikuu, unaolenga kuwajengea uwezo wa ubunifu na ujasiriamali wanafunzi ili kuwezesha kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumetoa taarifa kwenye upande wa afya, tayari kwenye upande wa elimu Walimu 7,000 wamekwishaajiriwa na hii ni kukabiliana na upungufu hasa hasa wa Walimu wa Sayansi katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Kazi nyingine zinaendelea zikiwemo programu ya maandalizi ya utekelezaji wa programu ya mitaala mipya na yamebainishwa

katika maeneo mbalimbali na tutaendelea kupewa taarifa na Mawaziri wa Kisekta katika taarifa za utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais za ndani ya siku 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya maji kama ambavyo tumetoka kuelezewa kwa kirefu, kazi kubwa imeendelea kufanyika na niwatoe hofu Watanzania. Popote pale ambapo bado kazi haijafanyika wajue tutawafikia. Vimebaki vijiji takribani 1,500. Mpango unaopangwa ni wa kutekeleza *programs* mbalimbali za upatikanaji wa maji ili kuweza kuhakikisha kwamba vijiji vyote hivyo vinapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafirishaji kazi kubwa imefanyika. Kama ambavyo wengi tumeshuhudia meli kubwa mpya ya *New MV Mwanza* inayotoa huduma za usafiri wa abiria na mizigo katika Ziwa Victoria imezinduliwa rasmi. Kukamilisha ujenzi wa jengo la viongozi na lenyewe ni moja ya jambo ambalo limefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipokwenda kuzindua meli ile ya Mwanza kazi ambayo Mheshimiwa Rais alinituma, nilienda kushuhudia meli kubwa ambayo ni ya tofauti, ni ya aina yake ambayo ingeweza kufanya kazi baharini, lakini iko katika Ziwa Victoria na imeanza kazi ya kutoa huduma katika Ziwa Victoria kwa wananchi wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Hii ni hatua kubwa ambayo imefanyika na inaonesha wazi kwamba nchi haijasimama inasonga mbele. Nchi inasonga mbele na kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika katika upande wa usafirishaji, kama ambavyo Naibu Waziri alitoa taarifa hivi karibuni, Shirika la Ndege la *ATCL* limeanzisha *route* mpya ambayo sasa kutoka Dar es Salaam tutakwenda mpaka Accra Ghana. *Route* hiyo imezinduliwa tarehe 28/1/2026 na hivyo kufikia vituo 17 vya Kimataifa. Hii ni hatua kubwa kwa nchi yetu na tunaendelea kutangaza kwamba nchi yetu haijasimama, inaendelea kusonga mbele. Katika miaka chini ya 10 tulikuwa na ndege moja, sasa tumeenda kufika kwenye vituo 17 tukiwa na ndege takribani 16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mazingira wezeshi kwa wajasiriamali na vijana kujiajiri kwa kuongeza wigo wa upatikanaji wa mitaji kwa Mheshimiwa Rais kutoa shilingi bilioni 200 zitakazowezesha vijana wajasiriamali wanaofanya shughuli mbalimbali nchini kuzingatia na kuingia katika kutekeleza majukumu yao huku wakiwa wanapata fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni machache tu. Waheshimiwa Mawaziri wataendelea kutoa taarifa hizo kama ambavyo wamekwishatoa katika baadhi ya sekta kuhusu utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais alizozitoa zinazohusisha siku 100 na utekelezaji wake ukiwa unaendelea.

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana nitoe taarifa hii kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba, taarifa zote ambazo zinatolewa na Waheshimiwa Mawaziri zitapelekwa kwa Katibu wa Bunge ili waweze kuwekewa kwenye vishikwambi vyao ili waweze kujua kile ambacho Serikali imekwisha kutekeleza na yale ambayo Serikali inatarajia kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa shughuli hizi zote, kama nilivyotangulia kusema pale mwazo, upo kwenye Ilani ya uchaguzi ya CCM, lakini pia upo kwenye utekelezaji wa dira mpya ambayo utekelezaji wake ndiyo unaenda kuanza na mipango ya miaka mitano mitano, pamoja na mpango wa mwaka mmoja mmoja utawasilishwa na Waziri wa Sekta na mjadala wake ni kama ambavyo umetoa mwongozo.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie Watanzania, Serikali imejipanga kutekeleza yale yote ambayo Mheshimiwa Rais aliyasema na leo hii kwenye mjadala ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoa, wametuongezea sisi Serikali nyenzo ya kutekeleza yale ambayo Mheshimiwa Rais ameyaonyesha kama dira ya uelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipindi chake cha pili.

Mheshimiwa Spika, wala tusitolewe kwenye uelekeo na wale wasioitakia mema nchi yetu. Wapo watu ambao hawajashiriki

wala kufuatilia utengenezaji wa Dira yetu ya Taifa. Niwataarifu kwamba Dira yetu ya Taifa kwa mara ya kwanza imetengenezwa kwa kukusanya maoni ya Watanzania kote mpaka mikoani. Kwa hiyo, ni dira yao ambayo wameiandika wakitaka kuonyesha ni wapi wanataka nchi yetu iende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi upande wa Serikalini tumejizatiti katika kutekeleza. Niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Watanzania kwamba, dira hiyo itaenda kutekelezwa na Ilani na utekelezaji utatumia fedha zetu na kama tulivyoona katika siku za hivi karibuni makusanyo yameongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi kwenye ripoti ya Mamlaka ya Mapato walionesha rekodi mpya ambayo haikuwahi kufikiwa ya makusanyo katika kipindi cha miezi mitatu iliyokuwa imepita kuanzia Oktoba kwenda Disemba. Zaidi ya shilingi trilioni 9.8. Muda mfupi Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ametuambia taarifa ya makusanyo kuhusu makusanyo ya Serikali zetu za Mitaa; na yenyewe ikiwa rekodi mpya zaidi ya shilingi trilioni 1.2, na malengo ikiwa ni kuboresha kwenda hadi trilioni mbili. Kwa hiyo, miradi itakwenda kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu, tulipotunga dira tumebainisha mle ushiriki wa Serikali na Sekta Binafsi. Tunapokwenda kwenye utekelezaji, wale ambao hawakushiriki kwenye uandishi wa dira watumie muda kusoma kile kilichoainishwa kwenye Dira yetu ya Taifa. Tutashirikisha Serikali pamoja na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanyia kazi, tutaleta mapendekezo ya kuangalia upya Sheria yetu ya Manunuzi pamoja na Sheria ya *PPP*, ya ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi. Yote hiyo ikiwa inalenga kuongeza nguvu kwenye nchi yetu ya utekelezaji wa miradi. Tuna miradi ambayo imebainishwa kama ambavyo nimetoka kusema. Imebainishwa na Ilani yetu ya Uchaguzi na mingine kwenye mipango yetu ya maendeleo. Kwa hiyo, tutakwenda kuitekeleza ili Watanzania waweze kupata

manufaa na utekelezaji huo wa miradi uweze kuwapa manufaa makubwa. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, nimeona niiseme hii kufuatia baadhi ya kauli ambazo niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wamechangia vizuri, habari zilizokuwa zinasemasema dhahabu, dhahabu. Tunapotaja akiba zetu tulizonazo sasa hivi, tunataja akiba ya fedha ambazo kwenye hizo akiba za fedha tunaongelea kiwango cha chini zaidi ya miezi minne ya uagizaji wa bidhaa. Ambapo sasa ninadhani tuna zaidi ya miezi 5.7 ya uagizaji wa bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, katika uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tuliongeza wigo wa kutaja akiba tulizonazo. Sasa hivi tunataja pia akiba ya chakula tulichonacho. Kiwango cha chini ambacho kinatakiwa kutosheleza akiba ni tani takribani 150,000, lakini Serikali ina akiba ya chakula takribani tani 450,000. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, maana yake nini? Panapotokea pana uhitaji Serikali inaweza kuuza ile ziada ambayo ni ziada ya kile kiwango cha lazima cha kubakiza kwenye akiba ya nchi. Inaweza ikauza ili iweze kusaidia maeneo ambayo wananchi wanahitaji kupunguza makali ya mahitaji ya chakula. Lakini sehemu nyingine Serikali inaweza ikauza akiba ya hicho chakula ili ipate fedha za kununua chakula kingine, ili wakulima wasibaki na chakula katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, itakuwa inauza si kwa sababu inatafuta fedha hizo ili ipeleke kwenye bajeti, itakuwa inauza kwa sababu Wakala wa Chakula aweze kujiandaa kununua chakula kwa wakulima kama sehemu ya kuwafanya wakulima wapate chakula, wapate fedha, wapate faida ya mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, hivyo hivyo na kwenye dhahabu; dhahabu inasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania. Hawa wanaoongelea dhahabu sasa hivi na hawajajua hata fedha ya kununua dhahabu ilitoka wapi, mpango ulianzia wapi, wao wanaenda kwenye tetesi tu dhahabu, dhahabu! Benki Kuu kama

msimamizi wa sera kuna wakati akitaka mfumuko wa bei uwe chini, kwenye fedha tu, achilia mbali dhahabu, wanatumia *Liquidity Papers* zake za kupunguza fedha kwenye mzunguko ndani ya nchi. Ni sera za kifedha za Benki Kuu ambazo huwa zinatumika na nchi yoyote.

Mheshimwa Spika, katika muda ambapo wanataka fedha ziende nyingi kwenye mzunguko wanatumia pia sera hizo hizo za kifedha ambazo zinaruhusu fedha ziende nyingi kwenye mzunguko wa fedha. Sasa, leo hii Benki Kuu imesababisha wachimbaji wadogo wengi wanufaike sana kwa ajili ya ununuzi ule wa dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, kama nchi, mpango ule ambao dira yake imetolewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunataka tuendelee na jambo hili la kununua dhahabu, hata iwe nyingi na nyingi na nyingi, mpaka tulingane na Mataifa mengine ambayo yalishanunua dhahabu nyingi. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, inapotokea soko la dunia limepanda, ni busara tu kuuza ili ununue dhahabu za wachimbaji wadogo huku wapate soko, wapate fedha nyingi, ni busara tu. Maadam kiwango cha chini kilichowekwa cha dhahabu inayotakiwa kuwepo kipo vilevile. Ni jambo la kawaida tu na haya wala si mambo ya mtaani ni mambo ya kisera, Benki Kuu watafanya. Kama ambavyo mambo mengine ya kifedha huwa yanafanyika, hivyo hivyo ndivyo inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, haya ya utekelezaji wa miradi tusije tukatumia, tukatembea na kauli za wale wasioitakia mema nchi yetu. Wao wanadhani kwamba nchi haina fedha inataka iuze dhahabu ndiyo iweze kutekeleza miradi. Makusanyo tunayapata kila siku, lakini pia na fedha zikishapatikana, kwani zile za dhahabu zitakuwa zinawekewa alama? Zenyewe zitakuwa zinawekewa alama? Wanataka zile za dhahabu zikiuzwa zifungwe shanga kwamba hizi ni za dhahabu? *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, ninadhani tuache kudandia hoja ambazo hatujui zimeanzia wapi na zimeenda wapi. Ninawahakikishia

Watanzania, duniani kote, moja ya taasisi zinazoongozwa na misingi ni Benki Kuu. Watu wasitoetoe taharuki kwenye taasisi ambazo zina heshima na uendeshaji wake una heshima na popote pale ambapo taasisi hizi zinaendeshwa kwa heshima zinazingatia misingi. Kama zinazingatia hiyo misingi, wale ambao hawana taarifa sahihi wasiingilie misingi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, niliona niliseme hili kwa sababu nimeona linaletaleta taharuki. Tusitumie taharuki, tusitengeneze taharuki, hizi ni taasisi zinazoendeshwa kwa heshima na Serikali haijakosa fedha za kutekeleza miradi na Serikali pia ina njia nyingi za kutekeleza miradi. Ikitokea Serikali inataka kutekeleza miradi kutumia rasilimali zetu ikiwemo dhahabu na wenyewe utakuwa uamuzi wa nchi yetu. Ikitokea Serikali inataka kutekeleza miradi kwa kutumia mahindi na wenyewe ule utakuwa uamuzi wetu. Ikitokea Serikali inataka kutekeleza miradi kwa kutumia makaa ya mawe, hiyo na yenyewe utakuwa uamuzi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, nimeona niliseme hili ili kuondoa taharuki ambayo watu walianza, walitaka kuianzisha. Benki Kuu imeshatoa taarifa ambayo ina-*clear* hiyo *doubt*. Nilitaka tu niongezee kwamba ni taasisi ambayo inaheshimika duniani na sisi kama nchi tutaendelea kuzingatia misingi hiyo na tumejipanga kutekeleza miradi kwa njia nyingi, zikiwemo za rasilimali, zikiwemo za ubia na Sekta Binafsi, zikiwemo za bajeti za Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kipengele kimoja. Ukienda kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge wameongelea kuhusu masuala ya uwajibikaji, masuala ya uadilifu, masuala ya uzembe na kadhalika. Ukienda kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 37, Mheshimiwa Rais anaanza kwa kusema, ninanukuu; "Tumezungumzia masuala mengi, ila msingi wa mafanikio yote haya ni utawala wa sheria, uadilifu na uwajibikaji katika ngazi kuanzia juu mpaka chini.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, ili kuhakikisha wananchi wananufaika na rasilimali za nchi pamoja na kupata huduma wanazostahili, tutaelekeza jitihada zetu kwenye mapambano dhidi ya rushwa, ufisadi, ubadhirifu, uzembe, ukosefu wa nidhamu

na maadili. Ni lazima tudhibiti wachache wanaotaka kuturudisha nyuma kwa kuendekeza maslahi binafsi”. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, na hii ni kauli nzito inayotoa uelekeo kuhusu tunafanya nini kwenye eneo hili. Ukienda kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 52(3), inasema: *“Katika utekelezaji wa madaraka yake, Waziri Mkuu atatekeleza au kusababisha utekelezaji wa jambo lolote au mambo yoyote ambayo Rais ataagiza kwamba yatekelezwe”.*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameelekeza haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoka kuongelea. Niwatoe mashaka, kwamba haya mambo mazito ambayo Mheshimiwa Rais ameyaelekeza kupitia hotuba yake hii yatakwenda kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaijua mianya ya maeneo haya ambayo Mheshimiwa Rais aliyabainisha. Mianya ya rushwa, mianya ya ubadhirifu, upotevu wa fedha, ninayajua. Fedha ya Serikali huwa inapotelea kwa kiwango kikubwa maeneo mawili. Ukikuta popote pale kuna fedha ya Serikali imepotea, yatakuwa kati ya hayo maeneo mawili; ama inapokusanywa ama kule inakotumika kwenye mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukifuatilia kwenye maeneo mengine yote kwenye sheria, yanayohusu kisheria, yanayohusu taratibu hizi yote yatakuwa yamekaa sawa. Sasa katika kutekeleza maelekezo haya ya Mheshimiwa Rais, ya kuweza kuhakikisha kwamba tunadhibiti mianya inayoweza ikasababisha wananchi wasipate mafanikio ...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninaongeza muda mpaka siku yetu itakapokwisha. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza haya kuweza kuhakikisha kwamba maelekezo ya Mheshimiwa Rais yanatekelezwa kwenye suala hili la udhibiti: tumeanza kufanyia kazi maeneo yale ambayo tunaona yanaweza yakawa

yanaacha mianya inayosababisha upotevu wa fedha; yanayoweza kusababisha baadhi ya watumishi wa umma, kutokuzingatia mambo ya maadili.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni kwenye sheria zetu: tulipotunga Sheria ya Maadili ya Utumishi wa Umma wakati ule tuliweka mkazo mkubwa kwa viongozi, inaitwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Waheshimiwa Wabunge, wanajaza hizo fomu pamoja na viongozi wengine. Pia, tunalo kundi lingine ndani ya utumishi wa umma ambalo lenyewe linajaza "Ahadi ya Uadilifu". Hizi fomu mbili zinatofauti kubwa.

Mheshimiwa Spika,Fomu ya Maadili, ina mambo mengi ya kuzingatiwa ambayo yanaweka alama za ufuatiliaji, atataja mali zake; wanaruhusiwa kufuatilia mali; wanaruhusiwa ku-*verify* nyongeza ya mali pamoja na mambo mengine. Hii nyingine ni "Ahadi ya Uadilifu" ambayo haimlazimishi sana mtumishi wa umma kutaja mali alizonazo ama nyongeza za mali, ama kubainisha kipato alichokipata.

Mheshimiwa Spika, nimeshatembelea Sekretarieti ya Maadili ya Utumishi wa Umma, kwa kazi aliyonituma Mheshimiwa Rais, nimekutana na taasisi yetu ya TAKUKURU. Katika kutekeleza hotuba hii nzito aliyoitoa Mheshimiwa Rais, nimeelekeza waangalie upya ile mianya ili tuweze kuziba hiyo mianya na kwa kuwa sasa hivi tupo kwenye dunia ya kidijiti hatuna hofu ya kwamba zile fomu zitakuwa nyingi, tumeona uangaliwe uwezekano wa kuanza kujaza fomu kwa watu wote wale ambao wapo kwenye maeneo ambayo yana viashiria vingi vya rushwa na yana vivutio vingi vya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli maeneo ya aina hiyo yenye ushawishi yanatofautiana na hata kama zamani ilikuwa hivyo kwa sasa mambo yanaenda yanabadilika. Ukitarajia kwamba Mbunge atahongwa rushwa kwenye jambo ambalo linafanyika kwa Afisa Madini anayetoa leseni, huko ni kuweka mtego eneo la tofauti na kile unachokiwinda. Ni dhahiri, kwamba yule anayetoa leseni atawashawishi sana wale wanaoshindania hiyo leseni kuliko mwakilishi huyu ambaye amekuja kuongea tu.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo, na wale wanaosimamia mikataba, Kamati zetu zile za Zabuni: zinapata ushawishi mkubwa zaidi kwa wale wanaoshindania hiyo kazi kuliko Naibu Waziri. Naibu Waziri anaweza akajaza tu hapa, hafanyi maamuzi; hata Waziri sehemu nyingine siyo Afisa Masuuli, anaweza asiwe na ushawishi wa kiwango kama yule ambaye yeye anakaa kuamua nani apewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa hatusemi kwamba hawa viongozi wengine watakuwa hawahusiki na mambo haya, tunataka tulenge pale ambapo pana ushawishi. Hivyo hivyo, hata kwenye kila ofisi, kwenye ofisi ileile panatofautiana ushawishi, hivi leo Mheshimiwa Rais, ameimarisha masuala ya uwazi kwenye masuala ya ukusanyaji. Kamishna Mkuu wa Mapato ameimarisha masuala haya, mapato yameongezeka, tena yameongezeka akiwa anakusanya kwa weledi, kwa kufuata kanuni na sheria kama ambavyo Mheshimiwa Rais alielekeza.

Mheshimiwa Spika, bado hii haiondoi kwamba wapo wale wanaoingiaingia vitamaa, wapo wanaoingiaingia vitamaa. Kama sheria itakuwa haimpimi ana nini na nini na nini kuanzia anapoingia, kuanzia anapofanya, ni rahisi kukuta watu wakawa wanagawana mapato na Serikali. Kwa hiyo, maeneo yote yale yanayoleta mianya ya aina hiyo tunataka tuongeze udhibiti. Tunataka tuongeze udhibiti katika maeneo ambayo yanaviashiria vya upotevu wa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii itatusaidia kuongeza mapato ya kuweza kutekeleza miradi ya maendeleo. Hivyo hivyo na kwenye uzembe: tumesema tutashughulika na wale walio wazembe na mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuwapa heshima wale watumishi wa umma wanaofanya kazi vizuri. Nchi hii imepiga hatua kwa sababu kuna watumishi wa umma wanaofanya kazi vizuri, wapo wengi. Wanaofanya kazi vizuri ni wengi, wengi ndiyo maana nchi inapiga hatua: Tuna watumishi wa umma wanaofanya kazi vizuri. Ndiyo maana kuna wagonjwa wanatoka nchi nyingine kuja kutibiwa Tanzania, kwa sababu tunao watumishi wa umma wanaofanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia humu kuna Wabunge vijana ambao ni wasomi tu, wamefundishwa na watumishi wa umma wetu hapahapa nchini, lakini tutashughulikia wale walio wazembe. Ndiyo maana tumetaka kila eneo kuwe na uwazi, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, ametoka kulisema hili tumekubaliana kuwe na uwazi kote kwa ajili ya ufuatiliaji wa masuala yanayohusu mambo ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi ikishabainishwa, Waheshimiwa Wabunge, tumeshaijua, fedha zimekuja katika wilaya yetu tusipewe tu taarifa ya Mfuko wa Jimbo. Mfuko wa Jimbo ni sehemu ndogo sana ya fedha za maendeleo zinazokuja kwenye wilaya zetu, ni sehemu ndogo inaweza ikawa shilingi milioni 40 au milioni 50, lakini wilaya ikawa imepokea shilingi bilioni 40 za maendeleo. Taarifa zake za utekelezaji wa miradi na fedha zinapoingia zote wawakilishi wakiwemo Wabunge; wakiwemo Waheshimiwa Madiwani waweze kujua. Tunataka uwazi huo ili kuweza kuongeza ufuatiliaji wa masuala ya kimaendeleo katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hotuba hii imetoa maelekezo na imetoa uelekeo na Wabunge katika kuchangia kwao wametuongezea nyenzo za utekelezaji wa uwelekeo huo. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, wote kwa hoja na michango yote yenye tija ambayo wameitoa katika mjadala. Niwahakikishie kwamba, Serikali wakati wote itazingatia maoni na ushauri mnaoutoa katika mipango na utekelezaji wa majukumu yake katika ustawi wa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeyazingatia yote na tutaendelea kupokea na mengine kuanzia Jumatatu mjadala wa ajenda itakayofuata ya mpango, tutaendelea kupokea ili kuweza kuboresha na kuzingatia utekelezaji wa hotuba hii ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wamechangia na kutoa ufafanuzi wa hoja nyingi zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge, lakini kwa ajili ya muda tu, hawajawasilisha hoja zote

ambazo zipo katika ofisi zao. Ninawahakikishia Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kutoa na taarifa zingine na kama nilivyosema kwa Waheshimiwa Mawaziri watakapotoa taarifa za utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais za siku 100 tutawaletea hizo nakala laini ili na wao wawe na taarifa kamili hizo kwa ajili ya ufuatiliaji lakini pia na mawasiliano ya mafanikio hayo kwa wanachi wanaowawakilisha.

Mheshimiwa Spika, nilihakikishie tena Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imepokea maoni na michango ya Waheshimiwa Wabunge ambayo ni sehemu muhimu katika kusaidia Serikali kutekeleza kikamilifu vipaumbele vilivyoainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, aliyoitoa hapa Bungeni. Tumetaja tu baadhi ya maeneo, maeneo mengine yanaendelea kutekelezwa na Serikali ipo kazini.

Mheshimiwa Spika, michango hii inathaminiwa. Michango ya Waheshimiwa Wabunge inathaminiwa sana na itafanyiwa kazi na kama ambavyo Waheshimiwa Mawaziri wamesema, tutaendelea kushughulikia hata zile kero ambazo wametoka kuzibainisha. Tunatambua maeneo ya miradi ambayo inatakiwa iongezewe kasi; miradi ambayo inatakiwa kuanza, Waheshimiwa Wabunge tumepokea hizo hoja na tumeendelea kukaa kila wakati kuhakikisha tunaratibu utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, taarifa za utekelezaji wake tutaendelea kuwapatia siku hadi siku ili kuweza kuhakikisha kwamba wanawajulisha wanachi wa maeneo yenu kuhusu hatua ambazo tutaendelea kuzichukua katika kutekeleza hoja hizo ambazo zinajitokeza katika maeneo yenu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa nimeyasema hayo, niruhusu sasa kukushukuru wewe pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti kwa kuongoza vizuri mjadala huu. Mmetusaidia kupata hoja za Waheshimiwa Wabunge na uchambuzi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Sasa nitawahoji, kuhusu hoja ya kuipokea hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa ufunguzi rasmi wa Bunge la Kumi na Tatu, tarehe 14 Novemba, 2025.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote wamesema ndiyo, hivyo Bunge limekubali na kuipokea hotuba ya Mheshimiwa Rais.

*(Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa Ufunguzi Rasmi wa Bunge la Kumi na Tatu, Tarehe 14 Novemba, 2025 Ilijadiliwa na Kupitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ninakushukuru sana Mkuu kwa hotuba nzuri, Mawaziri kwa majibu sahihi, lakini na Wabunge kwa michango ambayo ilikuwa na heshima na tija na ukweli kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amesema Dira ya 2025 mpaka 2050 inataka uwekezaji wa 70% kutoka *private sector*, wa ndani na wa nje; 22% zitachangiwa na Serikali, asilimia nane itachangiwa na taasisi za umma. Tuna kazi kubwa ya kufanya.

Ninamshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kutoa mkono wake kuomba amani kwenye Taifa letu na kwenye hotuba yake, kwenye ukurasa wa 12, ninaomba msome. Ninanukuu sehemu moja tu: "Sitachoka kuonesha tena mkono wa maridhiano." Haya ni maneno mazito sana kwa kiongozi wa nchi anayetaka amani, umoja na maendeleo ya Taifalake. Ni Rais huyu, ndiye

aliyerudisha wapinzani waliokimbia Tanzania kuja kufanya siasa Tanzania, haya huwa hatuyasemi. Yeye ndiye alitoa mkono wake ali-*extend an olive branch* kwa watu wote walioondoka Tanzania kurudi na kuja kujenga Taifa lao. Rais kama huyu lazima aenziwe, apendwe na tumwombee kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Bashiru, amenukuu ukurasa wa 10: "Uadilifu wa utendaji wa Serikali." Ninawahakikishia Bunge hili na Wabunge hawa na Kamati zetu za Kudumu za Bunge, zitaungana na Rais kuhakikisha kila hatua ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais, yatafuatwa na yatekelezwa kwa mujibu wa sheria na mikakati. *(Makofi)*

Nirudie tena, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, maelezo ya Spika kuhusu mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara kuhusu swali lake namba tisa kutokujibiwa kikamilifu.

Waheshimiwa Wabunge tarehe 27 Januari, 2026 katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Tatu; Mheshimiwa Mwita Waitara, Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, aliomba mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 79 na 56 Kanuni za Kudumu za Bunge 2025 kuhusu swali lake la msingi namba tisa kutokujibiwa kikamilifu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maombi hayo, Kiti kiliahidi kutoa mwongozo baadaye. Hata hivyo, kabla ya kutoa mwongozo huo, Mheshimiwa Waitara baada ya kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Madini kuhusu suala alilolalamika ameomba kuondoa maombi yake na mwongozo. Kutokana na maelezo hayo ya Mheshimiwa Waitara kuondoa maombi yake, Kiti hakitatoa uamuzi kuhusu mwongozo huo. Ilibidi kwa mujibu wa Kanuni lazima tufute hoja hii katika *Hansard* za kumbukumbu zetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kutakuwa na *Bonanza* litakalofanyika kesho Jumamosi tarehe 31 Januari, 2026. *Bonanza* hili litafanyika katika viwanja vya Shule vya Sekondari ya

John Merlini iliyopo Miyuji Jijini Dodoma. *Bonanza* litahusisha michezo mbalimbali ya burudani, mashindano ya timu ya watani wa jadi Simba na Yanga. Litaanza kwa maandamano yatakayoanzia Chuo cha Mipango Dodoma saa 12 asubuhi, mgeni rasmi katika *Bonanza* hilo atakuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba. Baada ya *Bonanza* hilo jioni kutakuwa na taafrija itakayoanza saa 12.30 jioni na kuendelea. Kaulimbiu ya *Bonanza* hili ni: “Umoja wetu ni nguvu yetu.” *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, humu ndani kuna Wabunge ambao wana uhitaji maalum: Kuna mmoja ana uhitaji wa kupata alama za vidole ajue tunafanya nini na ninamwona anapata shida sana kwa sababu kutwa nzima anatazama nyuma sababu ndiyo karibu ya ile *screen* ili apate kujua na anaelewa na nimemwona alivyoombewa dua Rais na Mheshimiwa Dkt. Bashiru, alinyoosha mikono, kwa hiyo nikajua anaelewa na anafahamu. Ninampongeza sana Mbunge wetu kwa namna anavyofuatilia, lakini ili maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kila mwananchi apate haki Katibu wa Mbunge, ameandaa utaratibu mpya utakaotumika Bunge lijalo *Insha Allah*. *(Makofi)*

Utaratibu huu wa *multimedia*, wahusika wote, ukibonyeza kitufe chako nitakuona unataka kuuliza swali, huna haja ya kuandika *text* tena, lakini na yeye atapata huduma bora ya uhakika wa taarifa na maneno yatakayosemwa ndani ya Bunge. Ninampongeza sana Mheshimiwa Katibu kwa kuyatekeleza maagizo haya ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Baada ya maneno haya, sasa ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.56 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 2 Februari, 2026, Saa Tatu Asubuhi)*